Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA NANE

## KIKAO CHA TISA - TAREHE 11 FEBRUARI, 2005

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILSHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU):**

Hati ya Uhamishaji Fedha Na. 1 ya Mwaka 2004/2005 *(Statement of Reallocation Warrant N0. 1 of 2004/2005).*

**WAZIRI YA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:**

Taarifa ya Mwaka ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania kwa Mwaka 2002/2003 pamoja na Hesabu za Mamlaka hiyo kwa Mwaka 2001/2002 *(The Annual Report of the Tanzania Meteorological Agency for the year 2002/2003 Including Final Accounts for the year 2001/2002).*

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA (k.n.y. MHE. JOHN S. MALECELA - MWENYEKITI WA KAMATI YA ULINZI NA USALAMA)**

Taarifa ya Utekelezaji wa Shughuli za Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama kwa Mwaka 2004.

**MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:**

Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Uanzishaji wa Mahakam ya Kadhi Tanzanai Bara.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 100

**Maeneo Maalum kwa Ajili ya Wafanyabiashara Ndogo ndogo**

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA (k.n.y. MHE. CHRISANT M. MZINDAKAYA)** aliuliza:-

Kwa kuwa kumekuwa na usumbufu mkubwa kwa wafanyabiashara ndogo ndogo, Wamachinga wa Dar es Salaam na katika Miji yetu Mikuu hapa nchini juu ya kukosa maeneo maalum au maduka kwa ajili ya kuendesha biashara zao:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba sasa ni wakati muafaka kwa Jiji la Dar es Salaam pamoja na Miji mingine Mikuu nchini kuchagua na kutenga maeneo maalum yanayofaa kwa ajili ya kujenga vibanda vya kisasa vya biashara kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo wadogo?

(b) Je, Serikali haioni kwamba suala la vijana wengi kukimbilia mijini na kuanza kujihusisha na biashara ndogo ndogo kunatokana na Serikali kukosa mipango thabiti ya kutumia nguvukazi ya vijana tulionao katika kuondoka kwenye umaskini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Chrisant Mzindakaya, Mbunge wa Kwela, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa na takwimu kwa kipindi kati ya mwaka 2000 na 2004, Halmashauri za Manispaa za Dar es Salaam na Jiji la Dar es Salaam, limekwisha kutenga maeneo maalum kujenga na kuimarisha vibanda vya kisasa vya biashara kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo wadogo kama ifuatavyo:-

(i) Ujenzi wa mabanda 232 kwa gharama ya shilingi bilioni 1.3.

(ii) Ujenzi na uwekaji wa maumbo ya biashara kwa gharama ya shilingi zaidi ya milioni 63.6.

(iii)Ujenzi na uimarishaji wa maeneo ya kufanya biashara kwa maana ya masoko na magulio ambazo zimetumika shilingi zaidi ya bilioni 13.672.

Mheshimiwa Spika, aidha, juhudi kama hizi pia zinaendelea kutekelezwa na Halmashauri nyingine hapa nchi kama ifuatavyo:-

- Manispaa ya Moshi kuchangia shilingi milioni 10 na kwa kushirikiana na wafanyabiashara imeweza kujenga vibanda 80 katika eneo la Bombambuzi na eneo la Nguvu Kazi.

- Manispaa ya Iringa imetenga na kujenga vibanda 245 vya biashara ndogo ndogo kwa gharama ya shilingi milioni 171.5

- Manispaa ya Mbeya imeimarisha masoko ya Soweto na Igawilo kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo wadogo kwa gharama ya shilingi milioni 65.

- Manispaa ya Arusha imetenga eneo la Suye kwa ajili ya shughuli za wafanyabiashara wadogo wadogo na kujenga miundombinu na kuweka huduma za maji na umeme kwa gharama za shilingi milion17.5.

- Manispaa ya Dodoma imetenga maeneo ya *Area A, C, D, E,* Chadulu, Chinangali, Bonanza, Chamwino, Uwanja wa Sabasaba na Stendi Kuu ya Mabasi kwa ajili ya shughuli za wafanyabiashara wadogo wadogo ambapo shilingi milioni 92.8 zilitumika.

- Manispaa ya Tanga imetumia zaidi ya shilingi milioni 64 kukarabati majengo, ujenzi wa masoko na kituo cha Taarifa za Biashara kwa wafanyabiashara wadogo wadogo.

Mheshimiwa Spika, juhudi zote hizi zinafanywa na Halmasharui kwa kushirikiana na wadau wake mbalimbali ikiwa ni pamoja na wafanyabiashara wadogo wadogo na kwamba haya yote kutokana na maamuzi halali yaliyopitishwa na kukubaliwa na mabaraza ya Halmashauri za Manispaa.

Aidha, Serikali kwa upande wake inatambua umuhimu na matatizo kuhusu biashara ndogo ndogo na kwamba hatua zinachukuliwa ili kuzifanya biashara hizo na shughuli nyingine za uzalishaji mali kutambuliwa kisheria na hivyo kuwawezesha wahusika kujiendeleza zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo haya ni dhahiri kwamba Serikali tayari imekwishaanza kuchukua hatua mbalimbali kwa ajili ya shughuli ndogo ndogo.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli tatizo la vijana kukimbilia Mijini lipo lakini hatuwezi kusema sababu pekee ni mipango mibovu. Suala hili linatokana kwa upande na matokeo ya ukuaji wa Miji yaani *Urbanisation* jambo ambalo linaigusa dunia nzima ambapo fursa za ajira na huduma mbalimbali za kiuchumi, kijamii na miundombinu zimejengeka na hivyo kuwa kivutio kwa vijana kuhamia Mijini na wakifika hapo baada ya kukosa ajira katika sekta rasmi, vijana wengi huamua kufanya biashara ndogo ndogo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inao utaratibu mzuri na endelevu wa kuandaa mipango, malengo, mikakati na Bajeti na hatimaye kuitekeleza, kuiratibu na kuifanyia tathmini. Aidha, kwa kupitia Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji, suala la

ajira la vijana la kuondoa umaskini linashughulikiwa kikamilifu. Kwa kuendelea kutenga maeneo ya kufanyia shughuli mbalimbali, kutoa mikopo kwa vijana, kushirikisha mashirika ya Kiserikali na asasi za binafsi mbalimbali kwa ajili ya kuwezesha kutoa mikopo kwa vijana. Lakini vile vile kuhakikisha kwamba sera ambazo zinatungwa na Serikali kama vile Sera ya Maendeleo ya Jamii, Sera ya Vijana, Sera ya Sekta ya Kilimo na na kadhalika zinatekelezwa ipasavyo.

Mwisho ni kujenga miundombinu kama barabara, masoko,simu, umeme na maji vijijini ili vijana waweze kufanya shughuli zao huko huko bila kulazimika kuja mijini.

**MHE. LUDOVICK J. MWANAZILA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuweza kuuliza swali hili moja tu la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri ametoa maelezo mazuri sana jinsi Serikali inavyopanga mipango yake kuwasaidia wananchi. Lakini mipango hiyo bado haitekelezwi vizuri na haswa ukiangalia kwamba fursa kubwa ya wananchi wengi ni katika kilimo na hicho kilimo ndicho ambacho kingeweza kuwaajiri wananchi wengi kwa kuwapatia fursa ya mikopo na misaada mbalimbali kama pembejeo, je, Serikali haikubaliani nami kwamba bado haijaweka nguvu ya kutosha katika kuwapatia mikopo vijana ambao wangeweza kubaki vijijini kufanya kazi ya kilimo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, tunakubali kwamba bado zinahitajika juhudi kubwa zaidi katika kujaribu kuwasaidia vijana hawa kutokana hasa na sekta ambazo ndio zina wigo kubwa zaidi la kazi. Lakini naomba tu niseme kwamba Serikali kwa kweli inalitambua ndio maana unaona juhudi nyingi sasa zinaelekezwa katika eneo hilo la kilimo. Ni matumaini yetu kwamba baada ya muda huenda hiyo kasi ya ongezeko la vijana kuja mijini litapungua.

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali dogo la nyongeza. Baada ya kumaliza uchaguzi mdogo wa Serikali za Mitaa, soko la Midizini ambalo lilikuwa likihudumia na kutoa ajira kwa vijana zaidi ya 200 lilivunjwa. Je, Serikali inaweza kutoa sababu ya msingi iliyopekea kuvunjwa kwa soko hilo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, mara zote Serikali inapochukua uamuzi fulani kwa kawaida huwa wamefanya utafiti wa kutosha, wamejiridhisha kwamba hatua hiyo itaweza kuleta maendeleo au nafasi au fursa nyingine ambazo zinaweza zikasaidia zaidi. Kwa hiyo, mimi nina uhakika kabisa Mheshimiwa Mbunge sidhani kama uamuzi huo ulitokea tu bila kuwepo hali fulani fulani zilizozingatiwa. Lakini pengine kwa kuwa unaweza kuwa na undani wa jambo hilo, si vibaya mkarejesha jambo hili katika vyombo vinavyohusika, kwenye Halmashauri au shughuli zingine za Serikali liweze tena kutazamwa kwa lengo la kuona tufanye nini.

**MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nikushukuru kwa kuniwezesha kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa katika swali la

msingi kilichokuwa kinazungumziwa ni biashara kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo wadogo. Kwa kuwa sio kila eneo linaweza likafaa kwa ajili ya biashara, je, Serikali itakuwa tayari kuweka utaratibu katika mipango yake kwamba inapopanga mipango miji, kukawa na maeneo ya katikati ambayo ni mazuri kwa biashara, ili Serikali ikaondokana na utaratibu huu wa sasa hivi wakufukuzana na hawa wafanyabiashara wadogo wadogo kila mara?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, unaloona linafanyika hivi sasa Mheshimiwa Mbunge ni matokeo ya matatizo yaliyojitokeza huko nyuma. Tunajaribu kufanya marekebisho katika mazingira halisi tuliyonayo hivi sasa na ndio maana wakati mwingine purukushani zinatokea lakini kama nilivyosema wakati natoa maelezo, tayari Halmashauri zimeelekezwa vizuri ndio maana unaona wanajaribu kutenga maeneo ndani ya eneo ambalo kwa kweli hapo awali halikuwa na uelewa wa namna ya kupanga maeneo haya. Lakini nataka nikuhakikishie kwamba kwa sasa maeneo yote ya miji ambayo yanaendelea kupimwa, suala hili limezingatiwa kikamilifu kabisa.

Na. 101

**Utengenezaji wa Barabara za Mji wa Sumbawanga**

**MHE. LEPHY B. GEMBE (k.n.y. MHE. PAUL P. KIMITI)** aliuliza:-

Kwa kuwa gharama za kutengeneza barabara za Mji wa Sumbawanga ni kubwa sana kutokana na hali ya udongo wa kichanga:-

Je, Serikali Kuu inasaidiana vipi na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuhakikisha kuwa Barabara za Mji huo zinajengwa kwa kiwango cha lami, ili kupunguza gharama za mara kwa mara za kukarabati barabara hizo kwa kuendelea kuweka vifusi ambavyo huondolewa baada ya mvua na kwa awamu ipi barabara za mji huo zitawekewa lami?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Paul Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga Mjini, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua hali ya uchakavu na pia haja ya kuimarisha barabara za mijini ili ziweze kumudu ongezeko la magari na kurahisisha usafiri mijini ukiwemo Mji wa Sumbawanga.

Mheshimiwa Spika, Mji wa Sumbawanga una barabara zenye urefu wa kilometa 346.55, kati ya hizo kilometa 33.55 ni za changarawe na kilometa 313 ni za udongo. Aidha, kilometa 32.4 za barabara za changarawe na kilometa 155 za barabara za udongo

zipo kwenye hali nzuri. Hivyo barabara hizo zinahitaji matengenezo ya kawaida ili zipitike wakati wote.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa gharama za kutengeneza barabara za udongo ni kubwa. Hii inatokana na sababu kubwa mbili, kwamba:-

(i) Wakati wa mvua magari hulainisha na kubandua sehemu ya juu ya barabara na hivyo sehemu iliyobanduliwa huchukuliwa na maji.

(ii) Wakati wa kiangazi chembechembe laini za udongo huondolewa barabarani kama vumbi na hivyo kuacha chembechembe kubwa au mawe.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hizo unene wa tabaka la juu la barabara hupungua na hivyo kupunguza uwezo wa barabara kubeba mizigo. Hali hii husababisha mashimo pindi magari makubwa yanayopita na kusababisha barabara kutopitika kirahisi. Inakadiriwa kwamba gharama ya kutengeneza kilometa moja ya barabara ya changarawe ni kati ya shilingi milioni 14 mpaka 17 na kilometa moja ya udongo ni kati ya shilingi milioni 9 na milioni 10.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua hayo Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na Serikali ya Norway chini ya Shirika lake la kutoa misaada la *NORAD,* tumeandaa programu ya Taifa ya kukarabati barabara za Wilaya na Miji hapa nchini. Programu hiyo inajulikana kama Programu ya Taifa ya Usafilishaji Vijijini *(National Rural Transport Programme)* ambayo itaanza mwaka huu kwa kufanya utafiti na majaribio na itagharimu shilingi bilioni 13 katika kipindi cha miaka miwili ya mwanzo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kipindi cha majaribio kumalizika, wahisani wengine wataombwa kushiriki ili katika kipindi cha kati ya miaka 10 hadi 15 inayofuata kilometa 15,000 za barabara ziwe zimejengwa kwa kiwango cha lami. Halmashauri ya Mji wa Sumbawanga itahusishwa katika programu hiyo.

Aidha, katika mpango huo tutafanya majaribio ya lami za bei nafuu *(Low Cost Seals),* kwa kuzingatia aina za udongo, mwinuko kutoka usawa wa bahari, idadi ya magari na kiwango cha mvua. Majaribio haya yatatuwezesha kupata lami za bei nafuu ambazo tutazitumia kwenye barabara zetu na hivyo kupunguza gharama za matengenezo.

**MHE. LEPHY B. GEMBE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa katika jibu lake la msingi Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba barabara za bei nafuu za kiwango cha lami zitawekwa kwenye programu ambayo itasaidia kupata fedha hizo kutoka kwa wafadhili, je, Mji wa Mpanda ikiwa ni mmoja kati ya Miji ambayo inatarajiwa kuwa ni Halmashauri za Miji. Je, huko tutakuwa katika programu ya kuwekwa katika kiwango hicho cha lami?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ninaloweza kusema tu ni kwamba tutakiane kila la heri turudi tena hapa na tubahatike kurudi kwenye nafasi hizi nitahakikisha Mpanda angalau kama mdau mkubwa na mimi nakuwemo. Lakini la msingi zaidi ni kwamba Mheshimiwa Lephy Gembe ni kwamba mpango huu ni wa nchi na utazingatia Halmashauri zote, lakini hasa hasa kwenye miji pamoja na Manispaa.

Kwa hiyo, *concentration* zaidi tunajaribu kusaidia zaidi maeneo ya mijini lakini, hata vijijini itakuwepo *component* hiyo. Kwa hiyo, katika hili tukishirikiana na watakao kuwepo nina hakika tunaweza tukafanikisha tu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri amesema mpango huu ni wa nchi nzima pamoja na Halmashauri za Kigoma na Geita, wote mtanufaika. Kwa hiyo, tunaendelea na maswali. *(Kicheko)*

Na. 102

**Stahili za Mtumishi Aliyefariki Akiwa Kazini**

**MHE. MARY D. WATONDOHA** aliuliza:-

Kwa kuwa mtumishi akifariki akiwa kazini, mjane wake anayo haki ya kulipwa marupurupu na stahili zake zote kutokana na utumishi wa marehemu mume wake au mke wake:-

(a) Je, inachukua muda gani kwa maslahi hayo kuwafikia wafiwa?

(b) Iwapo mjane anakosa malipo kutokana na uzembe wa mtumishi wa Hazina, je, mjane huyo aelekeze wapi malalamiko yake?

(c) Je, wajane wangapi wameweza kulipwa toka mwaka 1995 - 2000 na waliolipwa walifiwa lini?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, (UTUMISHI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maria Watondoha, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taratibu za mirathi, mtu anayeteuliwa rasmi kuwa msimamizi wa mirathi ya marehemu anapaswa kuwasiliana na aliyekuwa mwajiri wa marehemu akiwa na nyaraka zifuatazo:-

(i) Hati ya Kifo cha Marehemu au *Death Certificate.*

(ii) Fomu Na. I, II, III na IV zinazohusu maombi ya kuteuliwa kuwa msimamizi wa mirathi na kiapo cha mwombaji.

(iii) Vyeti halisi vya kuzaliwa warithi au *affidavit of birth.*

(iv) Hati ya kiapo cha kulea au kutunza watoto.

(v) Barua ya Mahakama ya kumteua rasmi mhusika kuwa msimamizi wa mirathi.

(vi) Picha mbili za kila mmoja yaani msimamizi wa mirathi.

(vii) Picha mbili za kila mmoja yaani msimamizi, mjane na watoto kama wapo.

Mheshimiwa Spika, mwajiri akisha pokea nyaraka hizo, huzituma Hazina kwa mujibu wa utaratibu wa awali kwa ajili ya kutayarishiwa malipo kutokana na mirathi.

Mheshimiwa Spika, uzoefu umeonyesha kuwa mara nyingi imekuwa ikichukua muda mrefu kwa msimamizi wa mirathi kukamilisha nyaraka hizo kutokana na matatizo au sababu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kuanzia tarehe 01 Julai, 2004 ambapo kwa mujibu wa Sheria ya Hitimisho la Kazi kwa Watumishi wa Umma Na. 2 ya mwaka 1999, nyaraka hizo zikishakamilika na kumfikia mwajiri, anazituma kwa Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma. Baada ya kuwasilishwa huko, malipo ya mhusika huanza kutayarishwa.

Mheshimiwa Spika, muda utakaotumika kukamilika kwa malipo hayo ya mirathi utategemea sana kasi ya msimamizi wa mirathi katika kukusanya nyaraka sahihi nilizozitaja hapo juu.

(b) Mheshimiwa Spika, iwapo msimamizi wa mirathi yeyote anaona kuwa mtumishi wa Hazina amesababisha kukosa malipo hayo kwa sababu mbalimbali, anashauriwa kupeleka malalamiko yake kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na iwapo hajapatiwa majibu au hajaridhika na jibu apelike malalamiko yake kwa Katibu Mkuu, Menejimenti ya Utumishi wa Umma au Mawaziri.

(c) Mheshimiwa Spika, siyo rahisi kwa sasa kutambua orodha ya wajane/wasimamizi wa mirathi ambao wamelipwa katika kipindi cha mwaka 1995 na 2000 kwa sababu utayarishaji wa malipo katika Kitengo cha Pensheni pale Wizara ya Fedha huwa haufanyiki kwa kuonyesha makundi ya walipwaji. Ili kupata orodha hiyo kwa uhakika tunahitaji muda zaidi kwa kushirikiana na watumishi wenzetu wa Wizara ya Fedha naahidi kuleta takwimu hizi kwa maandishi kwa Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, ningependa kulialifu Bunge lako Tukufu kwamba tunasisitiza waajiri wote kuwa wahakikishe kuwa masuala ya mirathi yanapewa kipaumbele sawa na majukumu mengine ili kuepusha malalamiko toka kwa wasimamizi wa mirathi.

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Mheshiamiwa Spika, kwa kuwa nina ushahidi wa mjane aliyefiwa toka mwaka 1997 ambaye msimamizi wake wa mirathi ametimiza masharti yote na mpaka sasa hajalipwa, je, Serikali ipo tayari kuchukua hatua ya kuhakikisha analipwa?

(b) Kwa kuwa toka mwaka 1997 mpaka leo mjane hakuwa na msaada na watoto wake wameshindwa kusoma, Serikali ipo tayari kubeba mzigo huo wa kusomesha watoto wa mjane huyu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Bora akuletee jina la huyo mjane. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, (UTUMISHI):** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Maria Watondoha, kwa maswali yake mawili, kwanza kama ana ushahidi naomba aniletee jina la mjane na Serikali itahakikisha kwamba analipwa na pili Serikali kuchukua mzigo wa kusomesha watoto wake kwa kweli haitaweza, kwa sababu mpaka sasa hatujui ni nani amesababisha kuchelewa huko kulipa mafao haya na nina hakika ndugu wa marehemu watasaidia na jamii na hakika ina mpango wa kusaidiana wakati kuna matatizo kama hayo.

**MHE. MONICA N. MBEGA:** Mheshimiwa Spika, asante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa ucheleweshaji huu wa malipo unatokana na utaratibu mzima wa matayarisho ya malipo hayo ambayo unahusisha Wizara nne tofauti. Kwa maana Ofisa aliyefariki, pili Wizara ya Fedha, tatu Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba, nne Ofisi ya Ukaguzi.

Je, Serikali itakubaliana nami kwamba ni vizuri kuanzia sasa Wizara ya Utumishi ikasimamia mabadiliko ya Sheria ili yaletwe tubadilishe Sheria inayohusika na mirathi ili malipo ya mtumishi yule yafanywe wakati alipofariki au mke alipofariki? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, (UTUMISHI):** Mheshimiwa Spika, Serikali kupita sera zake mbalimbali na Sheria ambazo tumezipitisha hapa Bungeni, imejitahidi sana kupunguza urasimu ndani ya Serikali na kwa hiyo, baada ya Sheria hizo kupitishwa ni kweli kwamba sasa mambo yatabadilika lakini kubadilika kwa mambo huwa yanachukua muda.

Mheshimiwa Spika, nina hakika sasa kutakuwa na ufanisi zaidi katika ulipwaji wa mafao ya marehemu kwa ndugu zake. Naomba tuwe na subira lakini nawahakikishia kwamba tutajitahidi kama utumishi kuratibu kwamba haya mambo yasichukue muda mrefu kwa sababu kwa vyovyote vile Ofisi ya Rais, Utumishi haiwezi ikakaa na fedha na kwa hivyo ni lazima Wizara ya Fedha iendelee kulipa mafao hayo.

Na. 103

**Mikataba ya Wawekezaji na Serikali**

**MHE. BAKARI SHAMIS FAKI** aliuliza:-

Kwa kuwa wawekezaji wengi hawaheshimu mikataba waliyowekeana na Serikali kwa kupitia mashirika waliyokabidhiwa na kwa kuwa *PSRC* wameajiri kampuni ya kukusanya madeni kutoka kwa wawekezaji wasiolipa.

(a) Je, Serikali imeshawahi kutoa onyo kali kwa wawekezaji wanaobeza mikataba waliowekeana na Serikali?

(b) Je, *PRSC* wamekusanya fedha kiasi gani kutoka pale walipoajiri kampuni ya kukusanya madeni kutoka kwa wawekezaji wasiolipa madeni yao?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mbunge wa Ole, lenye sehemu mbili (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa baadhi ya wawekezaji wanashindwa kutekeleza mikataba ya mauzo waliyowekana na Serikali, aidha, kwa kushindwa kulipia gharama za mauzo au kushindwa kutekeleza mipango ya uwekezaji katika mashirika hayo. Serikali katika kuhakikisha kuwa wawekezaji wa mashirika hayo wanatekeleza mikataba ya mauzo ikiwa ni pamoja na kulipia gharama za ununuzi wa mashirika hayo imechukua hatua mbalimbali zikiwemo:-

(i) Kuongeza vifungu katika mikataba hiyo vinavyoipa Serikali nguvu ya kisheria kutengua mikataba ya mauzo kwa kuwanyang'anya wawekezaji watakaoshindwa kulipia gharama za mauzo au watakaoshindwa kutekeleza mipango ya uwekezaji katika mashirika yaliyonunuliwa.

(ii) Kuwafanyia uchambuzi yakinifu wawekezaji wote wanaoonyesha nia ya kuwekeza katika Mashirika ya Umma ili kubaini historia yao katika uwekezaji, uwezo wao kifedha, kiteknolojia, ujuzi na uzoefu katika shughuli hizo endapo wawekezaji wameeleza kuwa na uzoefu katika nyanja hiyo sehemu nyingine duniani.

(iii) Kuwahimiza, kutoa maonyo na kuwakumbusha wawekezaji kupitia barua, majarida na matangazo mbalimbali umuhimu wa kutekeleza makubaliano yaliyomo kwenye mikataba ya mauzo ili kuepuka adha zinazotokana na kutotekeleza mikataba hiyo.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imeajiri makampuni kumi ya kukusanya madeni ambayo yameweza kukusanya jumla ya shilingi bilioni 2,805.3 kati ya kipindi cha Julai, 2001 hadi Desemba, 2004.

**MHE. BAKARI SHAMIS FAKI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri kakubali

kwamba kampuni imekusanya zaidi ya shilingi tilioni moja. Swali je, fedha hii iko wapi na inatumika namna gani na kwa idhini ya nani?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Spika, fedha zozote zinazopatikana katika utaratibu wa ubinafsishaji pamoja na madeni yanayokusanywa na makampuni haya kwa maagizo ya Tume ya Kurebisha Mashirika ya Umma ni fedha zinazoingia Serikalini na hata tukiangalia utaratibu wa Bajeti za Serikali tunazoziweka yako maeneo mengine yanayoonyesha mchango wa Mashirika ya Umma na fedha zinazopatikana huko katika Bajeti ya Serikali.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ambaye ameeleza uzoefu wake, lakini kuna tatizo moja limejitokeza kwamba kuna baadhi ya wawekezaji, kwa mfano, hoteli ya pale Dar es Salaam, *Royal Palm* ambayo haijamaliza mkataba wake wa kusamehewa kodi, inabadilishwa majina, sasa hivi inaitwa jina lingine anauziwa mfanyabiashara mwingine inaanza *Sheraton, Royal Palm* halafu itakuja kuwa *Pawa Palm.* Sasa utaratibu huu ni vipi unachukuliwa hatua gani watu kama hao? *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Spika, kama tunavyosema siku zote hapa Bungeni, msamaha wa kodi hapewi mnunuzi anayenunua mradi ule au hoteli ile, msamaha wa kodi unatolewa kwa mradi wenyewe. Kwa hiyo, hata mnunuzi mwingine akija kwa sababu mradi umeshapewa msamaha wa kodi hakuna tena utaratibu kwamba mnunuzi yule mpya atalipa atasamehewa kodi ilo la kwanza.

Lakini la pili utaratibu huu wa kufuta kodi kwa maana ya *Tax Holdays* Serikali ilikwisha usitisha toka Desemba, 1997. Kwa hiyo, hata kama *Royal Palm* itabadilika kuwa *Pawa Palm* hautaweza kulipa kodi hizo. *(Kicheko)*

Na. 104

**Chama Cha Ushirika Mara *(Mara Cooperative)***

**MHE. TEMBE K. NYABURI** aliuliza:-

Kwa kuwa Vyama vya Ushirika vilianzishwa kisheria na Mkoa wa Mara ulikuwa na Chama cha Ushirika *(Mara Cooperative)* ambacho kilifilisika wakati kikidaiwa na wakulima na Vyama vya Msingi mamilioni ya fedha, na kwa kuwa Serikali ilikabidhi mali zilizobaki na madeni kwa mfilisi na iliwaahidi wananchi kushughulikia madai yao na kuyatatua:-

Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusu madai ya wakulima wanaodai fedha zao za miaka mingi na watarajie nini sasa?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Tembe Kerenge Nyaburi, Mbunge wa Bunda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Chama Kikuu cha Ushirika cha Mkoa wa Mara yaani *Mara Cooperative Union* kilifilisika mwaka 1996 kama alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge kikiwa kinadaiwa na wakulima kupitia Vyama vyao vya Msingi kiasi cha shilingi 241,917,896/= zilizotokana na mauzo ya mazao.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwepo kwa madai haya, pia wakulima kupitia Vyama vyao vya msingi wanadaiwa na Chama Kikuu kiasi cha shilingi 1,275,145,598/= kutokana na upotevu wa fedha za mazao, kutorejesha mikopo ya pembejeo na huduma nyinginezo walizopatiwa na Chama kikuu cha *Mara Cooperative.*

Mheshimiwa Spika, utaratibu unaotakiwa kufuatwa wakati mfilisi anapofilisi Chama cha Ushirika ni pamoja na kuuza mali za chama, kukusanya madeni kutoka kwa wadaiwa mbalimbali na kisha kuwalipa wadai kwa kutoa kipaumbele cha kulipa madeni ya Serikali au Taasisi zake, kulipa mafao ya watumishi na mwisho kulipa wadai wa mikataba mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1997, wakulima na hasa wanaushirika wa Mkoa wa Mara kupitia Vyama Vikuu vya *Mara Farmers,* Tupendane, Victoria na Tarime viliiomba Serikali kusitisha zoezi la kuuza viwanda vya kuchambulia pamba vilivyokuwa mali ya *Mara Cooperative Union (1984) Ltd.* kwa utaratibu wa mfilisi hadi hapo vyama vya Ushirika vitakapojiimarisha na kuwa tayari kuvinunua. Ombi hili lilikubaliwa na Serikali.

Viwanda hivyo vinavyohusika ni vya Ushashi, Kibara, Mugango na Tarime. Katika hatua za awali za kuimarisha uwezo wa *Union* hizo iliundwa Kampuni iliyoitwa *Cotton Industry Company (COICO)* kwa ajili ya kununua viwanda hivi. Hata hivyo *COICO* ilishindwa kujiendesha na hivyo kushindwa kupata fedha za kununulia viwanda hivyo hadi sasa. Aidha, Vyama Vikuu Mkoani Mara vimeendelea kudhoofika zaidi kiuchumi hali inayohitaji mkakati mahususi wa kuviimarisha ambao utatekelezwa mwaka huu wa 2005 chini ya mpango kabambe wa mageuzi na modenaizesheni ya Ushirika.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na uongozi wa Mkoa, Wilaya na Mashirika yasiyo ya Kiserikali, Shirika la Maendeleo la Kanada linaloshoghulikia uendeshaji wa *SACCOS (DID), Swedish Co-operative Centre* na *SIDA,* wamehamasisha wakulima kuunda upya Vyama vya Msingi vya mazao na Vyama vya Akiba na Mikopo. Uundaji huo mpya wa Vyama vya Ushirika vya Msingi vilivyo imara utawawezesha Vyama vya Ushirika hivyo kupata mitaji na kugharamia shughuli zao na hatimaye kulipia kwa mpango mahususi, viwanda vilivyo chini ya Mfilisi.

**MHE. TEMBE K. NYABURI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ninalo swali moja la nyongeza kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Waziri katika jibu lake la msingi amesema kwamba wakulima wanadai zaidi ya shilingi milioni 200. Wakati huo huo chama kabla ya kufilisika kilikuwa kinawadai wakulima hao zaidi ya shilingi bilioni 1. Sasa Serikali itakuwa tayari kufanya uhakiki upya? Kwa sababu kuna baadhi ya wakulima wa Vyama vya Ushirika ambavyo walikuwa hawadaiwi na Chama kile cha Ushirika, ili wale ambao walikuwa hawahusiki na kudaiwa na Chama kile cha Ushirika waweze kupata haki yao ya msingi?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Tembe Nyaburi, Mbunge Bunda, kama ifuatavyo:-

Ni kweli nimesema kwamba wakulima wanadai *Mara Cooperative* kiasi cha shilingi milioni 149 na wakati huo huo wakulima kupitia vyama vyao vya msingi wanadaiwa kiasi cha shilingi bilioni 1. Sasa zoezi la kuhakiki nani anadaiwa na nani hadaiwi, zoezi hilo lilishaanza kutekelezwa na Serikali na sasa hivi utaratibu huo wa kuchambua takwimu zote hizo ili kuhakiki ni nani anadaiwa na nani hadaiwi linafanyiwa kazi na ofisi yangu.

Mheshimiwa Spika, lakini hata hivyo kama nilivyosema kwamba hata kama itajulikana kwamba kuna watu wengine ambao hawadaiwi. Bado zoezi la kuwalipa hawa wakulima litakuwa gumu kwa sababu mali ambazo zilitakiwa ziuzwe ili mfilisi aweze kuwarejeshea hawa zitakuwa bado hazijauzwa. Hata kama zingekuwa zinauzwa utaratibu nilioueleza wa kwamba zinafuata kwanza Serikali na Taasisi zake mpaka wakulima mmoja mmoja waje wafikiwe, inawezekana kabisa kwamba wakulima wanaweza kuwa na haki ya kudai. Lakini mpaka zoezi litakalokuwa linatekelezwa kufuata utaratibu wa mfilisi likamilike ndio wanaweza wakalipwa.

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuweza kunipa nafasi niulize swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize swali moja la nyongeza. Kwa sababu Serikali hii iliwahi kutoa tamko mwaka 2000 kwamba madeni ambayo wakulima wanaidai *Mara Cooperative Union* yanashughulikiwa na yatalipwa mapema. Sasa leo ni miaka mitano baadaye na kauli ya Waziri ndio hii tunayoisikia.

Je, ni nini kinapelekea kupata kauli mbili ambazo zinagongana?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ibrahimu Marwa, Mbunge wa Musoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kilichosemwa kwa ujumla kwamba madeni ambayo yalikuwa wakulima wanadai yalikuwa yanachambuliwa, kama nilivyoeleza katika jibu la nyongeza hapa ambalo nilikuwa najibu kwamba yanahakikiwa ili yaweze kulipwa. Lakini vile vile nimejibu katika swali la msingi kwamba wakati zoezi la mfilisi linaendelea, wakulima

hao hao kupitia vyama vyao waliomba kwamba mali za *Mara Cooperative* zisiuzwe na kama zingekuwa zimeuzwa mali zile kwa utaratibu nilioueleza tamko hilo lingeweza likatekelezwa.

Lakini kwa sababu waliiomba Serikali kwamba vile viwanda visiuzwe wanakusanya nguvu ili waweze kuvinunua wenyewe, basi Serikali iliwakubalia kama ilivyo kawaida Serikali yetu ni sikivu na mpaka sasa tunavyosema kwamba ombi lao bado liko pale pale linaheshimiwa, viwanda vile havijauzwa. Kwa hiyo, mpaka hapo viwanda hivyo vitakapotafutiwa ufumbuzi wa kununuliwa ndipo zoezi la kuwalipa hao wakulima linaweza likafanyika.

Na. 105

**Mauzo ya Pamba**

**MHE. ISAAC M. CHEYO:** Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye hotuba yake Bungeni alitoa agizo kuwa kila mkulima wa pamba aliyeuza pamba na kupunjwa shilingi 25 kwa kilo atarejeshewa fedha hizo; na kwa kuwa wakulima wa pamba waliopunjwa wamejiorodhesha kupita kwa watendaji wa vijiji lakini hadi sasa fedha hizo hazijalipwa na hakuna dalili zozote za kulipwa fedha hizo:-

(a) Serikali inasema nini kuhusu madai haya ya wakulima wa pamba na hasa wale wa Bariadi Magharibi?

(b) Kama Serikali haiwalindi wanunuzi wa pamba binafsi, je, kwa nini isitumie mamlaka yake kuwalazimisha hao wanunuzi binafsi wawalipe wakulima hao?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Isaac Cheyo, Mbunge wa Bariadi Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tarehe 30 Julai, 2004 Serikali ilitoa tamko kwamba bei ya pamba mbegu ya msimu wa 2004/2005 itaboreshwa kutoka shilingi 250/= kwa kilo ya pamba ya daraja la kwanza hadi shilingi 275/= kwa kilo. Hatua hii ilichukuliwa baada ya majadiliano na maafikiano yaliyofikiwa baina ya Serikali na wadau wa zao la pamba kufuatia kuporomoka kwa ghafla kwa bei ya zao hilo katika soko la dunia. Baada ya tamko hilo, Serikali kupitia Bodi ya Pamba iliagiza kwamba ifikapo tarehe 15 Oktaba 2004, Halmashauri za Wilaya zinazohusika lazima ziwe zimewasilisha takwimu za wakulima waliouza pamba yao kwa bei ya shilingi 250/= ambao ndio walistahili kulipwa nyongeza ya shilingi 25/= kwa kilo.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 26 Januari, 2005 Wilaya zilizowasilisha takwimu za mapunjo ya bei kwa wakulima ni tisa tu kati ya Wilaya 18 zilizotakiwa kufanya hivyo. Wilaya hizo ni Biharamulo, Sengerema, Misungwi, Bunda, Musoma, Maswa, Bukombe, Igunga na Iramba.

Mheshimiwa Spika, Wilaya nyingine nne yaani Kahama, Shinyanga, Magu na Kwimba ziliwasilisha taarifa zao lakini taarifa hizo zilikuwa na kasoro mbalimbali kama vile kukosekana kwa tarehe za kuuzia na majina ya wanunuzi kutotajwa. Kwa hiyo, Wilaya hizi zimekwishaelezwa kurekebisha kasoro hizo. Wilaya nyingine tano ambazo bado hazijawasilisha takwimu zake za mapunjo ya bei kwa wakulima ni pamoja na Meatu, Kishapu, Geita, Serengeti na Bariadi Wilaya anayotoka Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Pamba Tanzania ilikwishawaagiza wanunuzi wa pamba tangu tarehe 21 Desemba 2004, kuwalipa wakulima kutoka Wilaya zile ambazo zimewasilisha taarifa kamili za mapunjo. Malipo hayo yalitakiwa yawe yamefanyika kabla ya tarehe 31 Januari 2005. Hata hivyo utekelezaji wake umechelewa kwa sababu wanunuzi wameomba wapewe muda ili waweze kufanya malinganisho ya takwimu zilizowasilishwa na Halmashauri na zile zilizoko kwa wanunuzi. Zoezi hili limeanza kufanyika na linatarajiwa kukamilika ifikapo tarehe 15 Februari, 2005.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi za Bodi ya Pamba kufuatilia taarifa kutoka katika Wilaya ambazo hazijaleta taarifa zao, ninawaomba Waheshimiwa Wabunge wanaotoka katika Wilaya tano za Bariadi, Meatu, Kishapu, Geita na Serengeti wazihamasishe Halmashauri za Wilaya zao ziwasilishe haraka takwimu za mapunjo ya malipo ili wakulima wa pamba kutoka katika maeneo hayo walipwe haki zao mapema.

**MHE. ISAAC M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, kwa kufuatana na taarifa ambazo mimi ninazo na hii ni Kata moja tu kati ya Kata 26 za Bariadi, hawa wananchi walitimiza wajibu wao wakajiorodhesha na wakapeleka kule ambako kunahusika na tangu tarehe 6 Oktoba walishawasilisha orodha hiyo tayari kwa kungojea malipo.

(a) Sasa wale ambao bado mpaka sasa Mheshimiwa Waziri anavyosema kwamba *TSMB* hawajapokea orodha ya hawa watu sasa waliosababisha uzembe yeye anawachukulia hatua gani?

(b) Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Waziri Mkuu alitaja pia shilingi 15,000 ya pembejeo ambayo inatakiwa iingizwe kwenye kitabu. Tatizo ambalo linatokea sasa ni kwamba kama mtu kwenye kitabu chake ameandikiwa shilingi 50,000 kwa ajili ya pembejeo, anapewa pembejeo ya shilingi 20,000, shilingi 30,000 inabaki mle na kitabu kinafutwa. Je, huo sio wizi na Serikali inawachukulia hatua gani hawa watu wanaowapunja watu kwa makusudi?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Isaac Cheyo, Mbunge wa Bariadi Magharibi, kama ifuatavyo;-

Mheshimiwa Spika, hapa mimi nilichokuwa naeleza chombo kinachotakiwa kiwasilishe taarifa ni Halmashauri ya Wilaya. Sasa Kata moja iliwasilisha basi limewasilishwa Wilayani na kwa hiyo, kinachotakiwa kwamba takwimu hizo zikusanywe

katika Wilaya yote ziliwasilishwe Bodi ya Pamba ili Bodi ya Pamba iweze ikaelekeza ili waweze kuwalipa wanunuzi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nilichosema nikasema kwamba basi kwa Wilaya hizi ambazo bado hazijakamilisha hizi takwimu, zifanye hivyo haraka na wakulima waweze wakalipwa.

Mheshimiwa Spika, sasa hatua gani tunawachukulia? Nimeomba hapa kwamba tushirikiane kwa sababu hizi Halmashauri za Wilaya ndio huko huko ndio tunakotoka sisi. Kwa hiyo, mtu wa kujua kwa uhakika kabisa kwamba ni nani kachelewa? Kata gani imecheleweshа? Nadhani ni pamoja na Mheshimiwa Mbunge kwa sababu yuko kule karibu. Kwa hiyo, hatukuweza kuchukua kama ni kuhimiza au kufanya nini, kusema kweli ni kwa Halmashauri ya Wilaya inayokuwa inahusika.

Mheshimiwa Spika, la pili juu ya utaratibu wa kukata hiyo shilingi 15,000 kwa ajili ya pembejeo. Tulipokuwa tunafanya makubaliano hapa juu ya utaratibu wa kutoa vipengele mbalimbali kwenye *costing,* tulikubaliana hili kwamba vile vile liingizwe kwenye takwimu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama utendaji unafanya kinyume na yale maelekezo tuliyokuwa tumeyafanya, basi itakuwa ni jambo zuri tupewe taarifa rasmi ili tuweze kujua kwamba kuna mapungufu yanayofanyika. Kinyume cha hivyo itakuwa ni vigumu kwetu kujua kwamba yanafanyika mapungufu haya.

Na. 106

**Ukarabati wa Sehemu za Barabara ya Mbeya - Mkiwa**

**MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilikwishaeleza nia yake ya kujenga barabara ya Mbeya, Makongolosi, Rungwa, Itigi hadi Mkiwa kwa kiwango cha lami; na kwa kuwa katika awamu ya kwanza kuanzia Mbeya - Makongolosi tayari imeshafikia hatua ya kufanyiwa usanifu.

Je, Serikali ina mipango gani kwa kipande kilichosalia katika kukifanyia upembuzi yakinifu?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ismail Iwvatta, Mbunge wa Manyoni Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sehemu ya barabara ya Mbeya - Makongolosi yenye urefu wa kilometa 115 inafanyiwa usanifu wa kina na kampuni ya *BCEOM* kutoka Ufaransa kwa kutumia fedha za ndani (Tanzania). Mkataba baina ya Serikali na kampuni hiyo ulitiwa

saini tarehe 22 Januari, 2004 kwa gharama ya shilingi 780,264,453.02 na kazi za usanifu wa kina zinatarajiwa kukamilika katika kipindi cha miezi kumi na mbili ifikapo mwezi Februari 2005.

Aidha, barabara ya Makongolosi - Rungwa - Itigi - Mkiwa yenye urefu wa kilometa 396 inatarajiwa kufanyiwa usanifu wa kina pamoja na ujenzi wa kiwango cha lami kwa awamu kutegemea upatikanaji wa fedha. Katika mwaka wa fedha wa 2002/2003 na 2004/2005 jumla ya shilingi milioni 700 zilitengwa kwa ajili ya usanifu na maandalizi ya kuitisha zabuni za ujenzi wa sehemu ya Mbeya - Makongolosi wakati huo huo tunatafuta fedha kwa sehemu nyingine.

Mheshimiwa Spika, aidha, pamoja na jitihada zilizoainishwa hapa juu, Wizara yangu itaendelea kuifanyia matengenezo barabara yote na kufanya mazungumzo na wafadhili ili kuona uwezekano wa ujenzi wa barabara hii kugharamiwa kwa pamoja kati ya Serikali ya Tanzania na wafadhili mara baada ya kazi za usanifu kukamilika.

**MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Lakini pili naomba nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na Wizara yake kwa majibu mazuri sana yanayoleta matumaini. Pamoja na juhudi na kazi nzuri sana inayofanywa na Wizara yake ya kuifanyia matengenezo hasa kipande cha kutoka Rungwa mpaka Kiluvya ambayo ni kilometa 89.

Je, Wizara yake itakuwa tayari kusaidia kufanya matengenezo kwa kipande kilichobaki cha kutoka Kilumbya kuja Itagata ambacho ni kama kilometa 60 baada ya sehemu nyingine zote kufanyiwa kazi vizuri na Wizara yake pamoja na wataalam wake?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ningependa kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ismail Iwvatta, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, matengenezo haya ya barabara hasa dakika hizi za sasa hivi naogopa sana kuziwekea ahadi kwa sababu Bajeti imebana kabisa kama tulivyoipitisha hapa. Kwa hiyo, tunajitahidi kwa uwezo wetu wote na ninajua kuna kisehemu Mheshimiwa Mbunge ameshawahi kukizungumzia kabla hata ya kufika hapa Bungeni anafuatilia sana barabara hii. Sehemu ya Kilumbya hadi Itagata nimezungumza na *Regional Manager* na nimemuomba atuletee taarifa tuone yeye kwa uwezo wake anaweza kusaidia vipi, lakini sasa hivi hapa Bungeni sitaki kuahidi kwamba nitatengeneza. Lakini nitajihidi.

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Kwa kuwa barabara anayoizungumzia Mheshimiwa Ismail Iwvatta, ni barabara ile ile ambayo inakwenda moja kwa moja mpaka Singida Mjini, inakwenda kutoka Singida hadi Katesh hadi Babati hadi Mkoa wa Arusha. Ni lini kwa ahadi zote nilizozisikia Serikali itawahakikishia wananchi hao kwamba barabara hii sasa inawekwa lami ili tusonge mbele?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ningependa kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, kama ifuatavyo:-

Serikali imeahidi sana barabara nyingi tu na bahati nzuri hii barabara anayozungumzia Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, inakwenda mpaka Katesh mpaka kule Manyara inapata bahati kwa sababu huu ni mkoa mpya na huwa unashughulikiwa maalum na maombi yake ni maalum kwa hiyo, kitu ambacho ninaweza kuahidi hapa kwa wananchi hawa ni kwamba nawaomba wawe wavumilivu waangalie mpango wa Serikali katika Mkoa huu mpya.

Na. 107

**Mahitaji ya Umeme Vijijini**

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI** aliuliza:-

Kwa kuwa mwaka jana Shirika la Umeme Tanzania *(TANESCO)* lilikabiliwa na tatizo la upungufu wa nishati ya maji hivyo kupelekea Bunge kupitisha Bajeti ndogo ya ziada ili kuliwezesha shirika liweze kutoa huduma ya umeme vijijini iliathirika sana kutokana na kusitishwa kwa shughuli hizo kwa ule mradi wa umeme wa Lamadi kwenda katika Wilaya ya Magu kwenda Nyashimo na kisha Lamadi kwenda Mkula Hospitali na kinu cha kuchambulia Pamba cha Ngasamo ambavyo ni vituo muhimu kwa maendeleo ya jamii na kukuza uchumi wa nchi:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuvipatia vijiji vya Kalemera, Nyamikoma, Kabita na Nyakaboja umeme kwa kuzingatia kuwa Serikali inatambua kabisa umuhimu wa biashara na vitega uchumi vilivyopo katika mtandao huo wa barabara kuu ya Mwanza - Musoma - Nairobi zikiwemo hoteli za *Speek Bay?*

(b) Kwa kuwa Serikali ilishaahidi Bungeni kutekeleza mradi huo, ni lini miradi hiyo ukiwemo ule wa Lamadi - Mkula - Ngasamo utatekelezwa?

(c) Je, Serikali haioni kuwa pia iko haja ya kupunguza gharama za kuunganisha umeme majumbani pamoja na ankara za umeme ili kuwawezesha wananchi kumudu kuweka umeme majumbani mwao na kumudu kuitumia nishati hiyo ili kuokoa uharibifu wa mazingira unaosababishwa na ukataji wa miti kwa ajili ya mkaa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI (k.n.y. WAZIRI WA NISHATI NA MADINI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, noamba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, Mbunge wa Busega, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mradi wa kupeleka umeme kijiji cha Nyamikoma kutokea kijiji cha Nyashimo umo kwenye programu itakayofadhiliwa na Benki ya Dunia pamoja na Serikali ya Tanzania ijulikanayo kama *Energising Rural Transformation (ERT)* na

utekelezaji wake unatarajiwa kugharimu shilingi milioni 230 na utaanza mara baada ya taratibu za kupata fedha zitakapokamilika.

Vijiji vya Kalemera, Kabita, Nyakaboja pamoja na hoteli ya *Speek Bay* vinatarajiwa kuingizwa kwenye programu hiyo katika awamu ya pili ya *ERT* ambayo itaanza baada ya taratibu za fedha za utekelezaji wa mpango huo kukamilika.

(b) Mheshimiwa Spika, mradi wa kupeleka umeme vijiji vya Mkula pamoja na Hospitali ya Ngasamo na kinu cha kuchambulia pamba kutokea Mji wa Lamadi pia umo kwenye programu ya *ERT* na utekelezaji wake unatarajiwa kugharimu shilingi milioni 680 na utaanza baada ya fedha kupatikana.

(c) Mheshimiwa Spika, ili kuwasaidia wananchi kumudu kuweka umeme majumbani mwao, Serikali kwa kushirikiana na *TANESCO* wamepanga utaratibu mpya wa ulipaji wa gharama za *service line* kwa awamu kuanzia Januari, 2005 ambapo ukiacha wateja wa huduma za waya nne *(three phase),* wateja wa huduma ya waya mbili *(single phase)* watakuwa na uhuru wa kulipa gharama kwa njia tatu tofauti kama ifuatavyo:-

(i) Njia ya kwanza ni kulipa kwa utaratibu ambao umekuwa ukitumia huko nyuma wa kulipa gharama zote mara moja.

(ii) Njia ya pili ni ya kulipa gharama katika awamu zenye kiwango sawa ndani ya kipindi cha miezi mitatu.

(iii) Njia ya tatu ni ya kulipa gharama katika awamu kumi na mbili zenye kiwango sawa ndani ya kipindi cha mwaka mmoja.

Mheshimiwa Spika, mpango huu maalum umewekwa ili kuwasaidia wananchi ambao hawana uwezo wa kulipia gharama za umeme kwa mara moja, kumudu malipo hayo kwa awamu *(instalments).* Kwa vile utaratibu huu ndio unaanza, *TANESCO* wameagizwa watoe mwongozo unaoeleweka kwenye ofisi zake Mikoani na Wilayani.

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri, napenda kuipongeza Serikali kwa mipango mizuri na kuweza kufanikisha shughuli hizi kufanyika vijijini. Lakini pamoja na pongezi, napenda kuuliza kwamba, kwa kuwa bado gharama za umeme ni kubwa tu ukilinganisha nishati ya Tanzania ya umeme na nishati ya nchi jirani, bado bei ya umeme hapa ni kubwa sana. Wananchi wanaweka umeme vijijini hawana uwezo licha ya mpango wa *TANESCO* kwamba wanaweza kuwaruhusu kuunganisha kwa awamu na kwa gharama mbalimbali.

(a) Je, Serikali haioni kwamba ni muda muafaka wa kuwa na viwango tofauati ili kuweza kuchochea zaidi wananchi vijijini, waweze kutumia nishati ya umeme badala ya kushindwa kutumia kwa sababu ya gharama kubwa?

(b) Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada ya Serikali napenda tu kusema kwamba mtandao uliobakia kutoka Nyashimo, Nyakaboja, Kabita, Kalemera hadi

Lamadi ni sehemu ndogo sana ukilinganisha kwamba umeme umetoka Musoma kuja mpaka Lamadi na kutoka Mwanza kuja Nyashimo.

Je, Serikali haioni kwamba walau hata kama ni kwa uwezo wa dharula ujaribu kuunganisha nishati hii ili wananchi waweze kupata?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI (k.n.y.WAZIRI WA NISHATI NA MADINI):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa napenda kumpongeza Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, kwa kazi nzuri aliyofanya ya kuhakikisha kwamba umeme umepatikana Bunda kutoka Lamadi na nina hakika kwamba akishirikiana na Wizara maeneo mengine hayatabakia.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni kwamba ni kweli gharama za umeme ziko juu na ziko za aina mbili, zile za uzalishaji zenyewe kwa maana ya maeneo tunayozalisha umeme na zile za kuunganisha umeme kwa wateja mbalimbali hasa vijijini.

Mheshimiwa Spika, Serikali sasa hivi ina mpango kwanza wa kuangalia utaratibu wa kuendeleza nishati mbadala, Serikali tumeshaanzisha miradi ya Gesi ya Songosongo ambayo itafufua umeme pamoja na ule mradi wa *Mnazi Bay* wa Lindi na Mtwara.

Lakini vile vile Serikali kama nilivyosema kwenye jibu la msingi imekwishatoa utaratibu wa jinsi gani wateja wanaweza kuunganisha umeme katika maeneo yao. Mwanzoni ilikuwa ni taabu kwa watu vijijini kulipia mara moja. Lakini utaratibu wa Serikali wa kuleta mpango wa wananchi vijijini kulipia kwa miezi 12 ni njia mojawapo ya kukata makali ya gharama hizo za umeme.

**MHE. KHAMIS AWESU ABOUD:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa umeme wa *TANESCO* una tabia ya kukatika na kwa sababu mikatiko hiyo watu wengi mara nyingi wanakuwa wameshaweka bidhaa zao katika sehemu mbalimbali.

Je, Serikali ina mpango wa kuwalipa gharama wale watu ambao wanaharibikiwa na mali zao?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI (k.n.y. WAZIRI WA NISHATI NA MADINI):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Khamis Awesu Aboud, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli mara nyingine umeme huwa unakatika na kuleta hasara kwa baadhi ya vifaa vya wateja katika maeneo yao. Lakini pale ambapo inathibitika kwamba kuharibika na vifaa hivyo kunatokana na hitilafu za umeme na sio hitilafu za uunganishaji umeme zinazofanywa kwa njia ambazo hazifuati utaratibu, upo

utaratibu wa kuomba fidia kupitia *TANESCO* na wananchi wengi wamefanya hivyo na baada ya tathmini wamekuwa wakilipwa gharama za uharibifu uliotokea.

Na. 108

**Umeme Mkoa wa Ruvuma**

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA (k.n.y. MHE. DR. LAWRENCE M. GAMA)** aliuliza:-

Pamoja na jitihada kubwa sana zinazofanywa na Wizara ya Nishati na Madini katika kuupatia Mkoa wa Ruvuma umeme wa uhakika wa *Mg. 132* kutoka Makambako, Njombe, Songea Mbinga na Namtumbo, je, maendeleo ya utekelezaji wa mpango huo umefikia wapi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI (k.n.y.WAZIRI WA NISHATI NA MADINI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Lawrence Gama, Mbunge wa Songea Mjini, kama ifuatavyo:-

Serikali ya Sweden kupitia Shirika lake la Maendeleo la *SIDA* limetoa fedha kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu *(feasibilitu study)* wa ujenzi wa njia kuu ya umeme wa kilovolti 132 kutoka kituo kipya kitakachojengwa cha Makambako hadi Mji wa Songea.

Mheshimiwa Spika, hatua zilizofikiwa hadi sasa ni kuwa *TANESCO* tayari wameshatangaza zabuni kwa ajili ya kumpata mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na tarehe ya mwisho ya kurejesha na kufungua zabuni itakuwa tarehe 18 Februari, 2005. Baada ya mshauri wa kufanya kazi hiyo kupatikana *TANESCO* itaingia naye mkataba na kazi kuanza mara moja. Kazi hiyo ya upembuzi yakinifu itachukua muda wa miezi 8 kukamilika kuanzia mwezi wa Aprili, 2005.

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii kwanza kupongeza juhudi za Serikali za kuondoa tatizo la umeme Mkoa wa Ruvuma, hasa pamoja na Wilaya zake. Kwa kuwa wananchi wa Wilaya hizi hasa Mbinga, Namtumbo hawajawahi kuona umeme hata mara moja wanasikia tu na umeme ni haki yao ya msingi; na kwa kuwa hata wakoloni walikuwa wanasema kwamba Afrika ni Bara la giza.

Je, Serikali kweli haioni umuhimu wa kuharakisha suala la wananchi ambao hawajapata haki yao ya msingi?

Je, kwa nini hasa tusikope tukaona kwamba tatizo hili la umeme hasa kwanye miji isichukuliwe kama ndio kipaumbele hasa ikizingatiwa kwamba maeneo haya yanazalisha sana?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI (k.n.y. WAZIRI WA NISHATI NA MADINI):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, kama ifuatavyo:-

Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba upatikanaji wa umeme ni haki ya msingi kwa wananchi hapa nchini ambao watatumia umeme ule katika kuendeleza maendeleo yao na Serikali inatambua kabisa kwamba Mikoa ya Kusini pamoja na Mkoa wa Ruvuma ni Mkoa ambao unahitajika kupata miundombinu ya umeme.

Mheshimiwa Spika, ndio maana hata katika ziara yangu niliyoifanya katika Mikoa ya Kusini niliona kwa kweli shida ambayo ipo hasa katika uwekezaji wa miradi mikubwa kutokana na kukosekana umeme.

Kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, sasa hivi Serikali ina utaratibu wa kuchukua umeme kutoka Makambako hadi Songea na mradi huu unatarajiwa kukamilika Juni, 2006. Katika kipindi hicho, nina hakika kabisa Mkoa wa Ruvuma utakuwa unapata umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo hivi sasa Serikali imekwishapeleka *generator* mpya ya *megawatt* mbili Ruvuma kwa maana ya mji wa Songea. Mji wa Songea unatumia *megawatt 3.5, megawatt* mbili zilizopelekwa sasa hivi kwa *generator* hiyo zitatosheleza kabisa mahitaji ya umeme katika Mji wa Songea. Kama nilivyosema awali, fedha za *SIDA* zitakuwa ni changamoto ya kupeleka umeme Mkoani Ruvuma.

Na. 109

**Hati za Kusafiria**

**MHE. KARIM SAID OTHMAN** aliuliza:-

Kwa kuwa Wabunge pamoja na Maafisa wengine wa Serikali ambao wanapewa hati za kusafiria za Kibalozi huwa wanapata *Visa* za bure wanapokwenda kutembelea nchi mbalimbali duniani:-

(a) Je, kuna mkataba wa Kimataifa unaozitaka nchi kufanya hivyo?

(b) Ikiwa jibu ni ndio, je, kwa nini baadhi ya nchi kama zile za *UAE* hususan Dubai wanatoza fedha kwa ajili ya *Visa* za pasi za aina hiyo?

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Karim Said Othman, Mbunge wa Chambani, lenye sehemu (a) na (b), naomba kutoa maelezo ya utangulizi kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hakuna mkataba wowote wa Kimataifa unaozitaka nchi kutoa *Visa* za bure kwa watu wanaotumia hati za Kibalozi wanaposafiri kutoka nchini mwao kwenda nchi nyingine duniani. Kutoza au kutokutoza ada ya *Visa* ni uamuzi wa nchi husika. Kuna baadhi ya nchi hazitozi ada za *Visa* kwa watu wenye pasi ya Kibalozi na wengine hawatozi iwapo kama wahusika wanasafiri kikazi kama hawasafiri kikazi, anatakiwa kulipia ada ya *Visa.*

Mheshimiwa Spika, nchi za Marekani, Uingereza na *UAE* ni miongoni mwa Mataifa duniani yanayotoza ada za *Visa* kwa wasafiri ambao hawaingii nchi hizo kikazi.

Na. 110

**Tanzania Kusaidia Nchi za Afrika Kupata Uhuru**

**MHE. OMAR M. MWENDA** aliuliza:-

Kwa kuwa nchi yetu iliamua kusaidia nchi jirani za Msumbiji, Angola na Afrika Kusini katika harakati zao za kupata Uhuru ambapo Makao Makuu ya harakati hizo yalikuwa ni Nachingwea; na kwa kuwa wananchi wa Mikoa ya Lindi na Mtwara waliathirika kiuchumi na kimaendeleo:-

(a) Je, kulikuwa na mkataba wowote wa kuisaidia Mikoa hiyo baada ya nchi hizo kupata Uhuru?

(b) Je, Serikali inaisaidiaje Mikoa hiyo iliyoathirika?

(c) Je, raia wa nchi za Msumbiji, Angola na Afrika Kusini wanaelewa kuwa Watanzania walijitolea nafsi na mali zao kwa ajili ya ukombozi wa nchi zao?

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Omar Mwenda, Mbunge wa Kilwa Kusini, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Ni kweli kwamba nchi yetu imesaidia nchi nyingi za Afrika katika harakati za ukombozi zikiwemo Msumbiji, Angola na Afrika Kusini. Mchango huo umetokana na imani yetu chini ya uongozi wa Rais wa kwanza wa nchi yetu Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Nyerere, kwamba nchi yetu haiwezi kuwa huru hadi nchi zote Barani Afrika zitakapokuwa huru. Kwa sababu hiyo, tulijitolea kwa hali na mali kusaidia harakati za ukombozi wa wenzetu waliokuwa bado wanatawaliwa. Maeneo mengi ya nchi yetu yalitumika kwa ajili ya shughuli za ukombozi ikiwemo Nachingwea.

Baada ya maelezo hayo, naomba sasa nimjibu Mheshimiwa Omar Mwenda, swali lake kama ifuatavyo:-

(a) Hapakuwa na mkataba wowote wa kusaidia Mikoa ya Lindi na Mtwara baada ya nchi za Msumbiji, Angola na Afrika ya Kusini kupata Uhuru. Tulipokuwa tunasaidia ukombozi wa nchi hizo tulikuwa tunatimiza wajibu wetu kihistoria na hapakuwa na sharti la malipo baada ya Uhuru kupatikana.

(b) Serikali inatambua umuhimu wa kusaidia maeneo yaliyoathirika kutokana na harakati za kusaidia ukombozi wa Bara letu. Kila Mkoa uliohusika pamoja na Lindi na Mtwara, imesaidiwa kupitia mipango ya maendeleo na programu mbalimbali zilizokuwa zinatekelezwa na Serikali tangu Awamu ya Kwanza hadi sasa.

(c) Wananchi wa Msumbiji, Angola na Afrika ya Kusini pamoja na Serikali zao wote wanatambua na kuthamini mchango wa Tanzania na wananchi wake katika ukombozi wa nchi zao. Ni kutokana na kuelewa kwao huko ndio maana Tanzania na Watanzania wanapewa heshima ya kipekee katika nchi hizo. Vile vile ndiyo sababu ushirikiano kati ya Serikali yetu na Serikali za Msumbiji, Angola, Namibia, Zimbabwe na Afrika ya Kusini ni mzuri sana.

**MHE. OMAR M. MWENDA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa wananchi na Serikali za nchi hizo zinafahamu mchango wetu wa Mikoa ya Lindi na Mtwara, je, Serikali iko tayari kuwashauri na wao watusaidie kama tulivyowasaidia sisi? *(Kicheko)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nataka kusema tu kwamba ni kweli Lindi huko Nachingwea ndiko kulikuwa na kambi ya *Farm Seventeen* waliyokuwa wanatumia *FRELIMO* na *ZANU, ANC* wala *SWAPO* hawakuwepo kule, *SWAPO* walikuwa Kongwa na baadaye Mbeya.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla tunachokizungumza ni kwamba wao wanatambua mchango wa Tanzania.

**SPIKA:** Mmh!

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Na Watanzania wote wamechangia sio Lindi na Mtwara peke yake, hapana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mwambie!

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mimi sidhani kama italeta heshima kwa nchi yetu kwenda kuwaomba, jamani eeh, Lindi na Mtwara tuliwasaidieni na sisi mtusaidie.

Mimi nadhani ni vizuri tulipe Taifa letu heshima, tulitimiza wajibu wetu hatuwezi kwenda kunadi matatizo yetu kwa Namibia, Angola na Afrika ya Kusini. Serikali

haijaona sababu hiyo ndio maana hatujaenda kuzungumza nao kwa ajili ya maombi hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu tunapata misaada mingi na katika misaada hiyo hata Lindi na Mtwara inafika. Kwa hiyo, hatuna sababu ya kwenda kwingine kuomba misaada hiyo, ahsante sana.

Na. 111

**Viwanda vya Kubangua Korosho**

**MHE. RAYNALD A. MROPE (k.n.y. MHE. BERNARD K. MEMBE)** aliuliza:-

Kwa kuwa mwaka 2002 Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa kwa uchungu mkubwa alielezea kusikitishwa kwake na mtindo wa kuuza korosho zilizobanguliwa nje ya nchi badala ya kuzibangua hapa hapa nchini:-

(a) Je, azma ya Serikali ya kuvibinafsisha viwanda vyote ili viweze kununua, kuajiri na kubangua korosho imefanikiwa kwa kiwango gani?

(b) Je, ile azma ya Serikali ya kuvipelekea vikundi mbalimbali hasa vya akinamama mashine ndogo za kubangulia korosho imetekelezwa vipi kwa vitendo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bernard Membe, Mbunge wa Mtama, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Tanzania ina viwanda vikubwa vya kubangua korosho kumi na viwili vilivyoko katika Mikoa ya Dar es Salaam, viwili; *TANITA I* na II; Pwani kimoja kilichoko Kibaha; Mtwara, vitano: Mtwara, Masasi, Newala I, Newala II na Likombe; Lindi, vitatu: vilivyoko Lindi, Mtama na Nachingwea na Ruvuma, kimoja kilichoko Tunduru.

Serikali imechukua hatua za kubinafsisha viwanda hivyo na hadi mwezi huu wa Februari, 2005, viwanda tisa vilikuwa vimepata wanunuzi, navyo ni *TANITA I,* Newala I na II, Kibaha, Masasi, Lindi, Nachingwea, Mtama na Likombe. Walioshinda *tender* za kununua viwanda hivyo wanakamilisha taratibu za kuvinunua ili wakabidhiwe. Viwanda vitatu ambavyo havikupata wanunuzi vya Tunduru, Mtwara na *TANITA II* vimeshatangazwa tena.

(b) Serikali inawahimiza wananchi, vikiwemo vikundi vya wanawake, kubangua korosho kwa kutumia mashine ndogo za mikono. Hata hivyo, hakuna mpango maalum ulioandaliwa wa kuvipelekea vikundi mashine ndogo za kubangulia korosho.

Katika jitihada za kuhimiza matumizi ya mashine ndogo za kubangulia korosho, Wizara imetoa mafunzo na kufanya maonyesho ya matumizi ya mashine hizo kwa maafisa ugani 80 wa Wilaya za Mikoa inayolima korosho. Jumla ya mashine 57 zimegawiwa kwa vikundi na Taasisi mbalimbali katika Wilaya kumi na mbili. Wilaya ya Kisarawe ilipata mashine sita; Mkuranga mashine sita; Kilwa mashine nne; Mtwara Vijijini mashine mbili; Mtwara Mikindani mashine nne; Masasi mashine tano; Lindi Vijijini (Tarafa ya Mtama) mashine nne; Tandahimba mashine nne; Bagamoyo mashine sita; Tunduru mashine sita; Newala mashine tano; Ludewa mashine tatu na Chuo cha Kilimo cha Naliendele kilichopo Mtwara kilipata mashine mbili.

Mheshimiwa Spika, wapo wafanyabiashara ambao wameanzisha viwanda vya kubangua korosho kwa kutumia mashine za mikono *(labour intensive method)* kimoja kiko Mtwara na kingine kiko Dar es Salaam. Nawapongeza sana wafanyabiashara hao kwa uamuzi wao wa kuanzisha viwanda hivyo. Kuanzia msimu ujao, watakaonunua korosho na kuzibangua humu nchini watapunguziwa sana kodi wakati wale watakaotaka kuuza nje korosho ambazo hazijabanguliwa watatozwa ushuru mkubwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali inawashauri wananchi kununua na kutumia mashine ndogo kwa sababu zinaongeza wingi wa korosho zinazobanguliwa humu nchini na zinaongeza ufanisi katika ubanguaji na ubora wa korosho.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa Serikali imetumia fedha nyingi sana katika kukarabati viwanda hivi vya korosho kabla ya kuvibinafisha, je, ni viwanda vingapi vilivyokarabatiwa na baada ya kukarabatiwa ni viwanda vingapi vinavyofanya kazi kwa majina na mpaka hivi sasa viwanda hivyo vimebangua kiasi gani cha korosho na kuna faida gani?

(b) Kama alivyokiri Mheshimiwa Naibu Waziri mwenyewe kwamba mpango wa kusambaza viwanda vidogo vidogo huko vijijini bado ni wa nadharia. Tunapenda kufahamu Serikali hasa hasa inataka kufanya nini katika Vijiji hivi na tutegemee nini kutoka Serikalini ili sehemu mbalimbali ziweze kujiandaa na mpango huo utakapokuwa umekamilika? Hivi Serikali mtaanza lini?

**NAIBU WAZIRI VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka mikakati ya kusaidia viwanda vidogo vidogo nchi nzima na kama nilivyokwishaeleza ni kwamba tutapitia *SIDO*. Tumejaribu kwenda katika Mikoa ya Kusini, Mtwara na Lindi kuhamasisha kwamba *SIDO* inatengeneza mashine ndogo ndogo zinazouzwa shilingi 50,000 na tumewasihi Waheshimiwa Wabunge wawasaidie wananchi wanaolima korosho waweze kupata mashine hizi kutoka *SIDO*.

Mheshimiwa Spika, Serikali haina mpango wa kujenga kiwanda kwa sababu tumeshajitoa katika kufanya biashara na sasa kazi yetu ni kutoa mafunzo, kutengeneza dhana kama tunazotengeneza, kuwapatia mikopo na kuwashauri wananchi waje kuchukua mikopo na kuanzisha viwanda vidogo vidogo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara amejibu swali la pili, swali la kwanza endelea kujibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo na Chakula, linahitaji takwimu nyingi sijui kama unazo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali ilitumia fedha kukarabati baadhi ya viwanda, havikuwa vyote kwa sababu baadhi ya viwanda hivi 12 vingine havikuanza hata kazi kama kile cha Tunduru kwa sababu ya tatizo la nishati. Kilichofanyika vichache vilikarabatiwa na vingine vikakodishwa kwa watu binafsi kuvitumia. Kwa hivi karibuni ilikuwa kiwanda cha Masasi na Kibaha. Lakini baadaye tumegundua kuwa hivi viwanda vikubwa vilivyokarabatiwa havisaidii sana katika *production* kwa sababu *machinery* zile zimepitwa na wakati. Ndio maana Serikali na hasa Wizara ya Kilimo na Chakula kwa kushirikiana na *SIDO* inahimiza kununua mashine hizi za shilingi 50,000 na kuhamasisha vikundi vya wanawake na vinginevyo kuanzisha viwanda vidogo vidogo. Ni rahisi zaidi na itawafikia wananchi kwa wingi zaidi kuliko kungojea mhisani aweze kuwekeza katika viwanda vikubwa halafu tuwe na matatizo tuliyokuwa nayo sasa. *(Kicheko)*

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Baada ya Serikali kuhamasisha wabanguaji wadogo wadogo, Mkoa wa Pwani ulianzisha *association* ya *Small Scale Cashew nut Processing Authority(SSCAPA)* na kwa utaratibu mzuri wa hawa wanajua hata kubangua kwa kisasa na wakamfundisha hata huyu mwenye *premier* kule Dar es Salaam...

**SPIKA:** Mmh!

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Waziri pamoja na Mkuu wa Mkoa walifuatwa na waka...

**SPIKA:** Sasa swali.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Swali, baada ya *SSCAPA* kumfuata Waziri wakiwasiliana na Mkuu wa Mkoa na Waziri kuahidi atawasaidia, je, Waziri wa Kilimo na Chakula amewasaidia kiasi gani na Naibu Waziri wa Viwanda amewasaidia namna gani *SSCAPA* kwa sababu mimi mwenyewe nimekwenda *SIDO* sijapata msaada? *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, kama tulivyozungumza ni kuwa tunahamasisha lakini kuna taasisi au Wizara ya Kilimo na Chakula inashirikiana nazo ambazo ni pamoja na *SIDO* na Bodi ya Korosho Tanzania. Tunachoomba ni kuwa Waheshimiwa Wabunge wakati mnapofanya mipango hiyo hakikisheni kama matawi ya Bodi mfano Bodi ya Korosho ina tawi lake Dar es Salaam pale karibu sana na lile jengo la pamba msaada huu unaweza kupatikana lakini kama wakifanya peke yao kijijini halafu mawasiliano ndio mpaka tunakutana Bungeni, inakuwa vigumu. Kwa hiyo, naomba kutoa wito tushirikiane huko huko Dar es Salaam na nakukaribisha Mheshimiwa, tuko tayari kutoa msaada, hiyo ni kazi yetu.

Na. 112

**Reli ya Uhuru - *TAZARA***

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA** aliuliza:-

Kwa kuwa mwaka 1976 Serikali ya watu wa China ilitoa mkopo kwa ajili ya ujenzi wa Reli ya Uhuru - *TAZARA* kwa nchi ya Tanzania na Zambia; na kwa kuwa, reli hiyo iligharimu mamilioni ya fedha hadi kuikamilisha ujenzi wake; na kwa kuwa kumbukumbu zinaonyesha kuwa deni hilo halijaanza kulipwa na Serikali zinazohusika (Tanzania na Zambia); na kwa kuwa si jambo la kiungwana kuanza kubishana au kuuza mali ambayo deni lake halijalipwa:-

(a) Je, ni kwa nini *TAZARA* (Tanzania) imeamua kuuza mali za Shirika *(non-core assets)* wakati ikitambua kuwa bado mkopo huo haujalipwa kwa Serikali ya China; na je, Serikali ya China imejulishwa kuhusu uuzaji huo wa mali za Shirika zikiwemo nyumba na maghala?

(b) Je, ni fedha kiasi gani kimepatikana baada ya muuzaji wa mali hizo na zimetumika kwa kazi gani na katika maeneo gani?

(c) Je, kwa nini hatua hizo za uuzaji wa mali *(non-core assets)* zimefanyika kwa upande wa Tanzania tu na sio za Zambia?

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ibrahimu Marwa, Mbunge Musoma Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kutokana na matatizo ya fedha yanayoikabili *TAZARA,* Bodi ya Wakurugenzi ilishauri Baraza la Mawaziri wa *TAZARA* kwamba baadhi ya mali ambayo haina uhusiano wa moja kwa moja na uendeshaji wa *TAZARA* ziuzwe. Ushauri huu ulikubaliwa na mali kama maghala na nyumba vimeuzwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Watu wa China imekuwa ikihusishwa katika vikao na maamuzi yote muhimu na katika ngazi zote kuhusu uendeshaji wa *TAZARA* kupitia mwakilishi wake anayeitwa *Cret Leader* na vile vile katika Menejimenti, Bodi ya Wakurugenzi na Baraza la Mawaziri. Aidha, kuna vikao vya *Tripartite* ambavyo huzihusisha Serikali zote tatu za Tanzania, Zambia na China. Vikao hivi huchukua maamuzi yote muhimu yanayohusu ushirikiano wa kiufundi baina ya nchi hizi tatu hususani namna ya kuiendesha *TAZARA.*

Katika hatua nyingine ya kushirikisha Serikali ya China kuhusu masuala ya *TAZARA* ni kwamba Serikali ya Watu wa China imekaribishwa iingie ubia na Serikali za Tanzania na Zambia katika uendeshaji wa *TAZARA*. Serikali ya Watu wa China

imezialika Serikali za Tanzania na Zambia kwenye mkutano utakaojadili kwa undani hatma ya *TAZARA* hasa baada ya kampuni ya *Price WaterHouse Coopers* kutoa ripoti yake kuhusu kuirekebisha *TAZARA.* Katika mkutano huo, utakaofanyika Beijing, China mwezi Mei, 2005, China itatoa msimamo wake kuhusu kuhusika na urekebishaji wa *TAZARA.*

(b) Mheshimiwa Spika, mpaka sasa mali zilizouzwa na *TAZARA* ni *Kinondoni Hostel, Upanga Senior Management Guest House, Kurasini Material Depot, Land on Long-term Lease ORYX* na *General Cargo Warehouse.* Jumla ya fedha zilizopatikana ni shilingi bilioni 5.91 na zimetumika kwa kulipia michango ya wafanyakazi *NSSF;* kulipia ushuru *TRA;* kulipia mafuta; kulipia vipuri; matengenezo ya njia ya reli na kulipia mafao ya waliostaafu. Kutokana na sera ya Serikali ya Zambia na Tanzania ya kuwezeshwa wafanyakazi wa *TAZARA* na kutokana na uhaba wa fedha za matengenezo ya nyumba za wafanyakazi, Menejementi ya *TAZARA* ilipeleka mapendekezo kwenye Baraza la Wakurugenzi na Baraza la Mawaziri wa *TAZARA* ikiomba kupunguza idadi ya nyumba za wafanyakazi ili kubakiza idadi ndogo itakayokidhi mahitaji ya Mamlaka. Nyumba zilizouzwa kwa wafanyakazi, Tanzania na Zambia ni 3,776.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kwamba Serikali ya Zambia iliwauzia nyumba wafanyakazi wake na wale wa Mashirika ya Umma zaidi ya miaka kumi iliyopita.

(c) Mheshimiwa Spika, majengo mengine kama vile maghala ya kutunzia vifaa mbalimbali yalijengwa na Wachina wakati wa ujenzi wa Reli ya Uhuru. Madhumuni yake ilikuwa ni kuhifadhi vifaa vya ujenzi na mali nyingine. Baada ya ujenzi mali yote hiyo ilikabidhiwa *TAZARA.*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa vifaa vingi vya ujenzi vilikuwa vinashukia Bandari ya Dar es Salaam, maghala mengi yalijengwa Dar es Salaam katika maeneo ambayo yana mvuto wa kibiashara. Ulipotolewa uamuzi wa kuuza mali hizo, matangazo yalitolewa katika vyombo vya habari katika Tanzania na Zambia. Mali nyingi ya Mkoa wa *TAZARA* wa Tanzania iliweza kuvutia wanunuzi wengi na kupata soko.

Kwa upande wa Zambia vile vile matangazo yalitolewa ila majengo hayakupata soko zuri kwa sababu zifuatazo:-

- *Mkushi River Motel* iko kwenye sehemu ya shamba haikupata bei kubwa.

- *Chozi Guest House* iko mbali na mji wa Lusaka imeshindikana kupata mnunuzi.

- Nyumba mbili zilizoko Lusaka wanunuzi wamekuwa hawafikii kiwango cha thamani ya jengo, hivyo kushindwa kuziuza.

Mheshimiwa Spika, ni nyumba moja tu *(Executive Guest House)* pale Lusaka ndio iliyopata soko zuri na kununuliwa.

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali ya nyongeza. Kwanza nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri na ya kina.

(a) Kwa kuwa huu mradi ulikuwa ni mkopo uliotolewa na Serikali ya China kwa Serikali za Tanzania na Zambia, je, pamoja na hatua hizi za kuanza kuuza baadhi ya mali ya Shirika hili la *TAZARA,* Serikali hizi mbili zina mpango wa kuanza kulipa deni hili lini ili tusije kuacha hili deni kwa watoto wetu kwa miaka inayokuja?

(b) Kwa sababu biashara ya reli inahitaji maghala, je, hatua hii inayofanyika sasa ya kuuza maghala eneo la Tanzania, Waziri haoni kwamba itakuja kuathiri shughuli za Shirika hili siku za usoni?

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, hivi sasa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China inatudai Tanzania na Zambia fedha kiasi cha *UN* bilioni 1.9. Malipo ambayo tumeshawahi kulipa ni milioni 65 tu kwa hiyo, deni ambalo halijalipwa ni kubwa. Lakini ndugu zetu hawa ni ndugu wa kweli maana kila baada ya miaka mitatu huwa wanatupatia takribani dola milioni 10 kutusaidia kuendesha *TAZARA.* Kwa hiyo, mkopo bado unaongezeka lakini hawajawahi kutudai wala kutulazimisha kulipa. Kwa hiyo, matarajio yetu ni kwamba siku moja tutazungumza ili angalau kama ilivyo katika mikopo mingine waweze kutusamehe lakini hayo tutazungumza nao.

Kuhusu mahitaji ya maghala hasa Dar es Salaam kwa sababu ndio Bandari, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba maghala kwa kweli sio shughuli ya msingi ya *TAZARA.* Yale yaliyo katika reli yenyewe tutaendelea kuyahifadhi lakini yale yaliyo karibu na Bandari kama yanahitajika na *TAZARA* basi tutaendelea kukopa kuyatumia lakini sio shughuli za msingi.

Na. 113

**Mionzi Itokanayo na Minara ya Simu**

**MHE. MARGARETH J. BWANA** aliuliza:-

Kwa kuwa inasemekana kuwa minara ya mawasiliano ya simu za mkononi inatoa mionzi yenye madhara kwa afya za viumbe hai hasa binadamu kwa kuwasababishia ugonjwa wa kansa baada ya kipindi fulani:-

(a) Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya tatizo hilo?

(b) Je, mionzi hiyo ina uwezo wa kusambaa umbali gani?

(c) Kama kuna ukweli juu ya jambo hilo, je, Serikali inachukua hatua gani kurekebisha minara hiyo ili kunusuru afya za wananchi?

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Margareth Bwana, Mbunge wa Viti Maalum, naomba nitoe maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba ongezeko la minara kutokana na kupanuka kwa mitandao ya simu za mkononi unaleta wasiwasi na mashaka miongoni mwa wananchi. Serikali inatambua kwamba ni muhimu wananchi wakapewa maelezo ya kitaalam ili waweze kuondoa hofu na pia kujilinda na madhara yanayoweza kuletwa na mionzi, iwe ya simu za mkononi au mionzi mingine.

Kuna aina mbili ya mionzi. Kuna mionzi inayozalishwa na masafa ya *X-rays* na *Gamma rays.* Hiyo inajulikana kama *ionising radiation.* Mionzi hiyo inapomwingia mwanadamu husababisha kuharibika kwa chembechembe za mwili *(cells)* na inaweza kuleta ugonjwa wa kansa. Pia kuna mionzi inayozalishwa na masafa ya radio ijulikanayo kama *non-ionising radiation.* Mionzi hii ikiingia katika mwili wa binadamu au kiumbe kwa ujumla husababisha ongezeko la joto mwilini. Madhara mengine ni pamoja na kuungua misuli, ngozi na sehemu yoyote ambayo mionzi hiyo imeingia.

Tume ya Kimataifa ya Uzuiaji wa Athari ya Mionzi *(International Commission for Non-Ionising Radiations Protections (ICNIRP)* na Shirika la Afya Duniani *(World Health Organisation (WHO)* kwa pamoja wametoa viwango vya usalama wa kulinda wananchi au watumiaji wa simu na wafanyakazi katika mazingira ya mionzi ili kuhakikisha kuwa mionzi inayowafikia haiwaletei madhara. Viwango hivyo hutumika na nchi nyingi duniani isipokuwa Marekani na Urusi ambao nchi hizo zina viwango vyao. Pia hutumiwa na wadau wengi kama vile wazalishaji wa vifaa vya mawasiliano na watoa huduma za mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bwana, lenye sehemu (a), (b na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mpaka sasa hakuna uthibitisho wa kitaalam unaonyesha kuwa mionzi inayotokana na mawimbi ya *radio* inaweza kusababisha kansa. Shirika la Afya Duniani *(WHO)* halijatoa tamko lolote linalohusisha mionzi ya *radio* na kansa.

(b) Mheshimiwa Spika, mionzi inayozalishwa na mawimbi ya redio kutoka mitambo ya simu za mkononi inaenda mbali zaidi ya kilomita kumi, nguvu yake inayoweza kusababisha athari hupungua jinsi umbali unavyokuwa mkubwa kutoka kifaa kinachounganishia mawimbi *(antenna).* Umbali ambao unahofiwa kuwa ni wa hatari ni kati ya mita moja hadi mita mbili kutoka katika kifaa kinachorushia mawimbi. Tahadhari zinazochukuliwa ni kwamba *antenna* hufungwa juu ya minara yenye urefu wa kati ya mita 35 hadi mita 75 hivyo kuwezesha kuzuia madhara ya mionzi inayozalishwa na mawimbi ya *radio.*

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA)* ikishirikiana na Tume ya Mionzi ya Taifa inatarajia kupima minara ya simu za

mkononi na mitandao mingine kama rada, vituo vya radio za utangazaji, *TV* na madishi vitolewavyo na mitandao hiyo ili kuoanisha makadirio ya mionzi hiyo na viwango vyake.

Mheshimiwa Spika, takwimu hizo zitasaidia katika kuandaa miongozo kuhusu usalama wa matumizi ya mionzi katika mazingira yetu. Zoezi litaanza mara baada ya Tume ya Mionzi ya Taifa kupata chombo cha kupimia mionzi. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine watahakikisha inatolewa elimu kwa wafanyakazi na waajiri inayohusu jinsi ya kujikinga na athari za mionzi.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi ya kujibu swali hili kutoa taarifa juu ya maeneo ambayo yamepata huduma za simu za mikononi hivi karibuni. *Mobitel,* Kayanga, Tunduma, Mbalizi, Tukuyu, Kyela, Rungwe Mashariki, Uyole, Kemendo, *Kagera Sugar,* Butiama, Bariadi, Lushoto, Pangani, Kibosho, Babati, Kasumulo, Endulemu na Manyara.

*Celtel,* Ilula hivi karibuni siku tatu zilizopita Kidete, halafu sehemu ya barabara kati ya Iringa na Mtera Ikwiriri, Utete, Kibiti, Horohoro na Makete. Maeneo yafuatayo yanategemea kupata huduma hizi ifikapo mwezi Juni mwaka wa 2005.

*Mobitel,* Simanjiro, Liwale, Kilwa, Lindi, Masasi, Tandahimba, Newala, Ihumwa, Chamwino, Bulyanhulu, Nyamasoro, Butarama, Mkundi, Kilombero, Ifakara, Ngara, Kondoa, Kishapu, Mlandizi, Chakechake, Wete, Mkoani, Madema, Hare, Handeni,Horohoro, Busagara, Geita, Geita Mines, Mtukura, Biharamulo, Nzega, Urambo na Manyoni. *(Makofi)*

*Celtel,* Nkasi, Ngudu, Misungwi, Sikonge, Mugumu, Liwale, Kibaya, Mahenge, Nachingwea.

*Vodacom,* maeneo yaliyo katikati ya barabara ya kutoka Arusha - Babati - Kondoa na Dodoma hadi Iringa.

Mheshimiwa Spika, nawakaribisha watumiaji wapya wa huduma za simu wasihofu mionzi ya *radio.*

**SPIKA:** Ahsante Waziri na hiyo ndiyo inatufikisha mwisho wa muda wa maswali. Yaliyobaki yatashughulikiwa kama kawaida.

Waheshimiwa Wabunge, matangazo ya Vikao vya Kamati kwa leo, kwanza, niseme tutakuwa na Kikao cha dharura cha Kamati ya Bunge ya Uongozi mara baada ya kipindi hiki cha maswali katika sebule ya Spika *(Speaker's Ground),* ambapo tutafanya Kikao wakati tunakunywa chai.

Kamati nyingine ni Kamati ya Maliasili na Mazingira, Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Anne Makinda, anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo, alikusudia wakutane saa 4.30 mara baada ya kipindi cha maswali lakini nafikiri sasa watakutana baada ya Kikao cha Uongozi, itakuwa labda saa 5.00 asubuhi kwenye chumba Na. 231. Kamati ya

pili ni ya Uwekezaji na Biashara, Mheshimiwa Shelukindo Mwenyekiti anaomba Wajumbe wake wakutane saa 6.00 mchana kwenye chumba Na. 227 ghorofa ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge wa Kupambana na Ukimwi *(TAPAC),* anaomba wake wabaki humu ndani ya Ukumbi wa Bunge kwa muda mfupi mara baada ya kuahirishwa kipindi cha Bunge cha asubuhi.

Waheshimiwa Wabunge, taarifa nyingine inahusu Miswada, leo asubuhi hii tutasoma Miswada kwa mara ya kwanza kwa lengo la kuijadili katika Mkutano ujao.

Makatibu waligawa Miswada hii asubuhi lakini kama kuna Mbunge ambaye hakupata, basi bado nakala zipo apewe. Lengo lake ni kwamba, Waheshimiwa Wabunge, waweze kuisoma Miswada hii kati ya sasa na Mkutano ujao, waweze kujadiliana na wadau kama wapo ili kusudi tutakapokuja kuijadili angalau tuwe tumeshaifanyia kazi.

La mwisho, leo ndiyo siku ya mwisho iliyopangwa kwa ajili ya Mkutano huu wa Kumi na Nane, napenda kuwaarifu kwamba, hotuba ya kufunga Mkutano huu itatolewa kuanzia saa 11.00 jioni.

Mwisho wa matangazo, Katibu endelea na *Order Paper.*

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

Muswada wa Sheria ya Uendeshaji wa Vyuo Vikuu wa Mwaka 2005 *(The Universities Bill, 2005).*

Muswada wa Sheria ya Uanzishwaji wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere wa Mwaka 2005 *(The Mwalimu Nyerere Memorial Academy Bill, 2005).*

Muswada wa Sheria ya Kutumia Stakabadhi za Mazao yaliyowekwa kwenye Maghala ya Mwaka 2005 *(The Warehouse Receipts Bill, 2005).*

Muswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Mfuko wa Nishati Vijijini wa Mwaka 2005 *(The Rural Energy Bill, 2005).*

Muswada wa Sheria ya kurekebisha Sheria ya Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika wa Mwaka 2005 *(The Co-operative Audit and Supervision (Amendment) Bill, 2005).*

*(Miswada iliyotajwa hapo juu ilisomwa Bungeni Mara ya Kwanza)*

**SPIKA:** Ahsante, kabla hatujaenda kwenye hatua inayofuata, Mheshimiwa Naibu Spika, wewe usiende kwenye Kamati ya Uongozi, njoo unipokee Kiti ili nikaongoze Kamati ya Uongozi.

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti*

## HOJA ZA SERIKALI

## AZIMIO

**Azimio la Kuridhia Mkataba wa Ushirikiano wa Utamaduni kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Korea *(Cultural Agreement between the Government of the United Republic of Tanzania and the Government of the Republic of Korea).***

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Azimio la Kuridhia Mkataba wa Ushirikiano wa Kiutamaduni kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Korea.

Kabla sijatoa maelezo ya Azimio hili, nawashukuru sana, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge Huduma za Jamii, Mheshimiwa Omar S. Kwaangw', Mbunge wa Babati Mashariki, pamoja na Wajumbe wa Kamati hiyo, kwa kuupitia na kuujadili Mkataba huo na kupendekeza Azimio hili lipitishwe na Bunge. Mkataba huu ni muhimu kwa nchi yetu katika nyanja za Elimu, Utamaduni, Michezo na Habari, kama nitakavyoufafanua. Kwa hiyo, kwa kuzingatia umuhimu wake, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, wakubali Bunge hili lipitishe Azimio la Kuuridhia Mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, upo uwezekano mkubwa wa ushirikiano kati ya nchi hizi mbili hata katika nyanja nyingine zikiwemo za maendeleo ya Elimu ya Ufundi na Uchumi, Mkataba huu ni hatua mojawapo ya kuimarisha uhusiano wetu na Jamhuri ya Korea. Mkataba wa Ushirikiano wa Utamaduni kati ya Tanzania na Korea Kusini ambayo ndiyo Jamhuri ya Korea ulitiwa sahihi tarehe 18 Desemba, 1998.

Masuala muhimu katika Mkataba huo kwanza ni kukuza ushirikiano katika elimu kwa kuwa na ziara za walimu, wasomi, wanafunzi na mabingwa wa masuala ya elimu, kwa nia ya kubadilishana utaalam na uzoefu kati ya Taasisi za Elimu ya Juu, kubadilishana vitabu vya kiada na ziada na vifaa vingine vya elimu kati ya asasi za elimu za nchi mbili hizi na kuhimiza na kuwezesha kuhudhuria kwa wasomi na mabingwa kwenye mikutano itakayoandaliwa na yoyote kati ya nchi hizi mbili.

Pili, kushauriana na kuwezesha kutambulika kwa shahada, stashahada na vyeti vingine vitolewavyo na kila nchi kwa madhumuni ya kutambuliwa katika nchi hizi mbili.

Tatu, kuhimiza ushirikiano katika maeneo ya utamaduni na sanaa hasa kwa kufanya yafuatayo, kutembeleana kwa waandishi, wasanii na wataalam wengine wa shughuli za utamaduni na sanaa, kufanya maonyesho ya sanaa za ufundi na za jukwaani na kushiriki katika matamasha, kualikana na kushiriki katika semina, makongamano na warsha zitakazoandaliwa katika kila nchi, kubadilishana vitabu, magazeti na maandishi

mengine kuhusu utamaduni na sanaa, kubadilishana habari na taarifa juu ya matamasha, mashindano na mikutano ya kimataifa ya Utamaduni itakayoandaliwa na yeyote kati ya nchi hizi mbili na kushirikiana katika utengenezaji wa filamu kuhusu utamaduni wa nchi hizi mbili.

Nne, kuhimiza kutafsiriwa na kuchapishwa kwa kazi muhimu za fasihi katika nchi hizi.

Tano, kuhimiza ushirikiano wa vyombo vya habari vya nchi hizi mbili kama vile redio, televisheni, filamu na magazeti.

Sita, kuhimiza ushirikiano na ubadilishanaji wa maandishi kati ya maktaba, makumbusho, majumba ya hifadhi ya sanaa za ufundi, nyaraka, vituo vya kuhifadhi habari za utamaduni mbalimbali, majumba ya sanaa za maonyesho na asasi nyingine za utamaduni.

Saba, kukuza ushirikiano katika masuala ya uhifadhi wa urithi wa utamaduni.

Nane, kutoa habari na maelezo ya nchi mwenza bila athari ya kueleweka vibaya kwa historia, jiografia na utamaduni wa nchi mwenza.

Tisa, kuhimiza kuanzishwa kwa vituo vya utamaduni vya nchi mwenza bila kuathiri vipengele vya Mkataba huu.

Kumi, kuhimiza kupanuka kwa shughuli za utalii kati ya nchi hizi mbili kwa kubadilishana ujuzi na utaalamu kati ya asasi za utalii za nchi, kubadilishana habari, maandishi na matokeo ya utafiti katika sekta ya utalii.

Kumi na moja, kuhimiza ushirikiano kati ya asasi za vijana na vijana wa nchi hizi kwa ujumla.

Kumi na mbili, kuhimiza ushirikiano katika nyanja za michezo kwa ziara za wataalam wa michezo na kwa kualikana katika matukio mbalimbali ya michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Azimio lenyewe kama ifuatavyo:-

KWA KUWA, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina ushirikiano mzuri na Jamhuri ya Korea na katika kuendeleza ushirikiano huo nchi hizi mbili zilitiliana saini Mkataba wa Ushirikiano wa Utamaduni kati yao mnamo tarehe 18 Desemba, 1998;

NA KWA KUWA, Mkataba huu utatekelezwa na nchi hizi mbili kwa kuzingatia usawa na maslahi ya pamoja katika nyanja za elimu, utamaduni, sanaa, habari, utalii, vijana na michezo;

NA KWA KUWA, Mkataba huu pia unaruhusu nchi moja kati ya hizi kuanzisha vituo vya utamaduni katika nchi nyingine ili kuendeleza utamaduni baina yao;

NA KWA KUWA, nchi hizi mbili zitashauriana na kuwezesha kutambulika kwa shahada, stashahada na vyeti vitolewavyo na kila nchi kwa madhumuni ya kutambuliwa katika nchi hizi mbili;

NA KWA KUWA, faida za kuridhia Mkataba huu ni nyingi ikiwa ni pamoja na kujenga ushirikiano katika nyanja za utamaduni, michezo, uhifadhi wa urithi wetu na utalii, kuwezesha walimu, wasanii na wanamichezo wetu, kunufaika na uzoefu na ujuzi wa wenzao wa Jamhuri ya Korea;

NA KWA KUWA, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bado haijaridhia Mkataba huu;

KWA HIYO BASI, kwa kuzingatia umuhimu na faida za Mkataba huu na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Bunge hili katika Mkutano wake wa Kumi na Nane, sasa linaazimia Tanzania Kuuridhia Mkataba wa Ushirikiano wa Utamaduni kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Korea *(Cultural Agreement between the Government of Republic of Korea and the Government of the United Republic of Tanzania).* Baada ya maelezo niliyoyatoa, naomba sasa Bunge lako Tukufu, likubali kulipokea na kulipitisha Azimio hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. JUMANNE H. NGULI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kamati ya Huduma za Jamii, naomba kutoa maoni ya Kamati kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Ushirikiano wa Utamaduni kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Korea *(Cultural Agreement between the Government of Republic of Korea and the Government of the United Republic of Tanzania).*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha maoni ya Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Ushirikiano wa Utamaduni kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Korea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuridhia Mkataba huu kutaipa nchi yetu manufaa mengi ikiwa ni pamoja na kujenga ushirikiano baina ya nchi hizi mbili katika nyanja za utamaduni, michezo, elimu, maonyesho ya sanaa, kushirikiana katika matamasha mbalimbali, kubadilishana vitabu vya kiada na ziada, uhifadhi wa urithi wetu, utalii, ikiwemo kuwezesha walimu, wasanii na wanamichezo kufaidika na uzoefu na ujuzi wa

wenzao wa Korea. Baada ya kulipitia Azimio hilo, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

Kwanza, utekelezaji wa Mkataba huu uhusishe pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu unagusa jamii ya Watanzania wote katika nyanja za utamaduni, michezo, utalii na elimu.

Pili, kwa kuwa, Mkataba huu unagusa Wizara mbalimbali ikiwa ni pamoja na Wizara ya Elimu na Utamaduni, Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu na Wizara ya Maliasili na Utalii, watendaji wa Wizara hizi zote na nyingine zitakazoguswa na Mkataba huu wajizatiti kuufanyia kazi kwa pamoja ili kutochelewesha utekelezaji wake kwa sababu ya urasimu unaoweza kujitokeza baina ya Wizara na Idara husika. Ni muhimu sana kwa Serikali kupima ufanisi wa utendaji kazi katika kutekeleza mikataba ya kimataifa kwa sababu umahiri wetu katika ushirikiano na nchi zingine utapimwa kwa kuangalia ufanisi na uadilifu wetu jinsi watendaji wetu Serikalini wanavyotekeleza kazi zao.

Tatu, nchi yetu ifanye juhudi za makusudi za kuwawezesha vijana wetu, waweze kwenda kushiriki shughuli mbalimbali nchini Korea kama vile michezo, sanaa, utamaduni, matamasha na mikutano iliyoandaliwa kwa ajili ya shughuli za kiutamaduni kwa mujibu wa Mkataba huu ikiwemo kupata nafasi za masomo nchini humo.

Nne, Serikali kwa kutumia vigezo maalum, iwe inafanya tathmini mara kwa mara ili kujua jinsi nchi inavyonufaika na Mkataba huu na tathmini hiyo iwe sehemu ya kazi za Kamati za Bunge wakati zinapojadili utendaji wa kazi za Serikali kila mwaka.

Tano, ushirikiano kwa mujibu wa Mkataba huu, ulenge kukuza vipaji vya wasanii na wanamichezo wetu hasa katika kufikia vigezo vya Kimataifa, vilevile fursa ya ushirikiano huu isije ikatumika vibaya kwa vijana wetu kuiga utamaduni wa nchi nyingine na kuanza kuupuuza na kudharau utamaduni wa Mtanzania. Serikali inashauriwa kuwa makini sana katika eneo hili na izingatie msemo usemao: “Samaki mkunje angali mbichi.”

Sita, ushirikiano huu unapogusa nyanja za utalii, Serikali iangalie isije ikaathiri mapato ya nchi yetu kwa kuruhusu wageni kutoka nchini Korea kuingia katika vivutio vyetu kwa visingizio vya ushirikiano huu, hivyo, rasilimali zetu zisije zikatumika kwa manufaa ya wageni.

Saba, tunashauri kuwa Serikali yetu itumie fursa ya ushirikiano huu kuimarisha vyuo vyetu vinavyotoa mafunzo ya usanii, michezo na utamaduni kama vile Chuo cha Sanaa Bagamoyo, Chuo cha Ualimu Butimba na kuimarisha Baraza la Sanaa la Taifa. Fursa hii pia sasa itumike kuimarisha timu zetu zitakazoshiriki katika michezo ya *Olympic,* kwa sababu ndani ya nchi yetu, lipo kundi la watu wenye ulemavu ambao bado hawajapata fursa kubwa ya kushiriki katika shughuli za utamaduni na michezo na kwa kuwa Jamhuri ya Korea imekuza sana vipaji vya vijana wao ikiwa ni pamoja wale wenye

ulemavu, tunaishauri Serikali itumie fursa hii kuboresha michezo kwa watu wenye ulemavu ili nao wanufaike na Mkataba huu.

Tisa, Kamati inaihimiza Serikali kuwasilisha Mikataba ya Kuridhiwa Bungeni mapema kwa ajili ya kuridhiwa ili kuiwezesha nchi yetu kuanza kunufaika na Mikataba hiyo mapema iwezekanavyo. Mkataba huu unaotarajiwa kuridhiwa na Bunge lako Tukufu leo, ulitiwa saini baina ya Serikali za nchi hizi mbili miaka saba iliyopita, kwani Mkataba ulitiwa saini mwaka 1998.

Mheshimiwa Naibu Spika, inaonyesha wazi kuwa udhaifu huu wa Serikali wa kutokuwasilisha Mikataba mapema mbele ya Bunge, sasa umeota sugu na hii inaonyesha jinsi Mikataba inayogusa utekelezaji wa Wizara nyingi, isivyoratibiwa sawasawa. Tunaishauri Serikali iunde chombo cha kuratibu shughuli muhimu za Kitaifa zinazohitaji kuridhiwa na Bunge kwa muda unaotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkataba huu kwa bahati nzuri katika kifungu cha 16(2), unakubali kuridhia makubaliano ya kuendelea na Mkataba moja kwa moja, uwe *renewed* baada ya miaka mitano kama hakuna nia ya kukatisha makubaliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kumpongeza Mheshimiwa Joseph Mungai, Waziri wa Elimu na Utamaduni na Mheshimiwa Bujiku Sakila, Naibu Waziri wa Elimu na Utamaduni, pamoja na Maafisa wa Wizara hiyo, kwa kuwasilisha Azimio hili mbele ya Kamati, kwa ufanisi mkubwa. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge, ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii, kwa kulitafakari Azimio hili kwa kina na umakini mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa Mkataba huu, Kamati yangu inaliomba Bunge lako Tukufu, likubali kuuridhia kwa manufaa ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. KHAMIS ALI SALEH - MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kutoa mchango wa Kambi ya Upinzani juu ya Azimio la Kuridhia Mkataba wa Ushirikiano wa Utamaduni kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Korea *(Cultural Agreement between the Government of the Republic of Korea and the Government of the United Republic of Tanzania).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na taadhima, ninaomba kuchukua nafasi hii ili niweze kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani Bungeni, kwa mujibu wa kifungu cha 43(5)(b) na 81(1), Toleo la 2004, kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Ushirikiano wa Utamaduni kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Korea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba wa wapiga kura wa Jimbo langu la Mgogoni - Pemba na familia yangu, tunawatakia heri ya mwaka mpya Waheshimiwa Wabunge wote na kuwapa pole wale wote waliofikwa na maswahibu ya kidunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya tano ya Azimio inaongelea ubadilishwaji wa tamaduni zetu za asili na zile za watu wa Korea. Hapa Kambi ya Upinzani bado ina wasiwasi kuhusu lugha itakayokuwa inatumika, kwani kama tunavyoelewa Tanzania ina tamaduni nyingi kulingana na makabila tuliyonayo. Kwa kawaida tunapofanya tafsiri huwa maana halisi ya lugha ile hupungua uzito wake kwa msisitizo. Kwa maana hiyo basi, Kambi ya Upinzani inaona kuwa ni muhimu wahusika wakuu wakatoka katika makabila husika.

Tanzania ni nchi yenye makabila mengi, yenye lugha tofauti, desturi na mila tofauti, maana yake ni kwamba, Tanzania kama nchi, haina utamaduni wa aina moja, hivyo, nikizungumzia nchi kuwa na utamaduni wa kushirikiana na Taifa lingine, haina maana yoyote, *unless* kufanyike utafiti wa kutosha kubainisha ni utamaduni upi wa Korea unaofanana na utamaduni wa kabila fulani hapa nchini na kuruhusu tamaduni hizo zishirikiane. Kwa hali iliyopo sasa, ambapo inafanana na Korea, haipo isipokuwa lugha kwa sababu lazima watu waongee lakini siyo kwa tamaduni, kama tulivyoeleza hapo mwanzo kwamba, Tanzania kama nchi haina utamaduni wa Kitaifa bali kuna tamaduni za kikabila.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya tofauti hizo za tamaduni, kama neno utamaduni linavyoelezwa na Kamusi ya Kiswahili, Kambi ya Upinzani ingependa kusisitiza utamaduni tunaoweza kushirikiana na Korea ya Kusini ni kama vile utamaduni wa kufanya kazi kwa nguvu na maarifa, utamaduni wa kuendeleza sayansi na shughuli nyingine ambazo zitaongeza tija kwa uzalishaji na ujasiliamali kwa lengo la kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ibara ya sita inaelezea uhamasishaji utakaofanywa na vyombo vya habari ili kuwezesha Umma kutoa hitimisho katika maandalizi. Kambi ya Upinzani inaomba maelezo toka kwa Mheshimiwa Waziri, kuwa ni lugha gani itakayokuwa inatumika, kwani tunapoongelea suala la utamaduni, Tanzania ina tamaduni za makabila yasiyopungua 120 na hayo huendesha shughuli zake kwa lugha zake?

Mheshimiwa Naibu Spika, lugha itumiwayo na vyombo vya habari ni Kiswahili na Kingereza, hivyo, tunaona lugha ipewe kipaumbele kwanza kabla ya hata utamaduni wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ibara ya 12 inaeleza kuhamasisha maendeleo ya utalii baina ya Mataifa mawili. Kambi ya Upinzani inavyoelewa uhamasishaji wa utalii wa nchi ni kitu kinachofanyika kwa kuzingatia Mikataba na Makubaliano fulani ambayo Wizara husika inawekeana na Kampuni au Taifa kwa niaba ya Serikali. Sasa Wizara ya Elimu na Utamaduni, suala hili inalichukulia vipi, kwani tusije tukajikuta tunaweka bomba la kuhamisha utajiri wetu wa utalii kwa kisingizio cha utamaduni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaelewa kuwa, tayari hapa kuna Kituo cha Utamaduni cha Watu wa Korea toka miaka kama kumi iliyopita, sasa tunaomba Mheshimiwa Waziri, atueleze kituo kama hicho cha Tanzania nchini Korea

kina wafanyakazi wangapi na ni maonyesho mangapi ya sanaa yameshafanyika huko mpaka sasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tumemaliza Wasemaji Wakuu, sasa kwenye orodha yangu ninao wachangiaji sita na ninadhani kwa leo tungeishia hapo. Ninaye Mheshimiwa Raynald A. Mrope, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mheshimiwa Edward Ndeka na wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Semindu Pawa. Sasa namwita Mheshimiwa Raynald Mrope.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia kidogo juu ya Mkataba huu wa Ushirikiano kati ya wenzetu wa Korea ya Kusini. Nilitaka tu kumweleza mwenzangu wa Kambi ya Upinzani, kuwa ile nyingine yenye jengo la utamaduni ile ni Korea ya Kaskazini, inaitwa *Democratic Republic of Korea,* kwa hiyo basi, hiyo ndiyo tofauti yake kubwa.

Kwanza, natoa shukrani kwa kupata nafasi hii ili niweze kuzungumza na ninamshukuru sana Waziri wa Elimu na Utamaduni, kwa kuleta Mkataba huu mbele yetu. Labda niseme tu kuwa, mimi kwa kadri ninavyowafahamu, Wakorea hasa Korea ya Kusini, kwa jinsi walivyoendelea sana katika nyanja ya Sayansi na Teknolojia, hili ni Taifa moja, ninaliita ni Taifa kubwa ingawa wenyewe wanajiita ni Taifa linaloendelea, lakini ninaliita Taifa kubwa ambalo tungekuwa tunahusiana nalo toka siku nyingi.

Kwa hiyo, huu Mkataba toka ulitiwa saini sasa ni miaka mitano, mimi ningekuwa nimefurahi kama ungekuwa umeletwa mapema zaidi Bungeni ili mahusiano haya kati yetu na Wakorea yaanze mapema zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuanzisha uhusiano na nchi yoyote ni lazima tuangalie jinsi gani sisi Wananchi tutanufaika katika uhusiano huo. Nikiangalia nchi yetu na hasa sehemu ninayotoka, kwa upande wa uchumi na fedha, tunahusiana na wafadhili kutoka Finland. Wao walikuja na taratibu zao mbalimbali za kusaidia hasa katika nyanja za maji, elimu, maendeleo ya jamii na kadhalika. Lakini niseme tu kwamba, baadaye tukaja kuona kuwa, Finland ingawa wana nia njema sana ya kutusaidia lakini uwezo wao ni mdogo.

Kwa hiyo, uwezo wa kuendeleza ile Mikoa ya Kusini ulikuwa hafifu. Sasa kwa sababu nimeona kuwa hawa Wakorea, kadri ninavyowafahamu, ningesema kwamba, kama hatuko tayari kinchi, basi tuwasogeze Kusini, yaani wasaidie Mikoa ya Mtwara na Lindi katika nyanja mbalimbali za utamaduni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeuelekeza uhusiano huo zaidi katika upande wa kukuza sayansi na teknolojia ambayo hawa wenzetu wanayo ya hali ya juu. Katika Mikoa hii ya Kusini, kwa bahati nzuri imegunduliwa gesi. Gesi hii kwa sasa hivi tumekwishaanza kuitumia kwa ajili ya kuzalisha umeme. Lakini Wakorea ni watu

wanaofahamu namna nzuri ya kutumia ile gesi ili iweze kutumika katika vyombo kama magari, pikipiki na kadhalika, yaani kwa kubadili ile gesi iweze kuwa kama mafuta.

Kwa hiyo, ninasema jamani, hawa tuwavute waje watufanyie hizi *studies* mbalimbali ili tuweze kutumia ile gesi kwa matumizi mbalimbali. Kama mnavyofahamu, wenzetu wa Korea ni mafundi sana wa kutengeneza magari ya Hyundai, Sonata na mengine ambayo yanatumika hapa nchini. Pia Wakorea ndio wanaotengeneza kompyuta, simu za mkononi za *Samsung* na kadhalika na vitu vyote hivi vinatengenezwa kwa *plastic*. Sisi Kusini kule kwa sababu tuna gesi ya kutosha tungeweza ku-*convert* gesi hii ili ituzalishie mazao haya ya *plastic.* Kwa hiyo, katika Mkataba huu tuwavute wale waje watufundishe namna ya kutumia rasilimali hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kabisa wangeweza kubadili ile gesi iwe *plastic* na kutengeneza kompyuta, simu, magari na kadhalika. Sasa mambo ya namna hiyo ndio tunaweza kufaidika kutokana na Mikataba ya namna hii, kwa sababu Mikataba hii inasema mambo mengi kama vile elimu, kukuza teknolojia na utamaduni. Hapa ningepingana kidogo na mwenzetu yule wa Kambi ya Upinzani, ambaye amezungumzia zaidi juu ya utamaduni.

Haya mambo ya kucheza ngoma na nini unaomba watu muwe mnabadilishana vikundi vya ngoma, tuache hayo, hebu tuvute mambo makubwa na mazuri ya maendeleo kama haya niliyoyazungumzia. Naamini tukifanya hivyo tutapata manufaa makubwa. Sidhani kama wenzetu wa Finland wale watasikitika kwamba, kwa nini mmeita Taifa lingine? Wale tuendelee nao katika mambo madogo madogo ya nyuki, mbuzi na kadhalika, lakini hawa tuwaite katika hii *gas reserve* tuliyoigundua, hebu tuitumie kisayansi kwa kuwatumia hawa kutokana na maendeleo makubwa ya teknolojia waliyoyafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niongelee suala la utalii. Nilipenda tu labda kulifahamisha Bunge na yule Kiongozi wa Upinzani kama yupo, kutokana na hotuba yake, nimwambie kwamba, utalii ni soko moja linalokua kwa kasi sana na karibu nchi nyingi zinatumia utalii kama zao mojawapo la kuuza nje. Sisi hapa Tanzania ni hivi karibuni tu tulipokuja kutambua kwamba, kumbe utalii unaweza kutuletea mambo mengi. Nizungumze kama Mwenyekiti wa Bodi ya Utalii, niseme kwamba, kwa mwaka 2004 pekee, watalii wameleta katika nchi hii dola milioni 731 sawa na Shilingi bilioni 731. Hiki ni kiasi kikubwa sana cha fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kazi kubwa iwe kuvutia watu mbalimbali na kwa upande wa Korea, mipango ya Bodi ya Utalii ni kujaribu kuwavutia watalii wa kutoka China, *North Korea, South Korea,* Japan na kadhalika, ili waje waangalie vivutio vyetu. Kitu cha kuzungumza kwa mfano, Korea peke yake inaweza kutoa watu laki sita, wakaja hapa nchini na hiyo itakuwa fedha nyingi sana. Sasa ningependa Mkataba huu uhusishwe na maendeleo ya utalii Kusini mwa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu za Kilwa pale kuna kila aina ya vivutio kama vile mapango mbalimbali, kuna historia kubwa ya watumwa waliokuwepo pale na

Waarabu, mambo waliyokuwa wanayafanya zamani na mambo ya kale yapo mengi sana. Halafu ukienda baharini ambapo Wakorea hawa wana-*interest* pia kumegunduliwa samaki aliyekuwa anaishi miaka milioni 150 iliyopita. Samaki huyu kama sikosei jina lake la Kiingereza anaitwa *Selucans.* Sasa *Selucans* amekuja kugunduliwa Kilwa. Hili ni jambo kubwa linalowavutia watalii wengi duniani. Katika Mkataba huu, tungewavutia wenzetu Wakorea waje wafanye kazi mbalimbali za samaki yule na pia kuleta watalii ambao watakuja kuona mazingira anapopatikana samaki huyu na pia kutembelea vivutio vyetu mbalimbali tulivyonavyo kule Kilwa mpaka *Selous*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naamini kabisa tukijikita kwenye utalii wa maeneo mapya ya Kusini, hawa Wakorea wanaweza kufanya mambo mengi makubwa kwa sababu mpaka sasa hatuna investment kubwa kutoka kwa Mataifa mbalimbali na tunahitaji hayo Mataifa yalete *investment* zao katika ujenzi wa mahoteli na vivutio vingine vingine ili watu waje kwa wingi. Sasa hivi kwa sababu barabara ya Dar es Salaam-Kibiti-Lindi mpaka Mtwara inajengwa, naona Mkataba huu unakuja wakati muafaka ili tuweze kupeleka watalii wengi, wengine watakwenda kwa barabara na wengine kwa meli na wengine wachache kwa ndege. Wanaweza kabisa kuyaendeleza maeneo yale kwa kila hali.

Kwa hiyo, niseme tu kwamba, Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni, ameuleta Mkataba huu wakati muafaka na hasa unapozungumzia kuhusu hizo lugha mbalimbali. Wengine hawaelewi sijui *Chung Zhu* na *Chong Chong,* basi mimi naamini kabisa kama wakiletwa Mtwara na Lindi kule na ninavyoona mazingira yapo tayari kabisa ya hawa kuweza kuja kusaidia kuinua haya yote yaliyotiwa sahihi katika Mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, naomba tena niunge mkono hoja hii na kwamba, huo Mkataba utiwe sahihi upesi na Waziri tafadhali sana akumbuke Kusini wakati akitia sahihi Mkataba huo na hawa akina *Chong Zhu* atuletee sisi kule Mtwara. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kwanza kukushukuru kwa kunipa nafasi hii. Lakini vile vile kutoa salaam za rambirambi kwa wenzetu wote ambao wamepoteza ndugu na jamii kwa kipindi ambacho sijazungumza kwa sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushirikiano kati ya Tanzania na Korea umekuwepo siku nyingi. Naomba kabla ya yote, nichukue nafasi hii kusema kwamba, naunga mkono hoja hii na naamini imekuja kwa wakati muafaka na tunaihitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi ya Korea kufikia mwaka 1961 ilikuwa inajulikana kama nchi ya Taifa maskini, nchi ya dunia ya tatu. Ilikuwa inaunganishwa na Tanzania, Rwanda, Burundi na nchi nyingine ambazo kwa kweli zilikuwa zinategemea msaada wa Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa *(IMF).* Hadi kufikia sasa hivi miaka michache iliyopita Benki ya Dunia na *IMF* walitoa Korea ya Kusini kwenye orodha ya

nchi maskini duniani na sasa imejiunga na orodha ya nchi kubwa duniani ambazo zinaitwa nchi za wafadhili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano wa Korea kama walivyosema Viongozi wetu mara kwa mara ni mfano mzuri sana ambao nchi yetu *realistically* inaweza kuiga kwa sababu tangu wakati wa uhuru walikuwa ni wenzetu, walikuwa ni wakulima wa chini, teknolojia yao ilikuwa ya chini, lakini kwa kipindi hicho kuanzia miaka ya 1960 mpaka sasa wamefika mbali sana na wanalo kila la kujivunia kwa *achievement* ambazo wameweza kuzipata. Mimi ningependa kusema kwamba ushirikiano wowote ni lazima ulenge maslahi ya nchi na natazama maslahi ya nchi yetu hasa katika ushirikiano huu wa kijamii na kiutamaduni tungeweza sana kufaidi kama tutajiandaa kwa namna ambavyo tungependa kushirikiana. Ukiwa mnyonge kupita kiasi uwezo wako wa kushirikiana na mtu yeyote pia unapungua kupita kiasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *GDP* ya Tanzania hadi sasa hivi nafikiri tumekaribia au kuzidi kidogo bilioni tisa, wenzetu wa Korea wamezidi zaidi ya bilioni elfu tano, kwa habari ambazo nilisoma sehemu kadha wa kadha. Hiyo inatupa changamoto na changamoto kubwa ambayo inatupa ni kwamba, sisi tutajiandaa vipi kupokea huu ushirikiano ambao ni mzuri kabisa. Changamoto ya kwanza itakuwa ni lugha. Katika kuendeleza utalii Mataifa mengi ambayo yameendelea kiutalii ya kwanza ni Afrika Kusini , ikifuatiwa na Kenya, Zimbabwe na Namibia, wamekwenda sana katika lugha na kwetu itakuwa vigumu sana kuwachukua Wabunge hawa ukawafundishe Kikorea, Kijapan au Kiitaliano. Lakini tunao vijana wa miaka kumi na tano, kumi na nane, ishirini au ishirini na tano, ambao wanao uwezo kabisa kama wakipewa nafasi ya kujifunza lugha, wakajifunza lugha zote duniani na mwisho wakawa ndio wale tunaowaita mhimili wa maendeleo ya ushirikiano kwa sababu lugha ni suala muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukipanda ndege za wenzetu wa Kenya *Airways* wale *staff* wanaofanya kazi utamwona mwingine kaandikwa anasema Kijerumani, mwingine Kifaransa, mwingine anaongea Kiitaliano na wameandika bendera za zile nchi wanazoongea. Lakini Tanzania nikiuliza ni vijana wangapi wapo fluent kuongeza Kifaransa, Kitaliano, Kijerumani acha lugha kama Kichina na Kijapan ambazo kwa kweli ni ngumu sana, hakuna. Nchi nyingi zinapotaka Utalii wa Afrika Mashariki, sababu ambazo wanaishia Kenya na sababu ambazo raia wa Kenya *naturally* wanapenda kufikiri kila kitu kipo kwao ikiwa ni pamoja na muziki mzuri wa Afrika Mashariki upo Kenya, Kiswahili ni lugha ya Kenya, ni kwa sababu wenzetu wa Kenya wamefika mahali wakawafundisha vijana wao wengi sana lugha. Watu walizungumzia sana wakasema zamani enzi za ujamaa nchi ilikuwa inasaidia, sasa hivi hatusaidii. Nchi isipo-*invest* kwenye *human capital,* hakuna namna yoyote ambayo nchi hiyo itashindana na nchi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi ambazo zinajiita za kibepari zina ujamaa mkubwa sana inapokuja kwenye suala la elimu. Zina Vyuo Vikuu ambavyo vinatoa fedha nyingi sana kusomesha vijana wao, zinatuma vijana wengi sana wakasome nje, wajifunze lugha kuanzia Kiarabu mpaka Kiyahudi. Katika kulitafakari hili ukienda kila kona ya dunia kama ni Chuo Kikuu kwa Wanafunzi au Walimu utakuta katika Vyuo Vikuu vya dunia

wanaofundisha Kiswahili ni Wakenya na sisi nafikiri tumebaki nyuma kidogo kwa sababu ushirikiano kama huu hatukuwa tumeufanya mapema. Hata hivyo, nafikiri wakati huu ni muafaka wa sisi kujaribu kuangalia tutakwendaje mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama suala la lugha halitasimamiwa tukachukua nafasi hii kuwapeleka vijana wetu bila kusubiri Wakorea watulipie, tukachukua *prosecution* ya vijana wakajifunza hicho Kikorea, Kijapan na Kichina, kama tusipofanya hivyo, tutaendelea kubaki nyuma sana katika nyanja za ushirikiano wa kijamii, uchumi na mila na desturi ambazo naamini mwisho wa yote watu wanaongea biashara na biashara zinafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la lugha ni la kwanza lakini la pili ni suala la kubadilishana wanafunzi. Nami naona njia pekee tunayoweza kwenda mbele ni kuhakikisha kwamba wale watu wadogo watakuja kuiva kwenye huu ushirikiano miaka 15 au 20 ijayo. Tatizo kubwa litakuwa kama tutauangalia ushirikiano huu kwa kujiuliza kwamba sisi tuliopo hapa tutafaidi vipi. Mimi naamini ushirikiano wa kweli ni ule ambao tutaujenga miaka 10, 20, 50 au 100 ijayo na msingi tunaouandaa sasa hivi utawafanya watoto, wajukuu na wajukuu wa wajukuu zetu kusema kwamba kweli misingi iliyowekwa ya ushirikiano imefika mahali nchi hizi mbili zimeendelea na zinafanya jambo ambalo linawasaidia watu wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala zima la Utalii ni ushindani. Kila mtu ambaye ana cha ku-*offer* kama vile Tanzania na wenzetu majirani tunashindana na dunia nzima, watu wanaokuja kutalii ni wale watu ambao wana kipato cha ziada na wananchi wa Korea Kusini kufikia sasa hivi wamejaliwa sana kupata kile kipato cha ziada ambacho wanaweza kukitumia kwa shughuli za utalii. Namna gani tuwavutie, ni lazima tuhakikishe kwamba sisi kama Taifa tuna maandalizi thabiti na tunawaweka vijana wetu ambao ndio wanahudumia na wanakuwa human resource katika utalii wawe tayari kushirikiana na wenzao na kushirikiana Kibiashara. Mimi nafikiri ushirikiano huu ni mzuri lakini focus yake kubwa iwe kiuchumi.

Mwisho wa yote tutakapojadiliana utamaduni na mambo mengine nafikiri focus itakuwa ni kuinua uwezo wa Tanzania na uwezo wa Watanzania kuweza kushindana na kuweza kuingia katika Soko la Korea na Soko la nchi za Mashariki ya Mbali kwa ajili ya kuinua uchumi wetu. Naamini kwamba, tunaweza kuvutia wawekezaji wa Korea kwa sababu sasa wanawekeza dunia nzima, tunaweza kuhakikisha kwamba vijana wetu na wafanyabiashara wetu wanaongeza jitihada katika ku-venture kwenda katika masoko mapya ambayo hawajakwenda na naamini Mashariki ya Mbali kama nchi za Korea ni mfano mzuri sana ambao tunaweza kuuiga.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ambalo ningependa kuligusia hapa ni kwamba, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaheshimika duniani kwa sababu ya Muungano wake na Muungano wetu na Zanzibar siyo tu kwamba umetuletea heshima kama nchi lakini umekuwa mfano. Tatizo kubwa sana walilonalo watu wa Jamhuri ya Korea, Korea ya Kusini na Korea ya Kaskazini ni lile tunalolifahamu la uhasama wa ajabu kati yao. Katika *Korean Peninsular* ni eneo pekee duniani ambalo lina majeshi na

lina silaha kubwa karibu kuliko katika maeneo yote ambayo yamewekewa silaha kwa sababu ya uwezekano wa kuzuka vita. Nami naamini mfano mdogo wa Tanzania katika ushirikiano huu tungeupeleka kama mfano ambao wananchi wa Korea ya Kusini na Kaskazini wataendelea kutiwa moyo wafikie mahali pa kuunganisha nchi zao ili liwe Taifa moja la Korea na Taifa lenye nguvu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nachukua nafasi hii tena kuunga mkono hoja hii na kumhakikishia Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni kwamba sisi tutakuwa pamoja kuhakikisha kwamba huu ushirikiano unasonga mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR MASUMBUKO R.M. LAMWAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi siku hii ya mwisho wa Kikao chetu, niweze kuchangia juu ya hii hoja ya ushirikiano kati ya Tanzania na Korea.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu Mkataba ni Mkataba wa Ushirikiano wa Kiutamaduni na yeyote atakayeusoma ataona kwamba, una nyanja kama tano hivi. Kuna mashirikiano katika nyanja ya elimu, uandishi wa vitabu, habari, vyombo vya habari na sanaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Tanzania kama mojawapo ya nchi za dunia hii, lazima ishirikiane na nchi nyingine. Hatuishi kwenye Kisiwa au yai, lakini hofu yangu ni kwamba, haya mashirikiano tunayotaka kuyaendeleza yanaweza kuwa mashirikiano ya upande mmoja, yanaweza yakawa mashirikiano ya mkubwa na mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwamba, Jamhuri ya Korea imeendelea sana kielimu, kisayansi, kiufundi na hata kiuchumi. Sasa hofu yangu ni kwamba, ushirikiano wa namna hii unaweza ukawa *one way* kwa maana ya kwamba, zile *exchanges* ambazo tunataka tuzifanye chini ya huo Mkataba wa Kitalii, Elimu na kadhalika, zitakuwa za upande mmoja kwa maana kwamba, kama tunataka kupeleka kundi Korea lazima tupate msaada wa Korea. Sasa huo ni ushirikiano ambao ni *one sided* na utafaidi upande mmoja tu na huenda utafaidi kwa faida za ule upande ambao wanajua wao. Mimi naomba pamoja na kuunga mkono hoja hii, Serikali iangalie sana kusiwe na *cultural imperialism against us.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la elimu, naomba hilo jambo liangaliwe kwa mapana zaidi ya tunavyolifikiria. Naomba nitazame *article* ya tatu ya huu Mkataba ambayo inasema kwamba, hizi Serikali mbili zitaangalia namna ya kutambua shahada, stashahada na vyeti vingine ambavyo vinatolewa kwenye Vyuo vya hizi nchi.

Ukweli ni kwamba, nchi yetu tayari inayo *system* ya kulinganisha shahada zinazotolewa nje ya nchi hii na zinazotolewa ndani ya nchi hii. Tunayo hiyo *system* chini ya Vyuo vikuu na chini ya Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu. Sasa inaonekana kazi ambayo ni ya kitaaluma kabisa ni *purely academic* inaingizwa sasa kwenye medani ya Siasa. Tukianza kusema Serikali zifikirie namna ya kutambuana,

tunaanza ku-*outer down standards* za elimu yetu na *standards* ya vitu ambavyo tunavitambua kwamba vinafaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu actually wakati sasa umefika Wizara ya Elimu ikishirikiana na Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu ianze kufikiria kwa kina sana juu ya vyeti ambavyo vinazunguka ndani ya hii nchi. Sisemi hivyo kwa sababu linanigusa mimi, lakini kwa mfano sasa hivi tuna watu wengi sana ambao wana *title* ya *Doctor* lakini Vyuo ambavyo vinatoa hizo *doctorate* havieleweki vizuri, sisi tunapokea na tunawaheshimu.

Hatujaona *Thesis* za hawa watu, kuna utaratibu wa kuitwa Daktari kwa mujibu wa Shahada ya Chuo Kikuu. Sasa hatari iliyopo ni kwamba tutakuwa na Madaktari wengi kama tulivyokuwa na akina Profesa Vulata na wenzake. Kwa hiyo, hii *article three* tuiangalie vizuri sana isiwe kwamba tutapokea *qualification* za watu wa nje bila kujua zinatusaidia kiasi gani na zinalingana vipi na *attitude* zetu za elimu.

lakini kwa sasa Mkataba wa namna hii ni Mkataba ambao utafanya vitabu vya ndugu zetu wa Korea vije vingi sana huku na sisi hatuna vitabu vya kupeleka kule kama sio vya udaku tu ambavyo havitakubaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia hata michezo ya kwenye *stage,* ukiangalia michezo inayochezwa kwenye televisheni au stage kwa kweli ni michezo ambayo haifikii vile viwango ambavyo unaweza kuvipeleka kwenye nchi nyingine. Hii ni kwa sababu pia *audience* inapenda vitu vya namna hiyo. Sasa umefika wakati pia tukuze ule utamaduni wa kukuza mambo yetu ya sanaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo lingine ambalo linanipa concern kidogo na ni juu ya Vyombo vya Habari na Uandishi wa Habari. Ukiangalia *Standard* yetu ya habari na jinsi tunavyotegemea vyombo vya nje kupata habari ni wazi pia tutakutana na ndugu zetu wa Korea tukiwa wanyonge. Kwa hiyo, nafikiri Serikali pia iingie katika jukumu la kuwapa moyo Waandishi wetu wa Habari ili kukuza kile kipaji cha Uandishi. Kwa mfano, huu mjadala unaoendelea sasa kati ya *Media Owners Association* na Serikali, uwe ni mdahalo ambao unakuza ile kazi ya Uandishi wa Habari na sio mdahalo wa kurekebisha Uandishi wa Habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni hayo niliyokuwa nayo, namalizia kwa kusema kwamba naunga mkono hii hoja mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika hoja hii ambayo naiona ni muhimu sana kwa yenyewe na kwa hoja nyingine za Maazimio ya ushirikiano wa aina hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niseme kwamba sababu yangu ya kwanza ya kusimama ni hoja nzito aliyoitoa Mheshimiwa Dr Masumbuko Lamwai na sitapenda kutumia muda, lakini niseme tu kwamba nilikuwa nataka kusisitiza hoja hiyo hasa *Article*

*three* ilinitisha, kwa sababu kama tulivyokwishakusema ndani ya Bunge hili, suala la *Academic degrees to cognition, Diplomas and Certificates* tukianza kuiweka nje ya chombo ambacho ndiyo peke yake kinatakiwa kutambua, tutaifikisha nchi yetu mahali pabaya. Kwa hiyo nilitaka nimalizie hapo kwa kuwa mwenzangu amelieleza kwa kirefu.

Sasa niendelee kugusia maeneo mengine ambayo nadhani vilevile katika Azimio hili yanatugusa sana. Nianzie na suala la elimu kwa jumla. Mimi nilifikiri katika Mkataba huu ambao unagusia ushirikiano wa kielimu na kiutamaduni, kama alivyosema mwenzangu na mimi nagusia *aspect* ya michezo. Nchi ya Korea imekwenda mbele sana hasa katika michezo kiasi kwamba hata ukisema tushirikiane, tubadilishane, sina hakika kama kuna cha kubadilishana sisi na wao. Wenzetu wana Vyuo vya Michezo, sisi hata kile Chuo kimoja cha Michezo tulichokuwanacho tumekifunga.

Sasa unapofikia hatua unasaini Mkataba wa namna hii unaingia katika hali ya kwamba wewe daima ni mdogo japo umesaini Mkataba wa ushirikiano. Ushirikiano, naomba nitumie hapa neno la Kiingereza la *partnership*. *Partnership,* maana yake ni watu wawili wenye uwezo wa kulingana wanaamua kushirikiana. Sisi tunaamua kushirikiana, tunaingia na mtaji gani katika ushirikiano huo?

Kwa hiyo, ningependa hapa niseme kwamba iwe ni changamoto kwamba Azimio hili linatukumbusha na sisi kwamba siyo tu kuweka Mkataba huu saini na kuuridhia, lakini vilevile iwe ni changamoto kwetu kwamba yale ambayo wenzetu wanayo na sisi hatuna, tuanze kuyashughulikia.

Kwa mfano, kwa upande wa michezo, tufufue vile Vyuo tulivyokuwa navyo, tuanzishe Vyuo vipya. Tunaposema tunashirikiana kwenye michezo tuwe na mahali ambapo Walimu wetu wa Michezo, Makocha wetu wanapata mafunzo ya kutosha na siyo tunakwenda kubadilishana nao, kitu ambacho wenzetu wana ngazi ya juu na sisi tuna kitu kilicho hafifu na mwisho tunapokea tu kutoka kwao.

La pili, nililotaka kulisema ni eneo hata la utalii tumezungumza kwa kirefu kabisa katika Mkataba wetu kuhusu utalii hasa kifungu cha 12 cha Mkataba. Ninaogopa kwamba, uzoefu tulionao sasa Watanzania hata vyanzo vya vyetu vya utalii hatuvitembelei. Ukiuliza hata ndani ya Bunge ni Wabunge wangapi tumekwenda Tarangire, Mikumi au *Selous*, ni wachache sana. Lakini tunazungumzia *a cultural exchange* kwa maana ya Tourism na hata sasa tuna wenzetu wengi tu wanakuja. Korea hata kabla ya Mkataba huu wanakuja. Mimi kwa kuwa nakaa Ngorongoro, ninawaona kila wakati. Ni karibu na kwetu Ngorongoro barabarani, pale Karatu, wanapita wengi sana.

Lakini tukizungumzia kwamba itakuwa ni *exchange* ni kweli tutafurahi kwa sababu sasa wenzetu watapata unafuu wa kuja. Lakini hiyo mimi sitaita ni *exchange. Exchange* iwezeshe pia na Watanzania wapate nafasi hiyo hiyo ya kwenda. Kwa hiyo, tuna changamoto kwa upande wetu wa kukuza utamaduni na kupenda utalii kuanzia na vianzio vya utalii vilivyoko ndani ndiyo tuanze kwenda nje. Bila kukuza utamaduni huo hapa kwetu, Mkataba huu utakuwa hauna manufaa kwa Watanzania wengi.

Lakini vilevile siishii hapo tu, tunazungumzia exchange ambayo tumeorodhesha. Ukizungumzia *writers, artists, exhibitions focal performance*, ukizungumzia utamaduni wa Mtanzania, kwa wenzetu wana uwezo wa kuja kutazama tu. Hata Viongozi wenu walizaliwa wangapi, ni utamaduni! Lakini sisi hatujaweka hata maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikwishaongea kwa mfano, hapa katika Bunge na ninashukuru huko mwishoni nadhani taratibu zimeanza kutengenezwa. Tunatumaini kwamba zitaanza kufikishwa na hatimaye utaweza kwenda kumwonyesha huyu mgeni unayetaka aje nchini kwako kwenye cultural exchange. Akitaka kuona Viongozi wenu wa Kitaifa wamezikwa wapi, hatuna mahali tunaweza kuonyesha; akitaka kuona labda nyumba ya makumbusho, lakini hata kwenye nyumba ya makumbusho hatuna vitu vingi vya kuonyesha pale vya makabila yetu.

Kwa hiyo, tungelipenda tuweze kuimarisha vile vya kwetu vya ndani tusiichukue tu kama nafasi ya kusaini Mkataba tukafikiria kwamba wenzetu watapata *access* ya kuja, lakini na sisi huku ndani tuchukue Mkataba kama ndiyo challenge na tuwe na programu kamili ya kuweka vianzio vyetu katika hali ya kuweza kuonekana kwa watu wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia *exhibition focal performance* tunatakiwa kuwa na mahali. Ukienda katika nchi za wenzetu kitu cha kwanza ukifika *Airport* unakutana nacho ni *fliers brochure,* wanakwambia leo kinachofanyika katika Mji huu ni hiki na hiki, *performance* zilizoko ni hizi na hizi. Sisi hizi hatujaziona.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna rafiki yetu hapa nafikiri wa *TTB* Mheshimiwa Raynald Mrope bahati mbaya ametoka, tungependa kutoa hii *challenge* kwamba unapopata mgeni Dar es Salaam au Arusha unapata kazi umpeleke wapi?

Tungependa kuwa na *directory* ya vianzio hivi ambavyo ni muhimu uweze kuvi-*exchange* kwa watu wetu. Tuna vianzio vikubwa tu sasa hivi. Kama ni wanyama, Mungu ametuwekea wale hatujawafanyia kazi, hakuna anayemlisha samba lakini yuko pale. Bahati nzuri Mungu anamlisha, anatafuta nyasi, anajitafutia chakula chake, anajitibu mwenyewe sisi tunapokea hela. Lakini hatuvifanyii kazi kwa maana ya sisi kuandaa nyenzo zinazowezesha Mkataba huu uweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka nimalizie kwenye eneo hilo. Lakini nilitaka kugusia kwamba *exchange* tunayoizungumzia mimi inanitisha kwa sababu ukizungumza *writers, artists, book writers, exchange of documentation* hata *documentation* tunazotakiwa kuzituma, sijui kama tunazo na hata sijui kama tuna *infrastructure* ya kuitoa. Mimi naogopa kama alivyosema mwenzetu Dr. Masumbuko Lamwai kwamba isije ikafika mahali tukawa sisi ni watu wa kualikwa tu. Tunaomba tiketi kwa wenzetu na ndiyo ilivyo katika factions nyingi. Watanzania sisi tusipoletewa tiketi hatuendi, usipolipiwa gharama ya ndege, usipolipia hoteli huendi kwa sababu hatuna uwezo.

Lakini hii inakwenda katika mfumo mzima wa uchumi kwamba uchumi wetu ni mdogo, waandishi wetu wa magazeti hawana namna ya kufanya, ndiyo maana hata mara

nyingine waandishi wa magazeti hata kwenda ku-*cover situations* katika nchi yetu wanashindwa. Leo umwambie wana-*exchange* kwenda Korea itakuwa vigumu, lakini Wakorea watakuja huku. *Coverage* ya sisi watatoa, tena watatoa ile wanayotaka wao siyo ile ambayo sisi tungependa kutoa.

Kwa hiyo, tunapenda iwe ni changamoto kwa nchi katika kuboresha na uchumi pia isiwe tu mazingira ya kuandika tu Mkataba, lakini Mwandishi wako wa Habari unayetaka aende Korea mshahara wake haufiki hata Sh. 60,000/=. Sh.60,000/= haimtoshi kwa chakula chake cha mwezi. Sasa atakwenda ku-cover vipi na atalipa vipi tiketi ya ndege ya kwenda kule? Kwa hiyo nafikiri kwamba hapa kwa kweli tuna changamoto nzito. Ni Mkataba ambao tunauona *very simple,* lakini una *implications* kubwa sana kwa watu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikifika kwenye suala la utamaduni wenyewe ni suala la lugha. Ukienda kwenye Kituo cha Wakorea pale Dar es Salaam, kuna *document* zinajaribu kufundisha hata lugha ya kwao. Wanafundisha utamaduni wa kwao, wanafundisha historia ya kwao, sisi hatuna *document* zinazotusaidia kufanya kazi hiyo. Ukitaka lugha ya kwetu ambayo leo tunasema kwamba tunataka iwe lugha ya Mataifa ndiyo nafasi ya kuipenyeza kwenda kuifundisha lakini uwezo huo tunao!

Bajeti yetu inaturuhusu kwenda kufanya kitu hicho au tunaiweka tu kwenye *document*? Maana yake ukiniambia hivyo ni kwamba narudi kwenye bajeti tuliyopitisha, hatuna vipengele vyovyote vya namna hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, unatakiwa kwenda kusaidia zile Balozi ziweze kuwa na *section* ya utamaduni inayoweza kufanya kazi ya *cultural exchange* ikiwa ni pamoja na ku-*facilitate* haya mambo ambayo hayapo, lakini bajeti zetu hazi-*provide*.

Kwa hiyo mimi nilikuwa nafikiria kwamba hapa tunapata changamoto nzito. Tunataka lugha yetu ya Kiswahili ikue, tunataka utamaduni wetu ukue, lakini unaweza kupeleka vipi kama kauli hii nzuri unayokuwa nayo kwenye Mkataba haiambatani pia kwa upande mwingine na kasma za bajeti ambazo tunazitengeneza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa upande mwingine ni kama alivyosema mwenzangu mmoja kwamba tuna tamaduni nyingi na mpaka leo hatujafikia utamaduni *exactly* unapozungumza utamaduni wa Mtanzania ni upi. Tumefika mahali tumefanya mashindano ya kutafuta vazi la Taifa, hata hilo hatujafikia muafaka bado.

Kwa hiyo, tungependa iwe ni pamoja na kuharakisha *process* za aina hiyo kwamba tunaposema tuna utamaduni wa Taifa, unasimama mahali unatambulika wewe kama Mtanzania kwa vazi lako tu, kwa kofia yako tu na kwa nguo yako tu. Sasa hii hatuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tuna mila. Tuna zile values ambazo Watanzania tunajulikana kwamba tuko wapole, tunazi-*export* vipi? Tuna hospitality tuna-*export* vipi? Tunazipeleka vipi? Wenzetu Ulaya hata *Korea Eastern Asia* yote, kidogo wako tofauti

na Ulaya. Unaingia kwenye treni wenzako asubuhi wanasoma magazeti tu hawasalimiani, wameshafikia hatua hiyo. Sisi bado tuna value watu wanasalimiana. Hii ni *value*! Tunaweza kuiona kama ni *commodity* kama kitu cha biashara tunachoweza kupeleka kule kwingine. Watu wanakaa vyumba hawajuani!

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mahali watu wakufa chumba cha jirani wanaweza kukaa siku nne, tano jirani hajui. Lakini sisi bado tunasalimiana asubuhi. Hizi ni values, lakini tunazi-*export* vipi?

Kwa hiyo mimi nafikiri kwamba hapa tuna changamoto nzito, tusione hili Azimio kwamba ni Azimio rahisi sana. Lakini kwa bahati mbaya Maazimio yetu mengi tukisha-*ratify* na tumeyamaliza Bungeni yanakaa kwenye shelve yameishia pale. Mimi naomba hili Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni alifanyie kazi na liweze kuzaa matunda yanayoweza kuonekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba niunge mkono Azimio hili. *(Makofi)*

**MHE. EDWARD N. NDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie katika kujadili Mkataba huu wa Utamaduni kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Korea.

Kabla ya kufanya hivyo, naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge waliotoa salamu za rambirambi kwa wananchi wa Jimbo la Kasulu Mashariki kwa msiba uliotokea wa Mheshimiwa Frank Mussati, ambaye Jimbo lake linapakana na Jimbo langu katika baadhi ya sehemu. Pia nawapa pole wale Waheshimiwa Wabunge wengine ambao walifiwa na wake zao. Marehemu wote hao Mungu awaweke roho zao mahali pema Peponi. Amin.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni kwa kuleta Mkataba huu mbele ya Bunge hili ili tupate nafasi ya kuchangia mawazo katika Mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama walivyosema wenzangu waliotangulia, hapa tunazungumzia Mkataba kati ya nchi yetu na nchi ya Korea ambayo ni nchi iliyoendelea katika nyanja nyingi. Napenda nitofautiane kidogo na baadhi ya wanaodhani kwamba ukishirikiana na nchi yenye uwezo au tajiri, iliyoendelea pengine utakuwa wewe hunufaiki. Inategemea ni jinsi gani utakavyotumia ushirikiano huo katika kuandaa mambo yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukichukua kwa mfano nyanja zile ambazo zimeonyeshwa pale kama elimu, utamaduni, utalii, zote ni nyanja ambazo sisi kama Taifa lenye rasilimali nyingi tunaweza kunufaika katika ushirikiano huo. Kwa mfano alivyokuwa anaeleza Mheshimiwa Raynald Mrope kuhusu eneo la utalii akawa anahimiza kwamba hawa ndugu zetu Wakorea waelekezwe katika Ukanda wa Kusini, kwa sababu kuna fursa nyingi za utalii, nakubaliana naye katika hilo kwa sababu katika

baadhi ya maeneo fursa zipo, lakini utalii ulikuwa bado haujaimarishwa. Hii ni sawasawa pia kwa Ukanda wa Magharibi hasa mwambao wa Ziwa Tanganyika.

Kwa hiyo wito wangu ni katika kuliangalia hili kwamba fursa ambazo zipo kwa mfano katika Ukanda wa Ziwa Tanganyika tunazo mbuga za Wanyama ambazo ni za kipekee, kama Mbuga ya Mahare mwambao wa Ziwa Tanganyika.

Lakini pia tuna maeneo yenye historia za kiutamaduni. Historia ya utamaduni inaweza kuwa mbaya iliyowaathiri katika kipindi fulani hasa tukizungumzia suala la biashara ya utumwa. Lakini ni maeneo ambayo yanaacha kumbukumbu ambazo vizazi na Jumuiya ya Kimataifa wangependa kuja kuyaangalia maeneo hayo kwa sababu ni maeneo ambayo yametokea ndani ya jamii na yamebadilika kutokana na majira hayo, lakini sasa inakuwa katika hali nzuri. Mambo haya yanaleta mvuto wa kitalii.

Sasa katika eneo hili, ni fursa nzuri ambapo hawa watalii wa kutoka nchi ambayo mna Mkataba nayo wakapelekwa katika maeneo hayo ambayo bado hayajapanuliwa zaidi katika sekta hiyo ya utalii, kwa sababu utalii siyo kuangalia vitu tu vya asili, lakini pia na utamaduni wa watu wenyewe. Nakubaliana na maelezo aliyoyatoa Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa ya kwamba tunazo values ambazo zinaweza kuwa ni mvuto, kama ule upole.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka tulipokuwa kwenye ziara, Kamati yetu ya Kilimo na Ardhi huko, maeneo ya Kilombero, tulikutana na Mzungu mmoja ambaye yuko kwenye Mradi wa Kilimo cha Umwagiliaji cha Mpunga. Yeye katika kueleza jinsi ambavyo anajiona yuko nyumbani hapa Tanzania, alisema yeye hadhani kwamba atafia mahali pengine zaidi ya Tanzania na baada ya kusema hayo, alilia machozi. Sasa ni kwa sababu anaridhika kuwa katika mazingira ya watu ambao wana uungwana, wana utaratibu na wana upendo na kadhalika. Kwa hiyo hii ni rasilimali ambayo tunaangalia ni jinsi gani tunavyoweza kufanya tuitumie kwa kuwavutia watu kutoka nchi hasa zile ambazo tumeingia nazo Mkataba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni la Elimu. Nadhani tuna kazi kubwa ya kufanya ili wananchi wetu waweze kujenga hiyo mila ya kujisomea na tunaweza kutumia Mkataba huu na wenzetu wa Korea wakatusaidia kuwekeza katika Sekta hii ya Elimu kwa upande wa Maktaba. Hili suala la Maktaba tumelichukulia kwamba siyo jambo muhimu sana na Maktaba tunazokuwa nazo ziko katika Miji tu. Lakini tunahitaji kuwa na Maktaba katika Vijiji.

Sasa wenzetu wa Korea kwa uwezo wao na kwa ushirikiano wa namna hii, kwa sababu azma moja ni kuendeleza elimu na kuendeleza elimu inaweza kupitia katika njia ya Maktaba na Maktaba za namna hii zikiwa katika maeneo ya Vijiji ni dhahiri itajenga hatua kwa hatua mila ya kujisomea kwa watu wetu. Kama alivyosema mchangia hoja mwingine aliyetangulia kwamba tusiangalie hivi sasa tuangalie miaka 20, miaka 30 ijayo kwamba tukiwekeza katika Maktaba katika Taifa letu ni dhahiri tutajenga hatua kwa hatua utamaduni na mila ya kujisomea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna faida nyingine ambayo imeelezwa chini ya Mkataba huu na mimi ninakubaliana nayo ni faida katika eneo la michezo. Ni dhahiri kwamba michezo ni aina fulani ya kiwanda ambacho unaweza kupata mapato makubwa sana katika muda mfupi. Fikiria mchezo wa mpira wa miguu ambao muda wake ni dakika 90, lakini kwa sababu ya mvuto wa watu kuangalia huo mpira wa miguu wanatoa fedha nyingi sana mamilioni ili waweze kuangalia huo mchezo na hasa inapofika katika michezo ya Kimataifa. Biashara inaongezeka na viwanda vinahamasishwa kwa kuwezesha nchi kuendesha michezo katika eneo lake la namna hiyo. Sasa hapa tunafanya nini?

Nimekuwa nikijiuliza kwamba katika Sekta hii ya Michezo hatujaangalia na hapa ningemwomba Mheshimiwa Waziri aliangalie hili kwa sababu linahusisha pia Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo. Ni suala la vifaa vya michezo. Sijaona mahali ambapo tunajielekeza kuwavutia wawekezaji wawekeze katika viwanda vya vifaa vya michezo. Tunahitaji jezi, tunahitaji viatu na katika nchi hii tunasema tuna ng'ombe milioni 17.

Kwa hiyo tuna bidhaa nyingi za ngozi na mipira inatokana na ngozi. Lakini hatujazungumzia hata siku moja kuwekeza katika viwanda vya kutengeneza zana za michezo hasa viatu na jezi. Lakini ni mahitaji muhimu sana kwa Taifa letu katika sekta hiyo. Kwa hiyo nadhani hawa Wakorea chini ya Mkataba huu tungetumia fursa ya Mkataba huu kuwavutia wawekezaji wawekeze katika viwanda vya kutengeneza vifaa vya michezo kama jezi na viatu kama nilivyosema. Nadhani Mkataba wa namna hii unaweza kutusaidia katika kuimarisha hilo. *(Makofi)*

Kuna jambo lingine hapa limezungumziwa linalohusu sanaa na utamaduni kwa ujumla kwamba tuna makabila mengi katika nchi yetu, ni sahihi na haya makabila yana mila zake na tamaduni zake. Lakini ni jumuiko la mila hizi na tamaduni za makabila yetu ndizo zinazofanya baadaye tuwe na utamaduni wa Mtanzania. Napenda niipongeze Bodi ya Utamaduni ya Taifa kwa utaratibu iliyouanzisha wa kuadhimisha Utamaduni wa Mtanzania kupitia makabila mbalimbali ambayo huwa unafanyika Kijiji cha Makumbusho Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshiriki katika baadhi ya maonyesho hayo ya Utamaduni wa Mtanzania na makabila si chini ya 15 yamekwishafanya maonyesho pale na Mkataba huu umesainiwa miaka saba iliyopita. Sasa katika maonyesho ya namna ile sijaona watu wamealikwa tuseme kutoka kwenye nchi kama hii kwa mfano, waje waone tunavyofanya yale maadhimisho ya Utamaduni wa Mtanzania kama sehemu mojawapo ya chanzo cha kuweza kuanza kujua Watanzania wanafanya mambo yao namna gani. Kwa hiyo, nadhani maadhimisho ya namna hiyo ingekuwa ni fursa moja ya kuwaalika watu kutoka nchi hasa zile ambazo tunaingianazo Mkataba ili waweze kuona jinsi tunavyoadhimisha huo utamaduni wetu na hatua kwa hatua hayo yakiunganishwa ndiyo yanayofanya utamaduni wa Mtanzania uweze kufahamika na kutangazwa katika maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naomba niungane na wenzangu kwa kuunga mkono Azimio hili kwa asilimia mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika kuridhia Mkataba wa Utamaduni kati ya Tanzania na Korea. Nchi ya Korea na Tanzania ni ndugu toka siku nyingi na tuliwahi kuwasiliana. Hata vitabu vyao viliwahi kuuzwa au kutolewa bure wakati mwingine katika miaka ya 1970 na 1975 vile vya aina Kim III Sung, viliwahi kutolewa kwenye Maktaba na katika Maktaba yangu nadhani asilimia 23 ni vitabu hivyo ambavyo vilikuwa vinasambazwa na viliandikwa kwa lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la kushangaza kweli wakati ule ambapo nilivikuta kwenye Maktaba maeneo mengine na huu ni mwendelezo tu wa ushirikiano, nadhani Mheshimiwa Waziri analeta ili kuthibitisha kwamba tuko pamoja na kusudi kuliendeleza. Lakini nilikuwa nimejiuliza: Je, tumejiandaa vipi? Nimeshukuru kwa kupata maoni kwamba tumejiandaa vizuri sana Watanzania katika hali hii.

Utamaduni ni eneo kubwa tu na ni eneo ambalo ni nyeti kwa Taifa. Kuna baadhi ya Tamaduni nyingine huwezi kuzipeleka kwingine wala huwezi ukazifundisha na utamaduni haufundishiki. Huwezi kutafsiri kutoka utamaduni wa nchi fulani nikaleta hapa nchini Tanzania, kuchukua utamaduni wa Wanyamwezi kuuleta kule kwa Walunguru au utamaduni wa Wamakonde, huo ndiyo utamaduni ambao unaeleweka katika maeneo yao.

Katika neno "Utamaduni", 'U' ni urithi, huwezi kurithi mambo ya kule Korea na ile 'T' ni taratibu au tabia ya nchi hiyo au tukio hilo na ile 'A' ni asili yako, kwa hiyo neno unapata Urithi, Tabia, Asili *(UTA)* na ile 'M' ni mila. Sasa mila za mtu fulani huwezi kuzihamisha kwenda kwa mtu mwingine, na ile 'A' ni Asili, mila ambazo ni za asili yako huwezi kuzi-copy katika maeneo mengine na ile 'D' ni desturi. Sasa huwezi kuchukua desturi ya mtu mmoja kwa mfano, kutoka huko Tanga, ukazipeleka desturi kwenda Kigoma. Zipo sekta mtambuko katika kuelimisha neno lenyewe "Utamaduni".

Kwa hiyo, ni vizuri hasa tamaduni zinazokubalika katika maeneo makubwa kuwa *convicted* ikawa ni utalii au maonyesho, nyingine zimeleta historia za mabezo. Hivyo, wakaziacha na kuziponda, kuna nyingine zimeleta historia za majigambo. Hivyo, wakaziendeleza watu wakapata manufaa wakatembea kifua mbele katika nchi zao. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema katika maandalizi kumbe yapo maandalizi mazuri katika Mfuko huu ambao mmeuandaa unaitwa Mfuko wa Utamaduni Tanzania *(Tanzania Cultural Trust Fund)* ambapo hapo kuna kipengele kimoja mmesema kwamba inabidi kupata wafadhili na nchi shirikishi ili kuchangia Mfuko huu. Nadhani hili ni jiwe moja unaua ndege wawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa tumepata tayari mwenzetu nchi mwenza ambayo inaweza ikashirikiana na sisi ila tusiunde Taasisi nyingine, tusiunde Taasisi mpya. Ni Taasisi ipi ambayo itakuwa tayari wao ndiyo rejea wetu watakaowakarimu hao na kushirikiana na Taasisi za Korea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa nilizonazo Korea zipo Taasisi karibuni 58 toka mwaka jana 2004 sijui kama zimeongezeka katika Sekta ya Utamaduni.

Ziko zile Sekta Mtambuka katika Wizara mbalimbali, nyingine ziko chini ya Mkuu wa nchi yenyewe katika kushughulikia utamaduni ambao unaweza ukamilikiwa na wananchi wenyewe, lakini hauwezi ukaruhusiwa kwenda ukaenezwa kwenye nchi nyingine. Ile inakuwa ya nchi ya pale pale unacheza dhikiri bila dufu, yaani watu wasisikie huko nje ni utamaduni wako wa kukusaidia tu kama mila, desturi za nchi zile, huwezi kuzihamisha kuja Tanzania au za kwetu ukazichukua ukazipeleka katika maeneo mengine. Hiyo ni mwiko. Wanasema ni mwiko! Neno “mwiko” linatumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, huwezi kuchukua utamaduni wangu ukautoa. Ni zile tamaduni ambazo zinahusiana kwa kutaka kuridhia nchi yako, hizo unaziacha ila tamaduni ambazo zinakuwa zinaeleweka kwa jumla ndiyo hizo ambazo Taasisi inabidi izisimamie. Ya kwanza, Nyumba ya Sanaa, tunayo tayari pale.

Ya pili, C*ulture Heritage Constituency* ya Dar es Salaam, *Museum* tunayo tayari pale, nyingine ya tatu, *Film Auto Video Constituency Tanzania National Television* tunayo tayari, ipo nyingine inaitwa *Language Literature Constituency.*

Sasa hawa nao wajitahidi katika lugha kuepukana na *Kiswanglish* katika lugha zao, kwa hiyo, kitabu hiki kimeandikwa *The Mfuko!* Sasa jaribuni kutafsiri vizuri, kwa sababu Kiswahili mnakijua. Anzisheni hata Redio ya Sauti ya Kiswahili kule Korea kama ilivyo kule Ujerumani ili Kiswahili kifahamike sana katika nchi hiyo. Ninajua jana ilikuwa siku ya Kiswahili, maneno mengi katika Kiswahili yameibuka mengine ya mitaani, Kiswahili sasa hivi kinasifika duniani na Afrika kwa ujumla. Kwa hiyo, la kwanza ni kuanzisha Kituo cha Kiswahili kwa Sauti ya Kiswahili kule Korea, kama kipo basi naomba kiendelee.

Kituo kingine ambacho kinaweza kikatumika ni hiki cha *Performing Arts Constraincies* pale *Bagamoyo College*, kingine kinaitwa *Cultural Industry Constraincies* kilichoko Afrika Sana. Sasa vingine vingi viundwe kwa mtazamo huo huo kwamba, tunaendeleza utamaduni wetu na nchi mwenza, ila ninatoa mapendekezo yafuatayo: Kwa upande wa elimu, wenzetu wa Korea wasije kusoma wala kufundisha hapa Tanzania, waje kutuwezesha katika sekta zetu na utaratibu wetu tuliojiwekea wa elimu yetu ya Tanzania.

Katika upande wa utalii, wenzetu wa Korea wasije kutalii katika mbuga zetu, waje kuimarisha kwa kutumia mbinu zao za kisasa katika sehemu hizo kwa kutumia utamaduni wao, kama tukiwapeleka Mikumi, Serengeti, maeneo ya Ngorongoro, basi wao watuelekeze jinsi watalii wanavyoweza wakavutiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni upande wa sayansi na teknolojia, tunayo tafsiri sahihi na vipaji maalum, kwa sababu kipaji ni majaliwa, kipaji cha mtoto ni kioja, cha mtu mzima ni changamoto na kipaji cha Mzee ni usia. Kwa hiyo, wenye vipaji maalum waweze kupelekwa kwenye maeneo au taasisi ili kuendeleza vipaji vyao. Katika teknolojia mabadiliko muhimu yanaendeshwa na dunia, basi waungane na Tanzania hata ikiwezekana wale wanaoweza kujifunza wapelekwe Korea kujifunza katika vyuo vyao na wale wasioweza kujifunza waachwe hapa hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utamaduni shirikishi kati ya Tanzania na Korea, basi tuweze kuangalia maeneo ambayo yananyambulika na kuyaunganisha pamoja, yale ya kwetu watuachie hapa hapa, tunacheza dhikiri bila dufu, mambo ya ngoma na mengine, watuachie hapa hapa.

Mwisho, wenzetu wa Korea wana tabia ya kujituma, kujitolea na kutokulalamika, lakini Watanzania tuna matatizo kidogo, hatujitumi sana, tukijitolea tunaona moyo unaanza kufa. Vile vile katika mambo ya kulalamika kila mtu atalalamika, kiongozi analalamika, sasa malalamiko yanapelekwa wapi. Kwa hiyo, tuache tuige tabia ya wenzetu wa Korea kutokulalamika, kujitolea na kujituma, *otherwise* tutashirikiana pamoja, pengine watatuacha kwenye mataa, kwa utaratibu huu tutaingia kichwa kichwa hivi hivi tu kwa sababu wenzetu tayari wameshatoka mbali. Kwa hiyo, nitakayoyasema kwa utaratibu huu ni kwamba, tayari tunayo sera ya michezo, naipongeza Wizara ya Elimu na Utamaduni, lakini zile Wizara ambazo zinahusika na taasisi zinazohusika zishirikiane.

Tusiunde taasisi nyingine kwa ajili ya ushirikiano huu, taasisi hizi zitasimamia isije ikawa *creation of job* ya watu wakasema sasa tunaanzisha utamaduni na Korea kikaanzishwa kitengo kinaitwa Korea, hapana. Tunazo kwenye taasisi yoyote inakuja, utamaduni inakuja kwenye utamaduni, ikija mambo ya utalii kwenye utalii. Kwa hiyo, sekta mtambuka zinazohusika katika Tanzania zinashirikiana pamoja, nilisema utamaduni ni urithi na tabia T, A ni asili yako na M ni mila na ile A ni asili na D ni desturi na ile U ni urithi tena lakini urithi vitu unarithi N njia na ile I za kuishi unapata utamaduni. Kwa hiyo, *then transferable* huwezi ukachukua utamaduni wa nchi ya Korea ukapeleka nchi nyingine kule kwa utamaduni, tuwe waangalifu sana, siyo neno nyambuliko kwa utamaduni ni neno ambalo linamhusu mtu mwenyewe na kabila lake na eneo analoishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri, ana muda chini ya saa moja, ingawa kanuni inakuruhusu lakini una chini ya saa moja tumalize ili mchana iwe ni kazi ya ku-*wind* tu, nilitaka kulisema hilo. Suala lingine ambalo nadhani Waziri atalikumbushia ni Mkataba huu unaohusu *The Republic of Korea* siyo Korea ya Kaskazini kwa Kim III Sung ni Korea ya Kusini najua Waziri atafafanua lakini nilitaka kuweka hilo sawasawa. Mheshimiwa Waziri, mtoa hoja.

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuhitimisha hoja yangu na napenda nianze kwa kukushukuru sana kwamba, umenisaidia kufafanua kwamba Mkataba huu tunaouzungumzia ni kati ya nchi yetu na nchi inayoitwa Jamhuri ya Korea na Jamhuri ya Korea ni Korea ya Kusini tuliyoizoea kuiita kama Korea Kusini. Lakini pia ni ukweli unao fahamika sana kwamba, Korea hizi mbili ziko katika juhudi mbalimbali ya kujaribu kuunganisha Taifa lao liwe na nchi moja. Kwa hiyo, hata tukiwachanganya changanya basi ni katika mawazo ya kuwasaidia kwamba, wazidi kujiimarisha kuelekea kwenye nchi moja na sisi rafiki zao tungependa kuwasaidia ili siku moja tuweze kupata Taifa la Korea likiwa katika nchi moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, waliochangia katika hoja hii, tumepata mchango mzuri unaotupa mawazo, wengine wameuliza maswali nitajaribu kuyajibu, lakini kikubwa sana kutupa mawazo ya kuzingatia wakati wa utekelezaji wa Mkataba huu. Ninawashukuru waliochangia humu ndani kwa kuzungumza, wakiwemo Mheshimiwa Jumanne Hamisi Nguli, Kaimu Mwenyekiti wa Kamati, Msemaji Mkuu wa Upinzani, Mheshimiwa Khamis Ali Saleh, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mheshimiwa Edward Ndeka na Mheshimiwa Semindu Pawa, wote hawa nawashukuru sana kwa mchango wao kwa kuzungumza humu Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini napenda pia kumshukuru sana aliyechangia kwa maandishi naye ni Mheshimiwa Zabein Muhaji Mhita, kwa mchango wake ambao ningependa niseme kuwa umesaidia sana kukumbusha na ninapenda nisome sehemu ya hotuba yake alisema: "Bunge ni muhimu mambo haya yashughulikiwe haraka kwa msingi kuwa sehemu nyingine ya Mkataba inayohusu *Agreement on Economic, Scientific and Technical Co-operation,* umekwisha pitia hatua zote na ya mwisho ya *exchange of letters of ratification* imefanyika tarehe 21 Januari, 2005. Namshukuru sana kwa kutukumbusha kwamba, Mkataba wetu mwingine wa ushirikiano na nchi hii ya Korea umekwisha anza kutekelezwa na kwa kweli zikiangaliwa rekodi za Bunge hili, Mkataba huo ulikwisha ridhiwa na Bunge hili mnamo mwaka 2003, ushirikiano katika masuala ya uchumi na uko katika hatua za kutekelezwa. Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kutukumbusha hapa Bungeni angalau kwa maandishi. Kati ya waliochangia sijui kalamu yangu imeruka vipi, jina la Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, namshukuru sana kwa mchango wake.

Sasa ningependa kupitia angalau kwa haraka haraka nitazingatia muda lakini napenda nichukue baadhi ya *point* ambazo Waheshimiwa Wabunge, wamezitaja hasa zile ambazo naziona zinastahili majibu. Katika ushauri uliotolewa na Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, kuhusu jambo la kuhusisha pande zote mbili za Muungano. Ninapenda nilitaarifu Bunge kwamba, hata katika makubaliano katika hatua za mazungumzo, kumekuwa na ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapunduzi ya Zanzibar. Kwa hiyo, napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba, hata katika utekelezaji tutaendelea kushirikiana pande mbili za Muungano ili manufaa yapatikane kwa pande zote mbili za Muungano. Nawashukuru sana kwa kuwahimiza kwamba, Serikali tujitahidi kuwawezesha vijana wetu ili

wanufaike katika ushirikiano huu hasa katika maeneo ya kujitahidi kwa wanamichezo wetu kuinua vigezo vyao katika mashindano. Tutaangalia namna ya kutumia uzoefu wetu, uzoefu wa wenzetu wa Korea katika maeneo ambayo tuna hakika wao wanatuzidi.

Kuhusu yaliyosemwa na Kambi ya Upinzani, kwanza, napenda nimshukuru sana Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Khamis Ali Saleh, kwa kuunga mkono. Unajua kama mnazungumza jambo Bungeni halafu Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, anasema kwa uwazi kabisa kwamba, tunaunga mkono hoja hii, hilo ni jambo zuri, linaonyesha ushirikiano, sio kupingana katika kila jambo, kweli upande mmoja unaitwa Kambi ya Upinzani lakini sio kupingana katika kila jambo. Kwa hiyo, namshukuru sana na nawashukuru sana Wajumbe wote wa Kambi ya Upinzani, kwa kuliunga mkono Azimio hili.

Katika maeneo ambayo Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani ameonyesha mashaka ama katoa tafsiri ambazo zinahitaji kufafanuliwa, ningependa nimfafanulie hili suala la utamaduni, maana yake amesema Tanzania ina makabila, haina utamaduni wa Kitaifa. Sasa napenda nimfafanulie kwamba, utamaduni wa Taifa ni muunganiko wa hizo tamaduni za makabila yetu, ndipo tunapata utamaduni wa Taifa na kwa nchi kama yetu yenye makabila zaidi ya 120, badala ya kusema hatuna utamaduni wa Kitaifa, ukweli ni kwamba, tuna utamaduni wa Kitaifa ulio tajiri sana kwa sababu unachanganya tamaduni zote hizi 120 katika nchi yetu. Hata lugha hakuna sababu ya kuwa na wasiwasi kwamba katika lugha hizi Kinyamwezi, Kihehe, Kiha na Kimasai, tutatumia ipi, ni wazi kabisa sisi tunaunganishwa na lugha ya Kiswahili, ndio lugha yetu ya Taifa, lakini pia lugha ya Kiswahili hakuna mwenye nayo. Karibu kila kabila lina neno lake katika lugha ya Kiswahili. Makabila yetu mengi katika Tanzania ni ya Kibantu na lugha ya Kiswahili imejaa sana maneno ya Kibantu. Lakini lugha ya Kiswahili pia imepokea maneno kutoka hata kwa wageni wetu, waliokuja katika nchi yetu. Kuna maneno ya Kiarabu asilimia kubwa tu katika lugha ya Kiswahili, wanaochambua wengine wanasema yanaweza kufikia hata asilimia 20.

Lakini hawa ni wageni waliokuja wakakaribishwa, kwa hiyo, nao wana mchango katika lugha ya Kiswahili, lakini hata waliokuja kutawala tuliwaita wakoloni, wana mchango. Ndio maana utakuta maneno mengine ambayo tumeyachukua kwa wale waliotawala kwa sababu kulikuwa na vipindi ambapo Zanzibar na Tanganyika ilikuwa na watawala tofauti, kuna maneno mengine yamechukuliwa kutoka kwenye Kiingereza, Kijeremani, kwa mfano, neno shule, huku bara tunaita shule, tumetoa kwenye lugha ya Kijerumani. Lakini ukienda kwa wenzetu Zanzibar, wanasema skuli, wao wamechukua *school* ya Kiingereza. Kwa hiyo na lugha hizo nazo zimechangia katika kuitajirisha lugha yetu ya Taifa. Kwa hiyo, tunayo lugha ya Taifa na kujua lugha nyingine ni sehemu ya elimu ya mwanadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimezungumziwa Kituo cha Utamaduni cha Korea kwamba, kiko hapa kwa miaka kumi, kwa kweli kama alivyonisaidia Mheshimiwa Naibu Spika kufafanua, kile kilianzishwa na rafiki zetu wa Korea ya Kaskazini, inayojulikana kama *People's Democratic Republic of Korea.* Sasa ni kweli kama walivyosema wengine, kinatoa mafunzo ya lugha, lakini hilo hakuna ubaya kama nilivyosema, kujua

lugha ni sehemu ya elimu. Ningenpenda baada ya hapo nigusie baadhi ya maneno aliyoyazungumzia Mheshimiwa Raynald Mrope, kwa kutoa wito kwamba, katika ushirikiano huu ungelenga kusaidia Mikoa ya Kusini.

Ningependa kumfahamisha kwamba, kutokana na ule ushirikiano nilioueleza, aliotukumbusha Mheshimiwa Zabein Mhita, ushirikiano katika maeneo ya uchumi, sayansi na teknolojia, tayari Jamhuri ya Korea wamekwisha kubali kutusaidia kuanzisha vyuo vya *VETA* kule Lindi, ambayo mimi naamini Lindi iko Kusini alikokuwa anakuzungumzia Mheshimiwa Raynald Mrope, lakini ni pamoja na pia kuanzisha Chuo cha *VETA* kule Manyara na katika Mkoa wa Pwani, vyuo vitatu. Hili si jambo linalofikiriwa, ni jambo ambalo wamekwisha kubali kutusaidia angalau ni kwa njia ya mkopo na utekelezaji utaanza katika mwaka huu wa fedha, kujenga vyuo hivyo vitatu vya *VETA*.

Kwa hiyo, nilikuwa napenda nichukue nafasi hii, niwashukuru wenzetu wa Korea kwamba, tayari katika ule Mkataba mwingine wamekwisha anza kutusaidia. Suala la kuvutia watalii, Mkataba huu pamoja na kwamba ni wa utamaduni, nina hakika utasaidia kuvutia watalii. Sisi wenyewe tuyaone sasa maeneo yetu, kwa mfano, wenzetu wa Kusini kuna magofu ya Kilwa, haya sasa ni namna ya kubuni, tuna ushirikiano na Korea, tunaweza kusaidiana nao vipi au tunaweza ku-*promote,* tunaweza kukuza utalii vipi kwa kupitia magofu yale yaliyoko kule Kilwa. Kwa mfano, kukuza utalii, kuna mfano wa *Kilimanjaro Marathon* inayotangazwa tunaisikia hapa. Kwa mujibu wa Mkataba huu tunawaalika wenzetu wa Korea mlete washiriki katika *Marathon* ya Kilimanjaro. Sasa kama na wenzetu wanataka kuvutia na kuutumia Mkataba huu ni suala sasa la kuiona hii kama *opportunity,* kama fursa ya kubuni na kule Kusini kitu kinachofanana na *Kilimanajaro Marathon,* pengine siku moja tuwe na *Mtwara Marathon* au *Lindi Marathon,* ambayo inaweza ikavutia watalii chini ya Mkataba huu.

Napenda nimshukuru Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, kwa kutukumbusha namna Korea ambayo kwenye miaka ya 60, tulipopata Uhuru, hali yake ya uchumi ilikuwa kama ya kwetu, lakini wenzetu wamekwisha piga hatua mpaka wameondolewa kutoka nchi maskini wameingia kwenye nchi wahisani. Tunapokuwa na ushirikiano tunaweza kujifunza kwa undani zaidi kutoka kwa wenzetu, wamefanya vipi, wametumia mbinu gani na kwa sababu ni ushirikiano katika masuala ya elimu na tunaelewa wana vyuo kama vile *Economic Institute* ya Korea, basi hapo ni mahali ambapo na sisi tunaweza kwenda kujifunza mbinu walizozitumia kuweza kupata maendeleo ya haraka.

Kwa sababu katika Mkataba huu liko suala zima la kubadilishana wanafunzi, ninamshukuru Mheshimiwa Dr Masumbuko Lamwai, amefafanua vizuri sana nyanja tano za ushirikiano zilizoko na akasema ushirikiano usiwe wa upande mmoja, usiwe wa mkubwa na mdogo. Lakini mengine tumejibizana hapa hapa, nadhani Mheshimiwa Edward Ndeka, alipozungumza alisema haoni ubaya wa kushirikiana mkubwa na mdogo na mimi napenda nikubaliane naye na kwa kweli ungesema ushirikiano siku zote uwe baina ya maskini peke yao, unawezekana ukawa hauna faida kubwa.

Lakini kama mnashirikiana wakubwa na wadogo ni jambo zuri, kuna uwezekano wa mmoja kujifunza kutoka kwa mwenzake ni jambo zuri, hakuna ubaya na sitegemei kwamba, ushirikiano huu unaweza ukaleta *cultural imperialism* kama alivyosema Mheshimiwa Dr Masumbuko Lamwai. Wasiwasi umetolewa katika kifungu cha tatu, nafikiri hata Mheshimiwa Dr Willbrod Slaa naye alisema lakini kifungu hiki Waheshimiwa Wabunge ukikisoma vizuri, nadhani hakina wasiwasi wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako, napenda nikinukuu kama kilivyoandikwa: *"The contracting parties shall study the question of mutual recognition of academic degrees, shall study"* hili ndiyo jambo watakalolifanyia kazi. Tunakubaliana kwamba, jambo hili tutalichunguza tushirikiane vipi. Sasa katika kulichunguza, upande wa Serikali hatuachi vile vyombo ambavyo tumeviunda kwa ajili ya kazi hiyo, tunalo Baraza la Ithibati ya Elimu ya Juu, ama kwa Kiingereza, *Higher Education Accreditation Council.* Hicho kitakuwa ndiyo chombo cha Serikali ambacho kitashiriki katika hili suala la kujifunza zaidi ili tukubaliane tutashirikiana vipi. Kwa hiyo, napenda kusema Waheshimiwa Wabunge, hawana sababu ya kuwa na wasiwasi juu ya jambo hili.

Vile vile Mheshimiwa Dr Willbrod Slaa, alizungumzia juu ya vyuo vya michezo, napenda kumfahamisha kwamba, tayari tuna mazungumzo na wenzetu wa Korea, kuangalia namna ya kutusaidia katika Chuo Chetu cha Michezo cha Malya, ambacho tunakwenda nacho kinasuasua lakini tumeanza kuzungumza nao namna wanavyoweza kutusaidia kwa sababu katika eneo hili wana uzoefu mkubwa zaidi. Vile vile alizungumzia pia juu ya kukuza utalii, njia moja iliyo wazi ni katika maeneo ya mambo ya kale kuyatumia kama vivutio kwa mfano, tuna *Olduvai Gorge,* ambayo iko karibu kabisa na kwake kule Mheshimiwa Dr Willbrod Slaa, kuna michoro ya mapangoni hapa Kondao Iangi ni kivutio kwa watalii, tuna magofu ya Kilwa ambayo nimekwisha yasema ama yale magofu ya kule Kaole na Bagamoyo, vyote hivi vinaweza vikatumika chini ya Mkataba huu kukuza utalii wa kutembelea katika maeneo hayo bila kusahau yale makazi ya watu wa zamani yaliyoko kule Isimila katika Mkoa wangu wa Iringa. Maeneo yote haya ya mambo ya kale yanaweza yakatumika kukuza utalii.

Ninapenda nimshukuru Mheshimiwa Edward Ndeka, yeye ametukumbusha kwamba, tuna shida kubwa sana ya maktaba nyingi ziko mijini, kwa hiyo, jambo hili la maktaba limo katika ushirikiano huu. Sasa mimi ninachoweza kusema hapa nikumbushe kwamba, suala la uanzishwaji wa maktaba ni miongoni mwa majukumu ya Halmashauri zetu za Wilaya na sisi Wabunge kama Wajumbe wa Halmashauri zetu za Wilaya na sisi ndiyo tunalipitisha hili Azimio ni suala la kuiona hii kama ni fursa. Mkataba huu ama Azimio hili ni fursa ya ushirikiano wa kutuwezesha kuanzisha miradi ya maktaba. Kilichowezekana mpaka nikasema leo hii Korea inatusaidia kuanzisha vyuo vya *VETA* kule Lindi, Pwani na Manyara, ningependa siku moja niweze kusema hapa Bungeni, Korea wanatusaidia kuanzisha maktaba katika wilaya hii na ile na ile.

Tuione hii kama ni *opportunity* ya kuweza kwenda kukaa katika Halmashauri zetu, tukaanzisha hii miradi ya maktaba na Wizara yangu iko tayari kushirikiana na Halmashauri ambayo wanataka kuanzisha mradi wa namna hiyo kwa sababu katika

Wizara, tunao utaalam, tunayo *Tanzania Library Service* chini ya Wizara, ambayo inayo wataalam wanaoweza kuisaidia Halmashauri au Halmashauri kadhaa, wakaanzisha mradi wetu na sisi Wizara tukauuza mradi huu chini ya makubaliano yaliyo katika Mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, tushirikiane tupitishe Azimio hili kwa maana ya kwamba katika utekelezaji wake tutaendelea kuangalia tunayoweza kuyatumia kwa faida ya kukuza udugu na ushirikiano wetu na ndugu zetu hawa wa Korea. Lakini pia kwa faida ya kusukuma maendeleo katika wilaya zetu na maendeleo katika nchi yetu katika nyanja zote zinazozungumziwa katika Mkataba huu. Namshukuru sana Mheshimiwa Semindu Pawa, kwa mengi aliyoyasema tena ameyasema kwa *speed* kubwa hata siwezi kuyarudia hapa kwa sababu mimi ni Mbunge wa miaka mingi kidogo, nadhani mwaka huu natimiza miaka 30.

Lakini naweza kusema kwamba, Mheshimiwa Semindu Pawa, anashika rekodi ya kusema maneno kwa lugha ya Kiswahili kwa haraka kuliko Mbunge mwingine yeyote ninayemfahamu katika Bunge hili na inawezekana hata katika Jumuiya ya Madola kwa sababu nimewasikia Wabunge wengi wanapohutubia katika Mabunge yao. Wazo lake la kwamba, ingefaa tuwe na Redio Sauti ya Kiswahili Korea, tumelisikia wazo hilo, tutaangalia namna linavyoweza kuzingatiwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote, kwa mchango wao hata kama sikujibu moja moja, nina timu nzima hapa ya wataalam kutoka kwenye Wizara zote nne zinazohusika na utekelezaji wa Mkataba huu, wako pale wamekuwa wakichukua *notes,* wamenisaidia kunipa majibu. Lakini kwa kulinda wakati, siwezi kuyatumia yote lakini nawahakikishieni kwamba, wataalam kutoka kila Wizara wako hapa na wamechukua ushauri na mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge na katika utekelezaji wa Mkataba huu tutayazingatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo naomba kutoa hoja.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la Kuridhia Mkataba wa Ushirikiano na Utamaduni Kati ya Tanzania na Jamhuri ya Korea liliridhiwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, baada ya kufika hapo, sasa nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni tutakapomaliza shughuli zote za kikao hiki.

*(Saa 06.27 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kikao kilichoanza asubuhi sasa kinaendelea.

**ND. DAMIAN FOKA - KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, shughuli zilizokuwa zimepangwa kufanyiwa kazi na Bunge katika Mkutano wake wa Kumi na Nane sasa zimemalizika.

**SPIKA:** Kwa taarifa hiyo, sasa namwita Mheshimiwa Waziri Mkuu, atoe hoja ya kuahirisha Bunge. *(Makofi)*

## KUAHIRISHA BUNGE

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nami niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kutoa pole kwa familia na Wananchi wa Jimbo la Kasulu Mashariki, kufuatia kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Jimbo hilo, Marehemu Mheshimiwa Frank Mussati, kutokana na ajali ya gari.

Aidha, nawapa pole Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, Mbunge wa Muhambwe na Mheshimiwa Benito Malangalila, Mbunge wa Mufindi Kusini, kwa kufiwa na wake zao na vilevile Mheshimiwa Daniel Yona, Mbunge wa Same Mashariki na Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, Mbunge wa Kikwajuni, kwa kufiwa na wazazi wao. Mwenyezi Mungu, azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. *(Amin)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Ndugu Damian Foka, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Katibu wa Bunge. Ndugu Damian Foka anajiunga kwenye utumishi wa Bunge akiwa na utaalamu na uzoefu mkubwa wa masuala ya uongozi na utawala. Tunategemea kuwa atatumia utaalamu na uzoefu huo katika kuwasaidia na kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge, kutekeleza majukumu yao kikamilifu. Tunamkaribisha tena na tunamtakia kila la kheri katika kazi yake mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumehitimisha shughuli zote zilizokuwa zimepangwa kutekelezwa katika Mkutano huu wa Kumi na Nane wa Bunge lako Tukufu. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kupitishwa kwa Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Kumi na Nne katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa mwaka 2004. Miswada mingine minne na Maazimio manne yamepitishwa. Serikali vilevile imejibu maswali ya msingi 111 na mengine mengi ya nyongeza. Kwenye majibu ya maswali hayo, Serikali imetoa maelezo kuhusu hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali katika kuondoa kero zinazowakabili Wananchi. Aidha, majibu hayo yameeleza japo kwa ufupi, mafanikio yaliyopatikana katika nyanja mbalimbali katika utekelezaji wa Ilani za Uchaguzi za Chama cha Mapinduzi. Bunge lako Tukufu vilevile lilipokea taarifa kuhusu kutiwa saini na Mheshimiwa Rais kwa Miswada sita iliyopitishwa na Bunge katika Mkutano wake wa 17 na hivyo Miswada hiyo sasa ni sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Kumi na Nne ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa mwaka 2004, kama alivyoeleza Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, Mheshimiwa Bakari Mwapachu, una lengo la kuendelea kutekeleza maoni ya Wananchi yaliyotokana na Waraka wa Serikali Na. 1 wa mwaka 1998. Hivyo, mabadiliko tuliyoyapitisha ni sehemu ya maoni yaliyotolewa na Wananchi na tutaendelea kufanya hivyo kutegemeana na hitaji la wakati husika.

Napenda kutumia fursa hii, kukupongeza sana Mheshimiwa Spika, kwa kuiwezesha Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Bunge lako Tukufu kukusanya maoni ya Wananchi na makundi mbalimbali ya jamii kuhusu Muswada huo, kutoka katika maeneo mengi nchini kadri ilivyowezekana. Hii inaonyesha jinsi Bunge lako Tukufu lilivyoupa umuhimu unaostahili Muswada huu. Mabadiliko ya Katiba yoyote yanafanywa kwa kuzingatia hali ya kisiasa, kiuchumi na kijamii ya wakati huo. Nchi yetu ina umri wa zaidi ya miaka 43 tangu tupate uhuru. Katika kipindi chote hicho, tumefanikiwa kuweka misingi imara ya mfumo wa sheria, kanuni na taratibu zinazotuongoza katika shughuli zetu zote za maendeleo. Kwa hiyo, dhana ya mabadiliko ni ya lazima kila mara kwa vile mazingira ya ndani na nje yanabadilika tena kwa haraka sana na hivyo kutuhitaji nasi kama Taifa kila mara kupitia sheria, kanuni na sera mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha kuwa zinaendana na mazingira ya wakati huo. Aidha, kadri tunavyoimarisha misingi ya Utaifa na Umoja wetu ndivyo tunavyoweza kufanya mabadiliko mengi na makubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya mabadiliko muhimu yaliyofanywa katika Katiba ni pamoja na kuongeza Viti Maalum vya Wanawake kutoka asilimia 20 hadi asilimia isiyopungua 30 na katika Wabunge 10 wa kuteuliwa na Rais, watano lazima wawe Wanawake. Aidha, kati ya Wabunge 5 wa kuteuliwa na Baraza la Wawakilishi, wasiopungua wawili lazima wawe Wanawake. Tulikwishaamua kuwa Wanawake wasiendelee kuwekwa pembeni katika uongozi wa nchi, hivyo, mabadiliko haya yanatekeleza azma hiyo. Jambo hili pia ni muhimu kwa kuharakisha maendeleo ya nchi yetu. Mabadiliko mengine yameweka wazi zaidi haki ya mtu kuabudu dini atakayo na mipaka yake na haki ya kujiunga katika vyama vya siasa. Badiliko lingine limemruhusu Waziri Mkuu kukaimu kazi za Rais endapo Rais na Makamu wake hawatakuwepo nchini. Badiliko hili linaimarisha misingi ya kutenganisha madaraka kati ya mihimili mitatu ya dola. Maeneo mengine yamehusu eneo la Majaji na Mahakama ambapo Miswada ihusuyo mabadiliko hayo nayo imepitishwa na Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu siku zote inasikiliza na kujali mawazo ya Wananchi na makundi mbalimbali ya jamii yetu. Hupokea ushauri na mapendekezo mbalimbali kuhusu sheria na sera zetu na kila inapowezekana kuyazingatia. Naomba tuendelee kuimarisha misingi ya demokrasia tunayoijenga ili tuweze kuendeleza taratibu tulizojiwekea za kuwashirikisha wadau mbalimbali katika harakati za maendeleo yetu.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu limepitisha vilevile Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Mwaka 2005. Marekebisho yaliyopendekezwa katika Muswada yana lengo la kuweka mazingira yatakayowezesha kufanyika kwa uchaguzi kwa uhuru zaidi na

vilevile kuhakikisha kuwa, kila atakayeshiriki katika zoezi la uchaguzi anapata haki anayostahili.

Tumesikia mara kwa mara malalamiko kuhusu kuundwa kwa kile kinachodaiwa "Tume Huru". Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Tume ya Uchaguzi tuliyonayo hivi sasa ni huru na inatoa maamuzi yake bila shinikizo kutoka sehemu yoyote ya nguzo yoyote ya dola au chama chochote cha siasa. Mapendekezo ya Muswada yana lango la kuzidi kuongeza imani ya wadau wote wa demokrasia nchini kuhusu usimamizi na uendeshaji wa shughuli za Uchaguzi. Hata hivyo, sheria ilivyo hivi sasa, inavipa vyama vya siasa fursa ya kuwa na wakala wao katika hatua mbalimbali za uchaguzi tangu uandikishaji hadi uhesabuji wa kura. Tatizo lililopo ni la baadhi ya wagombea au vyama vyao, kukataa matokeo kwa visingizio mbalimbali. Wanaomwezesha mgombea kushinda ni wapiga kura baada ya kupima Sera na Ilani ya Chama husika na sifa na uwezo wa mgombea mwenyewe. Wajibu wetu hasa wanasiasa ni kuheshimu uamuzi halali wa wapiga kura.

Hata hivyo, ipo dhana inayojengwa kila mara kuwa mgombea wa upinzani akishinda, uchaguzi unaelezwa kuwa ni huru na wa haki, lakini mgombea wa Chama Tawala akishinda, hata kama ni kwa asilimia kubwa, uchaguzi huo huhesabiwa kuwa sio huru na wa haki hasa katika nafasi ya Urais. Wito wangu kwa viongozi wa vyama vyote vya siasa, wanachama na wapenzi wa vyama mbalimbali vya siasa ni kuwa tushirikiane kwa dhati katika kujenga misingi imara ya demokrasia yetu na tukubali kuwa kushinda na kushindwa ni sehemu muhimu ya mchakato wa uchaguzi. Sheria zetu zimeweka mazingira kwa wale wanaoona hawakutendewa haki, kuitafuta haki yao kwenye vyombo vya sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Muswada mwingine uliopitishwa ni ule wa Sheria inayoainisha Masuala ya Kiutawala na Kinidhamu ya Majaji, Wasajili na utaratibu wa Ajira, Utumishi na Nidhamu katika Mahakama. Katika mazingira ya ndani na nje ya nchi yetu, tunao wajibu mkubwa kama Taifa wa kuziimarisha nguzo zote au mihimili yote mitatu ya dola ili iweze kutekeleza majukumu yao kikamilifu. Mahakama ni chombo muhimu sana katika suala la utoaji haki kwa Wananchi wetu. Pamoja na kutumia uwezo wetu na misaada kutoka kwa washiriki wetu wa maendeleo kuimarisha Mahakama kwa kuzipa vitendea kazi na kuongeza ajira ya Mahakimu na Majaji, bado upo umuhimu wa kuipa Mahakama nguvu ya kisheria ya kutekeleza wajibu wake kikamilifu. Serikali itaendelea kushirikiana na mihimili mingine ya dola katika kuiwezesha kutekeleza majukumu yao vema.

Mheshimiwa Spika, katika mazingira ya utandawazi na mabadiliko makubwa ya kiteknolojia yanayotokea nchini, masuala ya kisheria yanayohusu Serikali yanaongezeka na hivyo kuhitajika kupata ushauri katika ngazi mbalimbali. Muswada wa Sheria inayoainisha Majukumu ya Kazi za Mwanasheria Mkuu wa Serikali wa Mwaka 2005 unakusudiwa kuweka mazingira ya kiutawala na kiuendeshaji yanayomwezesha Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wanasheria wengine kuishauri Serikali ipasavyo. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, kama ambavyo imekuwa ikifanya

wakati wote, Serikali itaendelea kuzingatia na kusimamia utawala unaoheshimu na kufuata sheria na Katiba ya Nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tarehe 14 Desemba, 2004, Waziri wa Elimu na Utamaduni, Mheshimiwa Joseph Mungai, alitangaza matokeo ya Mtihani wa Taifa wa Darasa la Saba wa mwaka 2004. Matokeo ya mtihani huo yamelipa Taifa letu changamoto zaidi ya kuwekeza katika elimu katika ngazi zote. Taarifa hiyo ilionyesha kuwa idadi ya wanafunzi waliofaulu imeongezeka kutoka asilimia 27.4 mwaka 2002 ambao ndio mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) hadi asilimia 48.6 mwaka 2004. Haya ni mabadiliko makubwa sana. Tafsiri ya hali hii ni kuwa idadi ya wanafunzi wanaofaulu kuingia Elimu ya Sekondani inaongezeka maradufu. Aidha, takwimu hizo pia zimetuonyesha kuwa idadi ya wanafunzi wa kike wanaofaulu imeongezeka mara mbili kutoka asilimia 20.11 mwaka 2002 hadi asilimia 41.84 mwaka 2004. Napenda kutumia fursa hii kuwapongeza kwa dhati walimu wetu wote na uongozi wote wa elimu nchini, nawahakikishia kuwa Taifa linatambua na kuthamini sana kazi nzuri wanayoifanya. Wito wangu kwao ni kuwa matokeo haya mazuri tuyaendeleze ili wanafunzi wa kwanza wa mpango wa MMEM watakapohitimisha masomo yao ya Elimu ya Msingi, kiwango cha kufaulu kiwe kikubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafanikio hayo makubwa katika Elimu ya Msingi, yanatutaka sasa tuelekeze nguvu zetu katika Elimu ya Sekondari. Kama sote tunavyofahamu, idadi kubwa ya wanafunzi wa darasa la saba waliofaulu nchini kote, wanakosa nafasi ya kuendelea na Elimu ya Sekondari. Naomba nitoe mfano wa mkoa mmoja tu ili kuelezea hali iliyopo sehemu nyingi nchini. Katika Mkoa wa Shinyanga kwa mfano na hali hii inafanana kwa mikoa mingi, katika mwaka wa 2004, jumla ya wanafunzi 40,332 walifanya mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi. Kati yao, wanafunzi 17,492 ambayo ni asilimia 43.4 walifaulu mtihani huo. Hata hivyo, kutokana na upungufu wa Shule za Sekondari ni wanafunzi 4,721 tu ambao ni sawa na asilimia 27 ya wale waliofaulu, ndio waliochaguliwa kujiunga na Kidato cha Kwanza. Ili kukabiliana na ongezeko kubwa la wanafunzi wanaofaulu, tunayo kazi kubwa sasa ya kuongeza juhudi zetu katika ujenzi wa shule mpya za Sekondari, kuongeza vyumba vya madarasa katika shule zilizopo, kujenga maabara na mahosteli, hususan kwa ajili ya wanafunzi wa kike na kuajiri walimu wengi zaidi.

Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES) umeshaanza. Katika mpango huo, Serikali inatoa ruzuku ya maendeleo ya shilingi milioni 7 kwa ujenzi wa darasa na shilingi milioni 9 kwa ujenzi wa nyumba ya mwalimu kwa shule zilizojengwa na wananchi. Serikali imeshatoa zaidi ya shilingi 22 bilioni kwa mikoa yote nchini ikiwa ni ruzuku kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa na nyumba za walimu. Hata hivyo, napenda kusisitiza kuwa, uzoefu wetu wakati wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM), umeonyesha kuwa pale Wananchi waliposhiriki kikamilifu kwa kutumia nguvukazi yao na hata kuchangia upatikanaji wa baadhi ya vifaa, wameweza kutumia fedha zilizotolewa na Serikali kwa ufanisi mkubwa sana uliowezesha ongezeko la vyumba vya madarasa na hata nyumba za

walimu. Aidha, mchango wa Serikali unapelekwa pale tu ambapo Wananchi wameonesha juhudi za kuanza kujenga shule zao.

Kwa msingi huo, Wilaya yenye Miradi mingi ya Shule za Sekondari za Wananchi zinazojengwa, zitapata mgao mkubwa zaidi wa fedha kuliko zile ambazo zina miradi michache. Wito wangu kwa viongozi wa kisiasa na Watendaji Wakuu wa Serikali Mikoani na Wilayani ni kuwa, tuwahamasishe Wananchi waanzishe Miradi ya Ujenzi wa Shule za Sekondari. Nataka kusisitiza kuwa shilingi 7 milioni au shilingi 9 milioni zinazotolewa kwa ujenzi wa chumba cha darasa au nyumba ya mwalimu, siyo agizo kuwa fedha hizo zitumike kujengea jengo hilo moja tu bali zisijenge chini ya hapo, lakini fedha hiyo inaweza kujenga zaidi ya jengo hilo moja kwa kushirikiana na nguvu za Wananchi na kwa kubana matumizi. Tusipofanya hivyo, mikoa yetu itaanza kupishana katika maendeleo ya elimu na pia katika maendeleo ya kijamii kwa ujumla. Kupishana sana kwa maendeleo baina ya maeneo au mikoa ndani ya nchi moja ni hatari hata kwa amani na usalama wetu. Kwa msingi huo, ni vema tuanze sasa kutekeleza kwa nguvu zetu zote, Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari ili tuweze kukabiliana na hali hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio mazuri, tunalo tatizo kubwa la utoro kwenye shule zetu za msingi. Utoro huo unasababisha wanafunzi kuacha shule kabla ya kuhitimu elimu hiyo ya msingi. Ingawa takwimu za Wizara ya Elimu zinaonesha kuwa tatizo hilo limeanza kupungua katika miaka mitatu mfululizo kuanzia mwaka 2002, bado hali ni mbaya. Kwa mfano, wanafunzi waliomaliza darasa la saba mwaka 2004 walianza darasa la kwanza mwaka 1998 wakiwa 691,982, lakini waliomaliza mwaka 2004 walikuwa 499,241 tu, ambao ni asilimia 72.2. Kwa hiyo, asilimia 27.8 ya wanafunzi walioanza Elimu ya Msingi mwaka 1998 hawakumaliza elimu hiyo. Yapo matatizo ya ajira ya watoto ambao yanawavutia wanafunzi kuacha shule, lipo pia tatizo la watoto wa kike kupata mimba. Ni wajibu wa wazazi, viongozi wa vijiji, yaani Maafisa Watendaji wa Vijiji na Kata, kuhakikisha kuwa kila mtoto wa Taifa letu anapata fursa ya kumaliza Elimu ya Msingi. Ni wajibu wetu wote kupambana na wale wote wanaosababisha wanafunzi kuacha shule.

Mheshimiwa Spika, nilipokuwa nahitimisha hoja ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu katika Mkutano wa Kumi na Sita, niliahidi kuunda Kamati itakayodurusu utekelezaji wa Sera ya Madini, kwa lengo la kuchambua na kutathmini kwa pamoja hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge na Wadau wengine kuhusu mwenendo wa sekta ya madini nchini. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati hiyo imehitimisha kazi yake na imenikabidhi taarifa yake tarehe 4 Februari, 2005. Taarifa hiyo imegusa maeneo mengi yanayohusiana na uchimbaji wa madini. Serikali itaifanyia kazi taarifa ya Kamati kwa lengo la kupunguza malalamiko mbalimbali yaliyojitokeza kuhusu mwenendo wa sekta hiyo ili iendelee kuwa kichocheo cha ukuaji wa uchumi wetu. Napenda kuipongeza Kamati hiyo iliyoongozwa na Dr Jonas Kipokola, kwa kazi nzuri waliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kazi zote zinazotekelezwa na Serikali kwa ushirikiano na Wananchi, taasisi mbalimbali na washiriki wetu wa maendeleo, zina lengo kuu la

kupunguza na hatimaye kutokomeza umaskini. Moja ya vikwazo vikubwa katika mapambano yetu dhidi ya umaskini ni ongezeko kubwa la idadi ya watu lisilooana na ongezeko la ukuaji wa uchumi. Matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2002 yanaonyesha kuwa wastani wa ongezeko la idadi ya watu nchini ni asilimia 2.9. Ipo Mikoa yenye ongezeko la idadi ya watu la asilimia 4.8. Hili ni ongezeko kubwa na ambalo matokeo yake yanajitokeza katika umri wa makundi maalum. Matokeo hayo ya Sensa yalionesha vilevile kuwa, watoto katika kundi la umri wa miaka 0 - 14 ni asilimia 44 ya idadi ya watu nchini. Hili ni kundi kubwa na lisilozalisha ambalo linahitaji kuhudumiwa. Kundi hili linahitaji lishe, huduma za afya, elimu na huduma nyinginezo.

Kwa upande wa elimu, hili ndilo kundi lililopo kwenye Elimu ya Msingi.

Kwa hiyo, pamoja na nguvu tunazoziweka katika kupanua huduma za jamii hususan elimu, tunao wajibu sasa wa kuongeza na kuelekeza nguvu zetu katika kutoa elimu na huduma za uzazi wa mpango kwa Wananchi wetu. Ni wajibu wetu sisi viongozi kuwaelimisha na kuwahamasisha Wananchi, watambue umuhimu wa kila familia kupata idadi ya watoto ambao ina uwezo wa kuwahudumia. Tusipochukua hatua hizo, vita vyetu dhidi ya umaskini vitakuwa vigumu na vya muda mrefu sana. Huduma za uzazi wa mpango hivi sasa zimefikishwa hadi ngazi ya zahanati na vituo vya afya, kwenye vijiji na mitaa yetu. Wapo wataalamu wa afya ambao wanaweza kuwasaidia Wananchi kwa kuwapa elimu. Ni wajibu wetu sisi viongozi wa kisiasa kutoogopa kulisemea hili na kuwasaidia Wananchi kutambua umuhimu wa uzazi wa mpango na uhusiano wake na vita dhidi ya umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zoezi la uandikishaji wapiga kura katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura linaendelea vizuri. Hivi sasa zoezi hilo limekamilika katika Kanda nne za Kusini, Nyanda za Juu Kusini, Kanda ya Kati na Kanda ya Ziwa. Kwa ujumla idadi ya Wananchi waliojiandikisha katika Kanda hizo ni 10,306,048, ambayo ni sawa na asilimia 94.9 ya Wananchi waliotarajiwa kujiandikisha. Jambo hili la Wananchi kujua umuhimu wa kujiandikisha ili hatimaye kupiga kura, linatia moyo sana. Napenda kutumia fursa hii, kuipongeza Tume ya Taifa ya Uchaguzi, kwa kazi nzuri ambayo wameshaifanya hadi hivi sasa. Tume imeweza kuchukua hatua za haraka kila palipotokea tatizo na hivyo kuwezesha zoezi hilo kuendelea. Zoezi la uandikishaji katika Kanda zilizobaki ni kama ifuatavyo:-

Kanda ya Kaskazini, yenye Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara na Tanga, inatarajiwa kuanza tarehe 19 Februari, 2005 hadi tarehe 11 Machi, 2005. Kanda ya Mashariki yenye Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Morogoro, itaanza kuandikishwa tarehe 29 Machi, 2005 hadi tarehe 18 Aprili, 2005. Aidha, uandikishaji kwa upande wa Tanzania Zanzibar kwa ajili ya Uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano na Wabunge, utaanza baada ya zoezi hilo kukamilika kwa upande wa Bara. Napenda kutoa wito maalumu kwa Wananchi wa Kanda hizo nao kujitokeza kwa wingi kama Watanzania wenzao walivyofanya. Tukumbuke kuwa hii ndiyo fursa pekee ya kuweza kujihakikishia kushiriki katika zoezi la upigaji kura katika Uchaguzi Mkuu mwezi Oktoba, 2005. Natoa wito maalumu kwa viongozi wote wa vyama vya siasa kuendelea kuwahamasisha Wananchi katika kanda ambazo zoezi hilo bado halijafanyika kujitokeza

kwa wingi kujiandikisha. Aidha, tuwakumbushe Wananchi kila mara umuhimu wa kuhifadhi vitambulisho vyao vya kupigia kura ili waweze kuvitumia wakati huo kwa chaguzi zijazo. Vilevile, tuhimize na kuwaelimisha Wananchi umuhimu wa kufuata na kuzingatia sheria kwa kukwepa vitendo vyovyote vyenye kuashiria udanganyifu au fujo katika vituo vya kuandikisha wapiga kura.

Mheshimiwa Spika, huu ni Mkutano wa Kumi na Nane wa Bunge lako Tukufu, bado tuna mikutano miwili tu kabla Bunge hili halijafika mwisho wa uhai wake. Vuguvugu la uchaguzi limeshaanza katika ngazi mbalimbali. Katika kipindi cha takriban miezi minane ijayo, joto la uchaguzi litakuwa linapanda kadri tunavyokamilisha hatua moja baada ya nyingine kuelekea kilele cha uchaguzi. Katika vuguvugu hilo ni lazima vilevile shughuli zetu mbalimbali za ujenzi wa Taifa ziendelee. Viongozi na Watendaji Wakuu wa maeneo ya kazi wanalo jukumu la kuhakikisha kuwa, vuguvugu la uchaguzi halikwamishi shughuli zozote za Serikali wala za Wananchi. Joto la uchaguzi huweza vilevile kusababisha vitendo vya uvunjifu wa amani. Wito wangu kwa Watanzania ni kuwa, tuendelee kujadiliana kuhusu mustakabali wa uongozi wa nchi yetu kwa amani. Tujenge hoja zetu na kuzitetea kwa maelezo ya kushawishi bila kutumia fujo au nguvu.

Mheshimiwa Spika, nafasi za uongozi zina ushabiki mkubwa hasa ngazi ya Urais. Ni vema wanaowania nafasi hizo wawe na busara za kuona na kutambua hilo. Kwa mfano, jambo hili likichanganywa na hisia au miekeleo ya udini, ukabila au ukanda, ni hatari sana kwa imani yetu. Napenda nirudie tena jambo ambalo nimelisema mara nyingi kuwa, hakuna dini yoyote, kabila lolote, wala ukanda wowote katika nchi hii, wenye uwezo wa kumweka Rais wa nchi yetu peke yake. Rais atakuwa tu yule ambaye anavuka mipaka ya hayo yote. Kama vinavyotuambia vitabu vyetu vitakatifu, viongozi wa nchi huteuliwa na Mwenyezi Mungu. Basi tumwombe Mungu, atuteulie kiongozi mzuri, atakayedumisha amani na kusimamia maendeleo ya Watanzania. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, taarifa mbalimbali kuhusu vuguvugu hili zinawafikia Wananchi kupitia vyanzo mbalimbali vikiwemo vyombo vya habari. Vyombo vya habari vina wajibu mkubwa zaidi wakati huu. Ni vema wamiliki wa vyombo vya habari na waandishi wa habari kwa ujumla, watambue kuwa wao ni Watanzania wenye nafasi na dhamana muhimu sana katika kuwaelimisha Wananchi wenzao waweze kutumia kura zao kwa uangalifu. Ninawasihi sana waepuke lugha za uchochezi na waweke maslahi ya Taifa letu mbele katika habari wanazozipata kwenye vyombo vyao katika kipindi hiki. Tunajua huu ni wakati mzuri wa biashara ya magazeti yetu, lakini hitaji la kuuza gazeti lisisababishe mfarakano katika jamii. Tuelewe kuwa hii ni nchi yetu sote na kwamba, uchaguzi ni utaratibu tu wa kubadilisha uongozi wa nchi katika ngazi mbalimbali na kamwe usiwe chanzo cha mfarakano au chuki miongoni mwetu. *(Makofi/Kicheko)*

Kwa mantiki hiyo, kila raia wa Tanzania ana jukumu la kulinda amani hii kwa nguvu zake zote. Kwa wale wanaoweza kumwomba Mwenyezi Mungu, kwa ajili ya amani ya nchi yetu, wafanye hivyo. Wanaoweza kuwaelekeza wengine njia bora za kuishi kwa amani, wafanye hivyo na wale wa kuonya wengine wafanye hivyo hivyo. Kama italazimu, basi wale wa kutoa adhabu kwa wanaokaidi utaratibu huo, itabidi nao

wafanye hivyo hivyo. Mwisho wa yote, napenda kuwahakikishia Watanzania wote kuwa, mwenye dhamana ya kulinda amani hii ni Serikali iliyoko madarakani, kwa kushirikiana na raia wote wema, kwa maslahi ya umma na vyombo husika vya Serikali vya usalama vitaendelea kuimarishwa ili kutekeleza kwa ukamilifu jukumu hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwishoni mwa mwezi Januari, 2005, Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini, imetoa tahadhari kuhusu uwezekano wa baadhi ya maeneo ya nchi yetu, kupata mvua nyingi kuliko kawaida na hivyo kusababisha mafuriko. Katika tahadhari hiyo, Mamlaka imeeleza wazi kuwa, Wananchi waliojenga na kuishi kwenye mabonde wako katika hatari zaidi. Tatizo la Wananchi kuishi kwenye mabonde yenye kupitisha maji mengi wakati wa masika, linaendelea kuongezeka katika maeneo mengi nchini. Tatizo hili ni kubwa zaidi katika baadhi ya miji yetu, hususan Jiji la Dar es Salaam, ambapo watu wamediriki hata kujenga nyumba za kudumu katika maeneo ambayo yanaeleweka wazi kuwa ni mkondo wa maji wakati wa masika. Halmashauri zetu zote zimepewa mamlaka Kikatiba na Kisheria, kusimamia shughuli zote za maendeleo ya Wananchi.

Maendeleo ya matumizi ya ardhi katika miji yanaongozwa na mipango yenye kugawa matumizi ya ardhi kwenye miji kwa ajili ya shughuli mbalimbali. Aidha, yapo maeneo yanayotengwa mahsusi kuwa hayafai kwa shughuli zozote. Kwa msingi huo, moja ya majukumu ya Mabaraza ya Madiwani ya Halmashauri zote nchini ni kusimamia kikamilifu matumizi ya ardhi ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa yale maeneo yote yaliyoainishwa kuwa ni hatari na hayafai kwa makazi ya watu yanabaki tupu. Tatizo kubwa lililopo katika baadhi ya Halmashauri zote nchini ni kusimamia kikamilifu matumizi ya ardhi ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa yale maeneo yote yaliyoainishwa kuwa ni hatari na hayafai kwa makazi ya watu yanabaki tupu. Tatizo kubwa lililopo katika baadhi ya Halmashauri zetu ni usimamizi hafifu wa sheria za mipango miji. Pale wanapojitokeza baadhi ya Wananchi na kuvunja sheria na taratibu na kuanza kujenga kwenye maeneo hayo, hatua za haraka zichukuliwe mara moja na tusitoe mwanya hata kidogo kwa wakorofi wachache wanaotaka kuharibu matumizi ya ardhi kwenye miji yetu. Uongozi wa Mikoa yote nchini na hususan Mamlaka za Halmashauri, zianze sasa kuchukua hatua za kuwaondoa taratibu Wananchi wanaoishi mabondeni na kuwapangia maeneo au viwanja mwafaka vya kujenga nyumba zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuhitimisha hoja yangu, ningependa kusugia mambo machache yafuatayo:-

Kwanza, ni utaratibu wetu wa kupitisha Miswada ya Sheria. Tarehe 7 Februari, 2005 wakati tulipokuwa katika hatua za mwisho za kupitisha Muswada wa Sheria wa Mabadiliko ya Kumi na Nne ya Katiba, wakati Mheshimiwa Spika unatuhoji, Waheshimiwa Wabunge wa Upinzani, walikuwepo wote isipokuwa wawili walitoka nje. Hii ilikuwa kabla ya hatua ya Kamati ya Bunge Zima. Itakumbukwa kuwa, asubuhi ya siku hiyo tuligawiwa hoja mbalimbali za mabadiliko katika Muswada zilizopendekezwa na Waheshimiwa Wabunge wa Upinzani na wa Chama Tawala. Kwa utaratibu wa Kanuni zetu, Mheshimiwa Mbunge anayetarajia kutoa mabadiliko katika Muswada, hutoa hoja yake hiyo wakati wa hatua ya Bunge likiwa limekaa kama Kamati. Hoja hiyo

hujadiliwa na hutolewa uamuzi wa Bunge kukubali au kuikataa. Siku hiyo ya tarehe 7 Februari, 2005, hoja zilizotarajiwa kutolewa nyingine zilijadiliwa na kutolewa uamuzi na Bunge na zile ambazo zilikosa watu wa kuziwasilisha, ambazo zilikuwa zimetokea upande wa Upinzani, hazikujadiliwa kwa sababu hapakuwa na wa kuziwasilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge, ana haki na uhuru wa kupiga kura ya ndiyo, hapana au ya kutokushikamana na upande wowote. Aidha, Mheshimiwa Mbunge, anaweza kutoka nje ingawa namna ya ustaarabu ni kupinga kwa kupiga kura ya hapana. Mimi sina tatizo na hatua waliyoichukua Wabunge wa Upinzani waliotoka nje, tatizo langu ni sababu zilizotolewa na baadhi yao walipoulizwa na waandishi wa habari. Sababu iliyotolewa ni kuwa, walitoka nje kwa sababu hoja zao walizoleta za kuleta mabadiliko katika Muswada zilikataliwa. Jambo hili lisiposahihishwa, umma wa Watanzania unaweza ukafikiri kuwa Wabuge wa Upinzani wanazuiliwa kutekeleza majukumu yao ya uwakilishi na Bunge, Serikali au Wabunge wa CCM. Hili siyo kweli. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge hao wa Upinzani, hawakusubiri hatua ya Kamati ili wawasilishe hoja zao ili kila hoja ijadiliwe na kutolewa uamuzi. *(Makofi/Kicheko)*

Narudia sehemu hii, "Waheshimiwa Wabunge hao wa Upinzani hawakusubiri hatua ya Kamati ili wawasilishe hoja zao ili kila hoja ijadiliwe na kutolewa uamuzi." *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ukikimbia kabla ya kuwasilisha hoja yako, utasemaje hoja yako imekataliwa? Kama Waheshimiwa Wabunge waliotoka nje walifanya hivyo kwa kutokujua, basi tunatoa pole na Mheshimiwa Spika, semina juu ya Kanuni za Bunge inahitajika. Nimetoa ufafanuzi huu ili umma usiendelee kuwa na tafsiri potofu juu ya kilichotokea. Bunge lako Tukufu linaendeshwa kwa kufuata Kanuni na siku zote nguvu za hoja hutumika badala ya hoja za nguvu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ninalotaka kuligusia ni kuhusu Muungano wetu. Nataka nikumbushe tena kuwa, Muungano wa Tanzania ni Muungano wa Watanzania wa Bara na wa Zanzibar, tusidhani ni chombo chetu sisi viongozi na tukakitumia tunavyotaka. Watanzania wa pande zote za Muungano wana faraja na Muungano wao na wana maslahi na manufaa na Muungano wao. Watanzania wa Bara wanahitaji wenzao wa Zanzibar na Watanzania wa Zanzibar wanawahitaji wenzao wa Bara, wamekaa hivyo kwa zadi ya miaka 40 hawatengamani. Wapo watu hasa sisi viongozi wanaozungumza sana juu ya kero ya Muungano kana kwamba, kuna jambo la ajabu limetokea. Hata kama kusingelikuwa na Muungano, ndani ya Tanzania Bara, kungekuwa na matatizo ili mradi tu hali ya umaskini bado ni kubwa. Kwa upande wa Zanzibar vivyo hivyo, kungekuwa na matatizo ama baina ya Unguja na Pemba au hata ndani ya Unguja au Pemba yenyewe hata kama Muungano usingelikuwepo. Matatizo ndani ya Muungano yapo na yataendelea kuwepo ili mradi tunakubali kuwa maendeleo ni mchakato. La msingi ni kuwa matatizo yetu tunayashughulikia. Nataka tuelewe wazi

kuwa katika Muungano wetu, pande zote mbili za Muungano zinajitegemea na wala hakuna anayebebwa wala anayembeba mwenzake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi sasa tunazungumzia uwezekano wa Muungano wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Nchi hizi zitakapoungana, zitahitaji kujifunza sana kutoka Muungano wetu wa Tanzania, vinginevyo waende wapi? Hata katika huo Muungano huo wa Afrika Mashariki kutakuwa na matatizo mengi bila shaka kuliko tuliyonayo sisi. Naomba Watanzania tujivunie Muungano wetu na hatutaruhusu mtu yeyote kuuchezea Muungano wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu la kukumbushana tu ni juu ya umahiri wetu wa kutumia Kiswahili. Tarehe 10 Februari, 2005 zilifanyika sherehe za Maadhimisho ya Siku ya Kiswahili, ambapo watu binafsi na Taasisi zilitunukiwa tuzo kwa mchango wao katika kukienzi na kukiendeleza Kiswahili. Napenda kutumia fursa hii, kuwapongeza kwa dhati wale wote waliotunukiwa tuzo hizo. Aidha, nalipongeza Baraza la Kiswahili la Taifa, kwa juhudi zake za kukuza na kuendeleza Kiswahili. Wito wangu kwa Watanzania wote ni kuwa tuitumie siku ya Kiswahili kama nafasi yetu ya kuipa lugha yetu ya Taifa msukumo zaidi kwa kuendelea kusisitiza na kuhimiza matumizi sahihi ya Kiswahili.

Napenda kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge kuwa, Kiswahili ndiyo lugha yetu ya Taifa na kule kukubaliwa kwake kama lugha mojawapo rasmi ya Umoja wa Afrika ni faraja kubwa kwetu Watanzania. Hivyo ni vema sisi Wabunge tukawa mstari wa mbele kwanza, katika kukitumia na pili, katika kukitumia kwa usahihi Kiswahili. Bunge lako bado halijawa mfano mzuri wa matumizi ya Kiswahili kizuri, licha ya kuwa sio vizuri kuchanganya lugha mbili katika sentensi moja na ni kosa kutumia lugha mbili katika neno moja. Sisi tunapoongea ndani ya Bunge, wanaotusikiliza ni pamoja na Wananchi wa kawaida, tunapochanganya lugha wengi wanashindwa kufuatilia tunayoyazungumzia ndani ya Bunge lako Tukufu. Tukumbuke kuwa yote tunayoyajadili hapa ni kwa faida yao. Leo sitatoa mifano ya jinsi lugha ya Kiswahili ilivyovurugwa hapa Bungeni, lakini hali hii ipo hata katika Ofisi za Serikali. Watanzania kama wenye lugha hii ya Kiswahili ni vema tukawa na fahari nayo kila mahali. Naomba tutumie Kiswahili fasaha kwa kadri inavyowezekana na hasa ndani ya Bunge letu hili Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika, Mheshimiwa Juma Jumaldin Akukweti, Mbunge wa Tunduru, Wenyeviti, Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mbunge wa Mbozi Magharibi na Mheshimiwa Anne S. Makinda, Mbunge wa Njombe Kusini, kwa kutuongoza vema katika Mkutano huu. Nawashukuru vilevile Wafanyakazi wa Ofisi ya Bunge, chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge, Ndugu Damian Foka, kwa huduma mbalimbali zilizowawezesha Waheshimiwa Wabunge, kutekeleza kwa ufanisi kazi zote zilizopangwa katika Mkutano huu. Ninaendelea kumpongeza sana Katibu wetu mpya, Ndugu Damian Foka, kwa sababu Waheshimiwa Wabunge, hawajapungukiwa katika huduma wanazozihitaji pamoja na ugeni wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru vilevile wafanyakazi wote wa Serikali, kwa kuiwezesha Serikali kutekeleza wajibu wake kwa ufanisi katika Mkutano huu. Vilevile

navishukuru vyombo vya habari, kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kutoa habari kuhusu kazi zilizokuwa zinatekelezwa na Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawatakia Waheshimiwa Wabunge, kazi njema ya kumalizia malizia kipindi hiki kinachoelekea ukingoni. Naomba tukasimamie yote tuliyoyazungumza, hasa suala la uandikishaji katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, kwa wale ambao bado na Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu. Najua hata Majimboni joto ni kali, lakini ninaamini mtalihimili. Nawatakia safari njema na kazi njema. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kutoa hoja kuwa Bunge lako Tukufu liahirishwe hadi siku ya Jumanne, tarehe 12 Aprili, 2004, litakalokutana tena saa 3.00 asubuhi hapa Mjini Dodoma.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naona *camera* zimehamia huku kwa haraka haraka kuwamulika wale watakaosema siyo. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijawahoji nikumbushe tu kwamba, kabla ya Mkutano ujao wa Bunge, kuna Vikao vya Kamati, ratiba nimeshawagawia. Nikumbushe tu kwamba, Vikao vya Kamati zote za Bunge vinaanza tarehe 29 Machi, 2005, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mjiandae kuwasili Dar es Salaam, tarehe 28 Machi, 2005 ili tarehe 29 Machi, 2005 kazi iweze kuanza.

Sasa tuamue hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ya kuahirisha Bunge mpaka tarehe 12 Aprili, 2005.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Kwa hiyo, walioafiki wameshinda, Bunge linaahirishwa mpaka tarehe 12 Aprili, 2005. *(Kicheko)*

*(Saa 11.52 jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne tarehe 12 Aprili, 2005 Saa Tatu Asubuhi)*